NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## Kikao cha Tatu – Tarehe 5 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 38, Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuwepo Dodoma huwa kuna maswali kwa Waziri Mkuu na pia tunaongozwa na Nyongeza ya Sita lakini Mheshimiwa Spika alikwishakutoa maelekezo siku Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuwa na hoja yake mbele yetu anapaswa kupewa nafasi kwa ajili ya hoja hiyo. Kwa hivyo, leo Waheshimiwa Wabunge hakutakuwa na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa George Malima Lubelege, Mbunge wa Mpwapwa sasa aulize swali lake.

Na. 20

**Ubovu wa Barabara ya Mima hadi Mkanana**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Mima hadi Mkanana ni mbaya sana na inapitika kwa shida sana wakati wote; na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa haina uwezo kifedha wa kuifanyia mategenezo makubwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara hiyo ili iweze kupitika wakati wote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mima hadi Mkanana ni barabara mlisho ya tabaka la udongo yenye urefu wa kilometa 26.5, inayounganisha barabara ya Kibakwe hadi Wotta yenye urefu wa kilometa 26 na barabara ya Gulwe hadi Seluka yenye urefu wa kilometa 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Vijiji vya Mima na Mkanana. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 shilingi milioni 40.84 zilitumika kufanyia matengenezo ya sehemu korofi urefu wa kilometa nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019, *TARURA* imetenga shilingi milioni 57 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi urefu

wa kilometa 6.5 na matengenezo ya kawaida urefu wa kilometa 10 ili iweze kupitika kwa wakati wote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Malima Lubelege, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tarehe 30 Desemba, 2017, Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo alitembelea Kijiji cha Mima na kuona barabara ya Mima ilivyo mbaya na nilimwonyesha ni barabara ya kwenda Mkanana, ile barabara kilometa 26 zote ni mawe matupu wala hakuna udongo kule, yote ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaposema anatengeneza eneo korofi, hili eneo lote kubwa linalobaki atatengeneza nani na wananchi wa Mkanana, Kibwegele wana shida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alipotembelea Mpwapwa tarehe 30 Desemba alikakuga barabara ya lami kilometa moja Mjini Mpwapwa na aliwaahidi wananchi wa Mji wa Mpwapwa kwamba kilometa zote 10 watazijenga kwa kiwango cha lami. Mbona sijaiona bajeti hii ya kujenga barabara za lami Mpwapwa Mjini kilometa 10? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lubeleje, *senior MP,* ambaye mimi huwa napenda kumuita greda la zamani makali yaleyale kutokana na kazi yake kubwa anayoifanya kule Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nikiri wazi kwamba nilikuwa na Mheshimiwa Lubeleje katika Jimbo lake na ni kweli barabara ile ina changamoto kubwa na hata siku ile

tulivyoenda kukagua kituo cha afya cha Mima tulitumia muda mrefu sana kutokana na changamoto za barabara ile. Hata hivyo, niliwaagiza wataalam kwamba wafanye uchambuzi wa kutosha nini kifanyike katika barabara ile, maana ukiangalia wigo wake, siyo hiyo peke yake, barabara hizo zote ambazo anazizungumzia Mzee Lubeleje ziko katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa bajeti iliyokuwepo hapa ni ndogo lakini kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini *(TARURA)* tunaziweka katika mpango wa utekelezaji maalum kwa kuzitafutia fedha kwa sababu eneo lile lina changamoto kubwa. Kwa hiyo, naomba nimwombe Mheshimiwa Lubeleje avute subira kwani ofisi yetu inafanya kazi kwa sababu wataalam nimewatuma kufuatilia kazi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za Mji wa Mpwapwa, ni kweli, mpango uliokuwepo pale ni takribani kilometa tano lakini mtandao wote wa barabara ya lami ni karibu kilometa 10 Mjini Mpwapwa. Hivi sasa wakandarasi wanaendelea na kazi na katika mpango wa bajeti ya mwaka huu, majibu ya Naibu Waziri alipokuwa anazungumza hapa ambayo ni mazuri sana yalikuwa yakijibu suala zima la Mtanana lakini suala la mtandao wa barabara za lami katika mpango wa bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Lubeleje ataona jinsi gani Serikali imejipanga kutekeleza mpango ule wala asiwe na hofu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selasini, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mvua zinazoendelea zimeharibu barabara nyingi sana za vijijini karibu nchi nzima mfano katika Jimbo langu la Rombo barabara nyingi sana za vijijini hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua *TARURA* inafanya kazi nzuri sana sasa hivi katika baadhi ya majimbo. Natambua pia kwamba kuna bajeti itasomwa hapa kwa ajili

ya kuiwezesha *TARURA* kuendelea na kazi zake. Je, Serikali ina mpango wowote wa dharura wa kuisaidia *TARURA* ili iweze kuwezesha barabara ambazo zimevunjika vijijini kupitika kwa sasa hivi ili wananchi waweze kupeleka mazao yao katika masoko na kadhalika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mvua zimenyesha kubwa katika maeneo mengi na kila neema inavyokuja huwa inakuwa na adha yake. Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika kwa vipindi vyote. Ni vizuri tukapata fursa ya kufanya uthamini maeneo ambao yameharibiwa na mvua ili hatua za dharura ziweze kuchukuliwa na wananchi wetu wasiweze kuendelea kupata shida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali dogo la nyongeza. Kuna ahadi nyingi tuliwaahidi wananchi wetu wakati tukiomba kura ikiwemo Mheshimiwa Rais kuahidi wananchi wa Itigi kuwajengea barabara ya lami inayoingia katika Mji wa Itigi kilometa nane. Je, ni lini sasa Wizara hii itatekeleza ahadi hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna ahadi nyingi ambazo zilitolewa wakati wa kampeni na yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge alitoa ahadi zake na Mheshimiwa Rais alitoa ahadi katika maeneo ambayo alienda kuomba kura. Katika kipindi ambacho aliomba na kutoa ahari ahadi utekelezaji wake ni

ndani ya miaka mitano. Upo utaratibu ambao umewekwa mahsusi ili kuhakikisha kwamba ahadi zote ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Rais zitaenda kutekelezwa. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, Ilani ya CCM inatekelezwa ndani ya miaka mitano na sisi ni waungwana tukiahidi huwa tunatekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiula, swali la nyongeza.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Yulansori, Lelembo wanapata shida kubwa ya barabara na Halmashauri haina uwezo kama ilivyo kwa wananchi wa Mpwapwa na kwa bahati nzuri Waziri wa TAMISEMI alishatembelea maeneo hayo, je, Serikali ina kauli gani kuwasaidia wananchi hawa ambao ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya mahindi, alizeti na vitunguu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilifika maeneo yale mimi na Mbunge tumetembelea barabara ile yenye kilometa 25.2. Kwa sababu changamoto za barabara ile ni kubwa kwani mmomonyoko umekuwa mkubwa kwa bajeti ya kawaida imekuwa ni jambo kubwa sana. Tuliwaelekeza wataalam wafanye upembuzi yakinifu wa barabara ile na inaonekana kuna madaraja na ukibadilisha kuweka tabaka la kifusi, bahati nzuri taarifa hizo zipo katika Ofisi yetu na katika mpango wa bajeti wa mwaka 208/2019 barabara ile ni miongoni mwa barabara za kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu unaokuja barabara ile tunaenda kuishughulikia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara inayounganisha Mkoa wa Iringa na Morogoro ni moja tu inapitia Kitonga; na kwa kuwa hoja hii nilishawahi kuileta kwamba siku itakapotokea barabara ya Kitonga imefunga kwenda Zambia na Afrika ya Kusini itabidi watu wazunguke Dodoma. Kwa kuwa wananchi wa Kilolo wa Kata ya Muhanga, Masisiwe, Idete, Itonya, Kimala wameanza kwa makusudi kabisa kupasua barabara ambayo Serikali ilishaahidi kuunganisha Mkoa wa Morogoro na kutokea kwa Mheshimiwa Susan Kiwanga, wamefanya jitihada kubwa, je, Mheshimiwa Waziri atakubali kuitembelea na kutuunga mkono ili wananchi waweze kupata nguvu na kuimalizia barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, nilivyofika katika Halmashauri na Jimbo la Kilolo, Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kilolo walizungumzia *concern* ya barabara hiyo. Kwa sababu jukumu letu kama Serikali ni kubwa ni kutoa huduma kwa wananchi, nami nilieleza wazi kwamba ni jukumu la Serikali kushughulikia barabara hii. Kwa sababu barabara hii itadondokea kwa wenzetu wa *TANROARD,* lakini ni Serikali yetu yote kwa ujumla, tutaangalia nini cha kufanya kwa ajili ya kuipa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pia siku ile wananchi walisema endapo barabara ile ikijifunga watashindwa kusafiri lakini hatuwezi kutoa ahadi ya moja kwa moja hapa. Niseme Serikali tumelichukua kwa ujumla wake na kuliweka miongoni mwa mipango mikakati ili siku za usoni barabara ile ikiwezekana tuiboreshe kwa huduma pana ya wananchi wa Tanzania lakini hata nchi jirani.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 21

**Kupata Hati Rasmi ya kuwa Hospitali ya Wilaya - Hospitali ya Manyamanyama**

**MHE. AGNESS M. MARWA** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la dawa katika Hospitali ya Manyamanyama iliyoko Wilayani Bunda na hii ni kutokana na hospitali hiyo kutokuwa na hati rasmi ya kuwa Hospitali ya Wilaya:-

(a)Je, ni lini Serikali itaipa Hospitali ya Manyamanyama Hati rasmi ya kuwa Hospitali ya Wilaya ili kuongeza mgao wa dawa na kupunguza shida kubwa wanayoipata wananchi?

(b)Je, ni lini Serikali itaongeza Waganga na Wauguzi katika hospitali hiyo ili kuongeza ufanisi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Manyamanyama hakijakidhi vigezo vya kupewa hati ya kuwa Hospitali ya Wilaya kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na timu ya ukaguzi kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto uliofanyika mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu uliobainika ni pamoja na ukosefu wa jengo la utawala; jengo la huduma za mionzi; jengo la kliniki ya macho; jengo la huduma za dharura; jengo la kufulia; ujenzi wa wodi ya upasuaji ya wanaume na wanawake; jengo la ufundi wa vifaa vya hospitali kwa maana (karakana); jengo la kuhifadhia maiti

na nyumba za watumishi. Hivyo, kituo hicho kitapata hadhi ya kuwa hospitali endapo miundombinu yote inayohitajika itakamilika ili huduma za msingi zenye hadhi ya hospitali ziweze kutolewa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya watumishi wa afya katika Kituo cha Afya Manyamanyama ni 165, watumishi waliopo ni 78 na upungufu ni watumishi 87. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, kituo kimepokea watumishi watano (5) akiwemo Daktari mmoja. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri imeomba kibali cha kuajiri watumishi wa afya 48 ili kupunguza pengo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Bado sijaridhishwa na majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri. Kutokana na sintofahamu ya wananchi hao wa Bunda, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri, nina *evidence* hapa nisome. Kutokana na kituo hicho cha afya kwa mwaka 2006, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ni Rais Mstaafu aliweka jiwe la msingi. Aliweka jiwe la msingi ili kusudi huo upembuzi yakinifu na hivyo vitu vingine vikikamilika ipewe hati ya kuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya huo upembuzi yakinifu anaousema hapa Mheshimiwa Waziri, mochwari imeshatengenezwa tayari na ipo, chumba cha dharura Mheshimiwa Waziri kipo, *X-Ray* tayari ipo, *Ultra Sound* tayari ipo na barua hii nitamkabidhi nikitoka hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, ya Wilaya ile lakini pia chumba cha dhararu kipo. Je, ni nini sasa kinachosababisha hii Wilaya ya Bunda na hicho Kituo cha Manyamanyama kisipewe hadhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa usimamizi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Bibi Janet Mayanja akiwa na Madiwani wake chini ya Mwenyekiti wa Halmashauri kutokana na mapato na makusanyo ya

Halmashauri wameweza kuweka vitu hivyo na vinginevyo. Ni kwa nini sasa hospitali hiyo isipewe hati? Kama mnatuelezea kwamba vituo vya afya vinatakiwa vibaki palepale ziwepo Hospitali za Wilaya, Mheshimiwa Waziri naomba majibu leo kwamba kama fedha ipo... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness ni kama unajijibu mwenyewe sasa. *(Kicheko)*

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali bado halijakwisha, naomba Mheshimiwa Waziri niambiwe kwamba ni lini sasa na sisi mtatuletea hiyo pesa ya kujenga Hospitali ya Wilaya ili tujue kile ni kituo cha afya? Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali naomba majibu ya kutosha. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli idadi ya wagonjwa wanaokwenda kupata huduma katika Kituo cha Afya cha Manyamanyama ni wengi sana na ndiyo maana kumekuwa na *concern* ya kwamba ni vizuri kituo cha afya kile kikapandishwa hadhi ya kutoka kituo cha afya kikawa hospitali ya wilaya. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba uhitaji wa vituo vya afya bado uko pale pale na ujenzi wa hospitali za wilaya bado uko pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na kazi nzuri ambayo anaifanya ya kuhakikisha afya za watu wake zinaimarika, ni vizuri tukahakikisha tunaheshimu ramani inayohusu hospitali ya wilaya ambayo ni tofauti na ramani inayohusu kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hospitali za wilaya ambazo tunakwenda kuzijenga kwa mwaka wa 2018/2019, *Bunda DC* ni miongoni mwa Wilaya ambazo zinakwenda kupata hospitali za wilaya. Kwa taarifa nilizonazo *Bunda DC*

na Bunda Mji, *Bunda DC* mpaka sasa hivi bado hawajajua wapi Halmashauri yao itakuwa. Kwa hiyo, pesa hiyo ambayo itakuwa ipo tayari kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya busara itumike ili pale ambapo papo tayari tuanze kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata fursa ya kuongea na Mkurugenzi jana, pamoja na Kituo cha Afya cha Manyamanyama tayari Halmashauri imeanza kutafuta eneo lingine la ukubwa wa hekari 40. Kwa hiyo, *thinking* yao ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na eneo mbadala kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka, swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Bunge lililopita niliuliza swali kuhusiana na hospitali ya wilaya ambayo tulikuwa tumeambiwa kwamba itajengwa katika Kata ya Chipaka kwenye Kijiji cha Chipaka. Sasa hivi inaonesha kwamba kuna mabadiliko ambayo yanataka kufanyika hospitali ile ikajengwe maeneo mengine ambayo hayana majengo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo tulilokuwa tumeliteua ni eneo ambalo lilikuwa na majengo ambayo yalikuwa yanatumika kwa ajili ya mradi wa kujenga barabara kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, kuna majengo zaidi ya 20, leo hii wanataka kupeleka maeneo ambayo hayana majengo kabisa. Mheshimiwa Waziri aliniambia hapa atahakikisha kwamba analifuatilia jambo hili na hospitali inajengwa eneo ambalo walikuwa wametuambia kwamba ni lazima itajengwa pale. Je, amefuatilia na anatoa majibu gani kwa wananchi wa Tunduma ili wawe na uhakika wa hospitali katika eneo la Chipaka na Kata ya Chipaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Marwa nimeeleza kwamba ramani kwa ajili ya hospitali za wilaya ambazo zimekuwa *designed* na Ofisi ya Rais, TAMISEMI zinajitosheleza. Katika pesa ambazo tunakwenda kuanzia tunakwenda kuanza na jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ramani ambayo ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa asingependa tukaenda kwenye majengo ambayo hayakidhi ramani ambazo tunazo, ni vizuri tukapeana nafasi na naamini na yeye mwenyewe akiona ramani pendekezwa ataafiki kwamba ni vizuri majengo yale yakatafutiwa kazi nyingine, lakini sisi tungependa tujenge hospitali ya wilaya yenye hadhi ya kulingana na Mheshimiwa Mbunge ambaye anatoka Tunduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa matatizo yaliyoko kule Manyamanyama hayana tofauti sana na matatizo yaliyoko kwenye Jimbo la Geita. Mwaka jana mwezi Machi, Waziri wa Afya alikipandisha Kituo cha Afya Nzela na kuwa hospitali ya wilaya kwa kuwa Wilaya ya Geita haina hospitali ya wilaya lakini kumekuwa na mkanganyiko kati ya TAMISEMI na Wizara ya Afya na Waziri hajawahi kutembelea eneo lile akaliona pengine akawa na huruma kama alivyopata huruma ya Waziri wa Afya. Je, ni lini Waziri wa TAMISEMI ataambatana na mimi kwenda kuona kituo kile kilichopandishwa hadhi na majengo na ubora ulioko pale ili aweze kuridhia na mambo yaende mbele? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nipongeze majibu mazuri ya Naibu wangu, Mheshimiwa Kandege aliyoyatoa katika maswali ya awali yaliyojitokeza, hata hivyo, naomba kujibu swali la mtani wangu Mheshimiwa Musukuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuambatana, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwanza aondoe hofu, kama tulivyokwenda katika Jimbo lake na katika Mkoa wa Geita mara nyingi na kufanya kazi kubwa sana, nimwambie mara baada ya Bunge hili la bajeti nitaomba twende kwa ziara maalum kwa sababu Mkoa wa Geita miongoni mwa mambo tunayokwenda kuyafanya ni ujenzi wa hospitali zingine za wilaya katika mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kila sababu kufika Geita kuangalia maeneo muafaka wapi tutajenga hospitali hizo kwa manufaa mapana ya watani zangu Wasukuma wa Mkoa wa Geita ili waweze kupata huduma nzuri ya afya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Musukuma asihofu tutaondoka pamoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nadhani na hivi Mwenge umewashwa Geita utakuwa umemsaidia Mheshimiwa Musukuma kumulika huko. Mheshimiwa Felister Bura, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kutupa fedha kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya cha Bahi. Kituo hiki kinawahudumia wananchi wengi sana kwa sababu mji ule unaendelea kupanuka kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilonalo, upanuzi unafanyika lakini hatuna vitendea kazi, watumishi walioko pale ni Manesi wanne tu na yuko Daktari mmoja na Matabibu wachache sana ambao hawakidhi mahitaji ya wagonjwa wanaokwenda katika kituo kile cha afya. Ni lini sasa Serikali

italeta watumishi na vitendea kazi vya kutosha kwa ajili ya huduma za Kituo cha Afya cha Bahi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimshukuru Mheshimiwa Bura kwa sababu yeye amekuwa Msemaji wa Mkoa wa Dodoma kwa nafasi yake ya Viti Maalum na anautendea haki sana mkoa huu. Naomba ku-*declare interest,* jengo ambalo tumemaliza hivi sasa katika Hospitali ya *General,* amefanya kazi kubwa sana kuhakikisha tumepeleka pesa na hivi sasa tumepeleka karibuni shilingi bilioni mbili hospitali ile inapata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, eneo la Bahi kweli tumeboresha kituo kile cha afya lakini siyo hivyo tu kwa kelele zake na za Mbunge wa Bahi mwaka huu tunakwenda kuanza ujenzi wa hospitali mpya za Wilaya za Bahi, Chemba pamoja na Chamwino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo, wenzetu kupitia Utumishi kabla ya Juni, kuna mpango mkakati kupata watumishi wapya katika sekta ya elimu na sekta ya afya. Pia kwa vile tunajua Bahi ni pumulio la makao makuu yetu ya nchi kwa maana ya hapa Dodoma tutajitahidi kuhakikisha tunawapeleka watumishi wa kutosha ikiwa lengo kubwa ni wananchi wa eneo lile waweze kupata huduma vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mipata, swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Bunge lililopita nilisimama hapa nikauliza juu ya *support* ya Serikali katika ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kasu, nikajibiwa kwamba siyo muda mrefu pesa zitapelekwa zaidi ya shilingi milioni 500. Nataka kujua, ni lini Serikali sasa itapeleka pesa hizo maana nimetoka Jimboni bado hatujazipokea pesa hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ya Serikali kupeleka pesa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kasu ni mara pesa itakapopatikana kwa sababu ni ahadi ambayo tumeiweka na tuko *very firm* katika hilo. Tutahakikisha katika mgao wa awamu inayofuata na kituo chake cha afya kinapata mgao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi, katika wilaya ambazo zinaenda kujengewa hospitali za wilaya ni pamoja na wilaya yake. Kwa hiyo, naamini adha ambayo wananchi wa Nkasi wamekuwa wakiipata kuhusiana na suala zima la matibabu litapungua muda siyo mrefu sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Anthony Komu.

Na. 22

### Bandari ya Kigoma kuwa *Port of Destination-CIF*

**MHE. ANTHONY C. KOMU (K.n.y. MHE. ZITTO Z. R. KABWE)** aliuliza:-

Mnamo tarehe 26 Julai, 2017, Mawaziri wa Uchukuzi wa Uganda, Burundi, Congo DRC na Tanzania walifanya mkutano katika Manispaa ya Ujiji-Kigoma na kuazimia kuwa kuanzia Januari, 2018, Bandari ya Kigoma itakuwa bandari ya mwisho kwa bidhaa ya Burundi na Mashariki ya DRC (Kigoma *Port of Destination CIF* Kigoma). Pamoja na Azimio hilo, mradi wa Bandari ndogo za Ujiji na Kibirizi zilipaswa

kujengwa na kuiwezesha miradi kama ya *Ujiji City-Great Lakes Trade and Logistics Centre:-*

Je, Serikali mpaka sasa imefikia hatua gani ya kiforodha na kibandari kuiwezesha *CIF*-Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Mkutano wa Mawaziri wa Uchukuzi wa Uganda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Tanzania waliazimia kuwa kuanzia Januari, 2018 Bandari ya Kigoma itakuwa Bandari ya mwisho kwa bidhaa za Burundi na Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo yaani Kigoma *Port of Destination.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa bandari hii pia ni muhimu sana kwa uchumi na ustawi wa Mkoa wa Kigoma na ndiyo inategemewa na wananchi wa Mkoa wa Kigoma na Mikoa ya jirani katika utaoji wa huduma ya usafirishaji wa bidhaa zinazopitia reli ya kati kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi jirani za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo tena kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulitambua hili, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari - Tanzania katika mwaka wa fedha 2017/2018 imetenga fedha kwa ajili ya kuendeleza Bandari ndogo za Ujiji na Kibirizi ili zikikamilika ziwezeshe miradi kama vile Ujiji *City –Great Lakes Trade and Logistics Centre.* Zabuni za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa bandari hizi zilitangazwa. Hata hivyo, kwa bahati mbaya hakuna mzabuni hata mmoja aliyejitokeza kuomba kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Machi, 2018, *TPA* imetangaza upya zabuni hizo Kimataifa ili kumpata mzabuni atakayefanya kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na athari za kimazingira. Zabuni hizo zimefunguliwa tarehe 3 Aprili, yaani juzi na jumla ya makampuni 21 yameonyesha nia ya kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kazi inayoendelea ni kufanya tathmini ya wazabuni ili kumpata mzabuni anayefaa kufanya kazi hiyo. Ni matarajio yetu kuwa kazi itaanza mara baada ya kumalizika kazi ya tathmini na kumpata mkandarasi wa kufanya kazi hiyo na hivyo kunyanyua kiwango cha utendaji wa Bandari ya Kigoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anthony Komu, swali la nyongeza.

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba bandari hii au mradi huu ni wa muhimu na utaleta nafuu kubwa sana kwa wananchi wa Kigoma, naomba Serikali iwaambie watu wa Kigoma, kwa kuwa mradi huu umeshachelewa sana, imetenga kiasi gani kwa bajeti inayokuja kwa ajili ya kuhakikisha sasa mradi huu unaanza mara moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kule Moshi tuna tatizo kama hili la Kigoma, tuna Stendi ya Kimataifa inapaswa kujengwa pale na Benki ya Dunia iko tayari kutoa fedha. Nataka nijue kutoka Serikalini, ni lini kibali kitatoka kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hiyo li tuweze kunufaika na huo msaada kutoka *World Bank?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayofanyika sasa hivi kama nilivyoeleza katika jibu la msingi ni kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hiyo ikishakamilika

wale ndiyo watatupa gharama zinazostahili kufanya kazi husika na ndipo tutakapojua tunatumia gharama gani katika ujenzi wa hiyo sehemu ambayo Mheshimiwa Mbunge anaifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili kuhusu stendi, nikiri kwamba umuhimu wa kuwekwa stendi hiyo ni mkubwa sana kwa sababu ni kweli Benki ya Dunia imeonesha nia ya kufadhili. Hata hivyo, bado Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia kuangalia namna nzuri itakayofanya ili kuhakikisha ujenzi wa stendi hiyo unafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Swali hili lina umuhimu wa pekee kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na napenda nimuulize swali moja dogo Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Bandari za Ujiji na Kibirizi unakwenda sambamba na ujenzi wa Bandari ya Nchi Kavu ya Katosho ambayo tayari Serikali imeshalipa fidia kwa wananchi wale. Napenda kujua, je, ujenzi wa Bandari ya Nchi Kavu ambayo tayari Serikali imeshalipa fidia wananchi wale unaanza lini maana sasa ni takribani mwaka mmoja tangu wananchi wale wamelipwa fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani za dhati kwa jinsi anavyojitahidi kupigania bandari za mkoa ambao anatokea. Ni kweli kwamba wakati huu mchakato wa usanifu wa kina na upembuzi yakinifu ukiwa

unaendelea tayari Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imekwishatangaza tenda kwa ajili ya kuanza ukarabati wa gati katika eneo la Kibirizi na Ujiji pamoja na Ofisi ya Meneja wa Mkoa wa *TPA* ili vyote viende sambamba kwa tenda moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Katosho nalo limeingizwa katika *package* ya peke yake ya kuanza kujenga sakafu kubwa ili treni inapopita pale kabla ya kufika kituo cha mwisho cha Kigoma iweze kuanza kushusha mizigo ambayo itakuwa inaweza kusafirishwa kwenye nchi jirani na maeneo ya mikoa ya jirani ikiwemo Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Mbarouk, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Tarehe 5 Agosti, 2017 wakati Rais alipokuja kuweka jiwe la msingi la bomba la mafuta pale Chongoleani-Tanga, tarehe 6 alizundua Kiwanda kipya cha Saruji cha Kilimanjaro na alinipa nafasi ya kuongea kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimtaka Mheshimiwa Rais kupitia Serikali ya Awamu ya Tano kufanya *categories* za mizigo katika bandari zetu. Nataka kujua, mpango ule umeishia wapi kwa sababu Bandari ya Tanga sasa hivi inafanya kazi chini ya kiwango na hata vifaa vya kisasa vya kuteremsha makontena ya *fourty feet* hakuna, Waziri ananiambiaje?

**NAIBU SPIKA:** Tanga naona kuna Kiswahili kigumu sana, ulimtaka Mheshimiwa Rais? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Mbunge ni mfuatiliaji mzuri nadhani atakuwa shahidi

kwamba sasa hivi Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imekwishaanza marekebisho na matayarisho ya kupanua Bandari ya Tanga. Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba Bandari ile ya Tanga inakwenda sambamba na wingi wa mizigo ambayo inategemewa kuanza kupatikana kupitia ujenzi wa bomba la mafuta la Hoima. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge asiwe na mashaka kuna utekelezaji wa upanuzi wa Bandari ya Tanga unaoendelea na wakandarasi wako pale wameshaanza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa, tutaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Vitendo vya Udhalilishaji kwa Watoto**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutokomeza vitendo vya udhalilishaji kwa watoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua ukubwa wa tatizo la udhalilishaji kwa watoto katika jamii na imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana nalo ikiwemo kuhamasisha wananchi kutoa taarifa za matukio ya aina yoyote ya udhalilishaji kwa watoto wakiwemo watoto wa kike. Kupitia Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009, Serikali imekuwa ikielimisha jamii wakiwemo wazazi na walezi

kuelewa wajibu wao wa kuripoti matukio ya udhalilishaji punde yanapotokea. Sheria hii imeelekeza kutolewa kwa adhabu kali kwa watuhumiwa wote wanaopatikana na hatia ya udhalilishaji wa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 ambao unaisha mwaka 2021/2022 umeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa. Kamati hizi wajumbe wake wamehusisha Idara za Mahakama, Jeshi la Polisi, Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii pamoja na Idara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti matukio ya udhalilishaji katika maeneo husika na kuyashughulikia kisheria. Aidha, Wizara imekwishatoa mafunzo ikiwamo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii wapatao 50 kutoka katika mikoa yote 26. Ili kuratibu uanzishwaji wa Kamati hizo, tayari mikoa tano wameshaanzisha Kamati hizo. Vilevile, Serikali imekwishaanzisha Madawati ya Jinsia na Watoto katika vituo 417 katika Jeshi la Polisi ili kuwezesha kushughulikia pamoja na masuala mengine vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya udhalilishaji watoto vinaweza kudhibitiwa pia kwa kupitia mtandao maalum wa mawasiliano kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali za udhalilishaji. Namba hiyo naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge inapatikana kupitia namba 116 na Waheshimiwa Wabunge wanaweza kupiga namba hiyo na kuwajulisha wapiga kura wao kuhusiana na namba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ya kutumia namba hii na mtandao huu ni kwa mtoto mwenyewe au mtu mwingine kwa niaba ya mtoto kuweza kuripoti tukio lolote la udhalilishaji wa mtoto. Mtandao huu huwasilisha taarifa la tukio hilo kwenye vyombo husika ambapo mwathirika hupata huduma stahiki za kiafya na unasihi na mtuhumiwa

kufikishwa katika mamlaka husika za kisheria. Katika kipindi cha Januari mpaka Disemba 2017, matukio 1,072 yaliripotiwa katika mtandao huu na kushughulikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, swali la nyongeza.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa vitendo hivi vinapotokea mara nyingi ushahidi wa awali haupatikani. Je, Serikali imejipanga vipi kutoa taaluma kwa wananchi nini kifanyike mara tu linapotokea jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali inachukua hatua za kutosha dhidi ya udhalilishaji huu lakini bado vitendo hivi vinaendelea kwa kasi kubwa katika jamii zetu. Je, Serikali haioni kwamba adhabu inayotolewa ni ndogo hivyo basi ilete sheria hapa Bungeni tuipitishe yeyote atakayepatikana na hatia ya kubaka mtoto mdogo ahasiwe? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, matukio mengi ya udhalilishaji sasa hivi yanakuwa *reported* na hii inaonesha kwamba mwamko wa jamii nao umeongezeka. Tumepanua wigo sana kupitia Idara zetu za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii pamoja na Jeshi la Polisi kwa kuanzisha Madawati ya kuweza kutoa taarifa kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini matukio mengi ya udhalilishaji dhidi ya watoto yamedhihirisha kwamba yanafanywa na watu wa karibu wa familia. Naendelea kutoa

rai kwa wanajamii na familia kuyatolea taarifa punde yale matukio yanapotokea na sisi ndani ya Wizara ya Afya pamoja na Jeshi la Polisi tumejipanga vizuri kuyashughulikia kwa uharaka zaidi pindi yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi kwa mujibu wa sheria udhalilishaji wa mtoto adhabu yake ni faini isiyozidi shilingi milioni tano na kifungo kisichozidi miezi sita ama vyote kufanyika kwa wakati mmoja. Sambamba na hilo, Serikali itaendelea kutafakari kwa kadri inavyoona inafaa kama kuna umuhimu wa kuongeza adhabu kutokana na matukio kama hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida Bakar, swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hili tatizo la udhalilishaji wa watoto sasa hivi limekuwa ni sugu ama ni donda ndugu yaani ni zaidi ya kila kitu na sisi wazazi inatuuma sana. Unaweza ukamuona mtoto anatoka mafunza mwanamume anamdhalilisha mtoto mchanga, hii iko sana kule kwetu Zanzibar, inauma sana maana hata wazazi wenyewe wengine wanawaingilia watoto wao. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa watu kama hao wanaofanya udhalilishaji wa watoto wetu hasa ikizingatiwa kwamba wakifanyiwa tatizo hilo wanaficha na wanamalizana wenyewe kule nyumbani hawapeleki taarifa kunakohusika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Bakar ambalo amelielezea kwa hisia kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria na Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, mtoto ana haki zake tano na naomba nizinukuu kwa faida ya

Waheshimiwa Wabunge. Mtoto ana haki ya kuishi; kulindwa; kuendelezwa; kushirikishwa na kutobaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na hilo, Serikali inakemea sana udhalilishaji wowote wa kijinsia dhidi ya mtoto. Ndiyo maana tumesema kwamba tumeweka mkakati wa kiserikali wa mwaka 2017/2018 ambao utaisha 2020/2021 na lengo na kusudio ni kuhakikisha kwamba tunatokomeza kabisa ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimetoka kusema kwamba udhalilishaji mwingi unafanyika katika ngazi ya familia. Naomba nitoe rai kwetu sisi Wabunge wote na jamii yote ambayo inaendelea kutusikiliza, tusiyafumbie macho matukio na udhalilishaji wowote dhidi ya wanawake na watoto na sisi kama Serikali tutaendelea kushirikiana na jamii kuchukua hatua za haraka kwa wote wanaofanya matukio kama haya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Udhalilishwaji wa watoto ni pamoja na watoto wa kike kutopata mahali pa kujisitiri katika shule zetu za msingi na sekondari. Serikali ilishatoa kauli kwamba shule zetu ziwe na vyumba maalum kwa ajili ya watoto wa kike kujisitiri wanapokuwa mashuleni lakini vyumba hivyo mpaka sasa havijakamilika. Ni kwa nini Serikali imeshindwa kusimamia kauli yake yenyewe wakati watoto wa kike wamekuwa wakidhalilika katika mazingira yao ya masomo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba watoto wa kike ambao wako shule wanahitaji sehemu ya kujisitiri wakati wakiwa katika siku zao.

Niseme tu kwamba hili tumeshaanza kulifanyia kazi kwa kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Elimu. Katika vyoo ambavyo sasa hivi tumeanza kuvijenga kwenye baadhi ya shule tumeshaweka utaratibu huo wa kuwa na vyumba na vyoo maalum kwa ajili ya watoto wa kike.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nashawishika swali hili kuwapa akinababa watuseme kidogo watoto wa kike, Mheshimiwa Silinde, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami niulize swali dogo la nyongeza. Moja ya udhalilishaji wa watoto ni watoto kuolewa wakiwa na umri mdogo na Serikali imekuwa ikitunga sheria tofauti kwa ajili ya suala hili. Hivi karibuni tumeiona Serikali ikienda Mahakamani kupinga watoto kuolewa zaidi ya miaka 18. Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo na yenyewe imekuwa iki-*entertain* udhalilishaji wa watoto kuolewa chini ya miaka 18? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde hilo swali ni la Naibu Waziri kweli wa Afya la kwenda Mahakamani? Nadhani hilo uliulize kama swali la msingi ili ajibu kikamilifu Waziri anayehusika kwa sababu yeye huyu siyo anayehusika kwenda Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na mikakati mizuri ambapo Wizara inahakikisha tunatokomeza hivi vitendo vya ubakaji nadhani Walimu wana nafasi kubwa ya malezi ya watoto wetu. Kwa nini tusiweke kipengele maalum kwenye mitaala yao jinsi ya kubaini na kuwafanyia *counseling* hawa watoto mara wanapobaini kuwa wamebakwa? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli jambo hili kwanza linakera na linaudhi lakini si muda mrefu tulikuwa na kikao cha Maafisa Elimu wote wa Mikoa na Wilaya na jambo hilo tumeliwekea msisitizo hasa katika suala zima la kuhakikisha kwamba, watoto wa kike wanalindwa. Hata hivyo, ushauri wa Mheshimiwa ni mzuri, Serikali tumeuchukua na tutakwenda kuufanyia kazi kwa kadri tutakavyoona inafaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu alitueleza kwamba kuna Madawati ya Jinsia 117. Hii inaonesha dhahiri kwamba kuna Wilaya nyingine hazina haya Madawati ya Jinsia. Ni ukweli kabisa kwamba kiwango cha ubakaji kwa maana ya watoto wa kike lakini na ulawiti wa watoto wa kiume kimekuwa kikiongezeka sana na tunajua sheria zipo. Ni kwa nini hawa watu wanaendelea kufanya hivi labda ni kutokana na mianya ambayo ipo kuanzia kwenye Jeshi la Polisi na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua kwa sababu sheria zipo lakini bado vitendo hivi vinaendelea, ni kwa nini sasa Serikali isije na njia mbadala kama tiba kabla ya hili tukio kutokea, kuwafanyia kama *counseling* hao wanaotenda kwa maana kwenye maeneo husika wazazi au jamii husika ili tuwe na tiba mbadala kabla ya tukio kutokea kwa sababu tunaona haya mambo yanatokea na sheria zipo ni kwa nini msibuni ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther umeshauliza swali lako. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali inafanya njia mbadala nyingi tu

na niweke tu kumbukumbu sawa kwamba Madawati ni zaidi ya 417 na kwenye Vituo vya Polisi vyote tumeweka Madawati ya aina hiyo ili kuongeza idadi iwe kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu njia mbadala, kama Serikali tumeendelea kuongeza jitihada za kutoa elimu licha ya hatua kali tunazozichukua. Ndiyo maana tunaendelea kuwasihi hata viongozi wa kiroho kwenye nyumba za ibada kuendelea kutoa elimu hiyo kwa sababu matukio haya maeneo mengi yanaambatana na imani za kishirikina. Wengine wanaamini wakifanya hivi watapata utajiri, wengine wanakuwa na kesi wanaamini wakifanya hivyo watakuwa wamesafishika kwenye kesi hizo na wengine wanaamini watapona magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, jamii kwa ujumla wake katika maeneo tofauti tofauti tumeona tupanue elimu hasa hasa zikiwepo nyumba hizo za ibada kwa sababu maeneo ambapo nyumba za ibada watu wameshika sana mienendo ya Kimungu matukio haya ya kikatili yamekuwa pungufu zaidi. Kule ambapo kuna imani nyingi za kishirikina ndiko ambapo matukio haya ya ajabu ajabu yamekuwa yakiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kazi hiyo kuwapa viongozi wa kiimani tunaendelea kutoa rai kwa wananchi kutoa taarifa ili sisi kwa upande wa Serikali tuweze kuchukua hatua kali kwa wale watakaobainika wamefanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmannuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Walimu ndiyo wanaowalea watoto wetu shuleni na ndiyo wanaotegemewa zaidi kuwa walinzi wa watoto hawa wanapokuwa shuleni. Hata hivyo, baadhi ya Walimu ndiyo wamekuwa na tabia za kuwadhalilisha watoto kwa vitendo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa kuna suala la elimu, mtoto yule anakuwa mwoga kutoa taarifa pale anapodhalilishwa na Mwalimu. Serikali ina mkakati gani wa kuwapa watoto elimu ili wawe na ujasiri wa kuripoti vile vitendo ambavyo wanafanyiwa na baadhi ya Walimu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali imeweka utaratibu shuleni wa kuwawezesha watoto wa kike kuwa na ujasiri wa kuripoti matukio ya udhalilishaji ambayo yanafanyika yaani *life skills* na pia tumeanzisha *club* mbalimbali za kuwawezesha watoto kuwa na ujasiri wa kuweza kuripoti matukio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuomba na kuwasihi watoto wasiwe na uwoga wowote kwa sababu Serikali yao inawalinda. Pale ambapo anafanyiwa vitendo ambavyo ni kinyume na matakwa ya Serikali, watoe taarifa na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote wanaodhalilisha watoto na kuwasababishia wasisome shuleni kwa amani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuwaadhibu wale wote wanaofanya vitendo vya udhalilishaji, lakini watoto hawa wanaofanyiwa udhalilishaji wanapata madhara ikiwemo kuambukizwa magonjwa na kupewa mimba. Je, Serikali ina jitihada gani za kuhakikisha watoto hawa ambao wamepata maradhi au wamepata mimba wanasaidiwa ili kutimiza ndoto zao za maisha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua ambazo nimetoka kuzieleza na ambazo Waheshimiwa Mawaziri wametoka kuzisema za kuchukua hatua kuhusiana na wahusika ambao wanafanya matendo hayo ya udhalilishaji, nami niendelee kutoa rai tu, changamoto ya kuyafikisha mashauri haya Mahakamani mojawapo ni kwamba ndugu na wazazi wa watoto wale wanakubaliana na mtuhumiwa kuyamaliza mashauri yao nje ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa rai kwa jamii kuhakikisha kwamba udhalilishaji wowote wa mwanamke na mtoto masuala haya yasimaliziwe mtaani, badala yake yaweze kufikishwa katika vyombo vya dola. Sisi kama Wizara na Serikali tutaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kwamba matibabu kwa wale ambao watakutwa wameathirika na virusi vya UKIMWI, kwa sababu huduma za tiba ya UKIMWI zinatolewa bure na Serikali na pale itakapothibitika kwamba binti yule ameweza kupata ujauzito basi huduma za afya kwa wajawazito ni bure kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia kuhusu kutokomeza vitendo vya udhalilishaji kwa watoto na kwa kuwa takwimu zinaonesha kwamba kila watoto sita wanaozaliwa watoto wanne sio wa baba mhusika. Je, Serikali inaonaje kuhusu udhalilishaji wa akinababa kwa kubambikiziwa watoto ambao siyo wa kwao ki-*genetic*? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke kumbukumbu sahihi ili hii dhana ili isizidi kuenea. Si kweli kwamba watoto sita katika watoto wetu tuliokuwa nao wote si wa baba ama wazazi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke vizuri jambo hili. Takwimu ile ilikuwa inatokana na wale waliopeleka vipimo vyao kwa ajili ya vinasaba kutambua uhalali wa mzazi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikilize, nataka tuelewane vizuri. Ni sawasawa unaenda katika wodi ya *TB* unataka kujua maambukizi ya wagonjwa wa *TB* katika wodi ya *TB.* Wale wote waliopeleka *sample* maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni wale ambao tayari wana wasiwasi kuhusiana na uzazi wa wale watoto na ndiyo maana hicho kiwango kilichopatikana kikawa hicho, lakini siyo kwamba kwa ujumla wetu Tanzania nzima watoto wengi hususan kwa akina baba siyo watoto wao, siyo kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiweke hiyo taarifa wazi ili sasa Wabunge na *especially* wanaume tusianze kukimbia majukumu yetu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza hapa nilidhani wanawake tunataka kuandamana humu ndani. Mheshimiwa Chegeni haya maelezo yake na watu tuna watoto wengi humu ndani... *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Kiswahili cha kawaida kabisa kinasema kitanda hakizai haramu, unaenda kupima kwa nini? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta matangazo kwenu ya wageni waliotufikia siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Mheshimiwa Spika na hawa ni wageni saba, wageni wangu mimi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mbeya. Hawa ni Watendaji na Wataalam wa Shirika la Marekani la Misaada ya Sekta ya Afya liitwalo *Henry Jackson Foundation For Medical Research International.*

Waheshimiwa Wabunge, shirika hili kupitia mradi wa *PEPFAR* limeajiri Watanzania zaidi ya 300 na linatoa misaada ya kununua dawa za *ARV's,* ujenzi wa *CTC,* vifaa tiba na ushauri kwa Nyanda za Juu Kusini pamoja na kufadhili mradi wa kutokomeza malaria kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Wageni wetu hawa wameongozwa na Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo Dkt. Joseph Chintowa. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph George Kakunda ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambao ni ndugu zake wanaotokea Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Venance Methuselah Mwamoto ambaye ni mdogo wake anayeitwa Telly Mwamoto, huyu ametoka Wilayani Kilolo Mkoa wa Iringa. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vile vile tunao pia wageni 59 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutoka Chuo cha Madini Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Clement Madinda ambaye ni Rais wa Serikali ya Wanafunzi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao kwa siku ya leo na nitamkaribisha Mwenyekiti ataendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Mlinga. Tunaanza na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mwongozo wangu unatokana na swali Na.23 ambalo limezua mjadala mrefu hapa Bungeni na inaonesha ni kwa jinsi gani tatizo hili limekuwa kubwa na limekithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Wabunge wenzangu wamezungumzia kuhusu watoto kunyanyasika hasa katika suala zima hilo la udhalilishaji/ubakaji lakini wanasahaulika watoto wenye ulemavu wa akili. Watoto hawa wanabakwa, wanalawitiwa na hata wazazi wanapokwenda kutoa taarifa katika Vituo vya Polisi na hata baadhi ya kesi ambazo nina ushahidi nazo zimefikishwa Mahakamani, zimefutwa kwa sababu sheria inaeleza kwamba ili mtu aweze kutoa taarifa za uhakika uwe na akili timamu, Katiba inatambua hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa tayari wana ulemavu wa akili na kwa sababu hawawezi kujieleza kwa ufasaha wamekuwa ni waathirika namba moja wa matukio haya ya udhalilishaji hasa ubakaji na suala zima la kulawitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa hawana pa kusemea na hata wanaposema kwa sababu tayari wanahesabika kwamba wana ulemavu wa akili inakuwa siyo rahisi ule ushahidi wao kukubaliwa Mahakamani au hata Polisi kwenyewe ushahidi unafutika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kauli kutoka kwa Serikali kwa Mwongozo wako ili basi watoto hawa tuone kwamba tunawasaidiaje kwa sababu ninao ushahidi wa kesi ambazo zimefutwa kwa kukosa ushahidi kwamba watoto hawa wameshindwa kujieleza. Serikali inalizungumziaje hili ili kuhakikisha kwamba watoto hawa na wao wanatendewa haki kama ilivyo watoto wengine wenye akili timamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nimesimama kwa Kanuni ya 68(7). Mwongozo wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati likiulizwa swali Na.23 alipouliza Mheshimiwa Rukia, alihoji ni lini Serikali italeta sheria ya kuwahasi wanaume wanaowabaka watoto wadogo wa kike. Naomba Mwongozo wako, je, ni lini Serikali italeta sheria kwa wanawake wanaowabaka watoto wa kiume, nao watahasiwa? Kama watahasiwa itatumika njia gani ya kuwahasi akinamama wanaobaka watoto wa kiume? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate Mwongozo wa Kiti kwamba siku ya leo kulikuwa kuna maswali yasiyozidi matatu na muda bado unaruhusu kwa sisi Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuuliza maswali kuhusiana na changamoto za Mikoa yetu. Nataka nipate Mwongozo wako, maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu leo hayakuwepo na maswali pia kwenye karatasi hii yako manne, ni kwa nini jambo hili limetokea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hivi navyoongea usiku wa kuamkia leo imetokea ajali mbaya sana na imesababisha vifo vya watu ambao siyo chini ya 12, Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara zetu kuna alama za barabarani ambazo sehemu ukikuta *speed* 50 ukazidisha *traffic* wanakukamata na wanakutoza *fine*. Hii iko hivyo sehemu zote zenye alama za barabarani na wamekuwa wakiifanya kazi hii kweli na juzi niliongea kuwa wamegeuka ma-*agent* wa *TRA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali ya jana imesababishwa na ubovu wa barabara, kwenye barabara kuna shimo na siyo hapo tu, ukitoka Morogoro kuja Dodoma kuna mashimo mengi kweli kweli na yamekuwa yakisababisha ajali. Nataka ufafanuzi wa kisheria kutoka Serikalini, sheria zimekaaje endapo ajali inasababishwa na ubovu wa barabara na hakuna alama zozote? Niliomba *traffic* waache kutoza faini magari tu waangalie na barabara zenyewe, sasa sheria imekaaje? Nataka ufafanuzi, nao *TANROADS* watozwe faini au la? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea miongozo minne. Mwongozo wa kwanza Mheshimiwa Amina kuhusu swali Na.23 amezungumzia kwa ufupi kuhusiana na watoto wenye ulemavu hasa wa akili na suala zima la ubakwaji na namna ambavyo wanashindwa kupata utetezi. Pia na Mheshimiwa Mussa amezungumzia swali hilo hilo la Na.23. Suala hili litarudi Serikalini kwa sababu ni pana na sote linatugusa. Kwa hiyo, watatuletea majibu baadaye kuhusiana na nini watakifanya na baadaye tutatoa mwongozo kwa haya yote mawili.

Kwenye suala la Mheshimiwa Rhoda Kunchela kuhusu maswali ya Waziri Mkuu kwa leo, tulishaambiwa mwanzo na Naibu Spika kwamba leo tulikuwa na hoja yake

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, hakutakuwa na maswali yake na maswali hayo manne yaliyo kwenye *Order Paper* ndiyo maswali ambayo yameletwa na Wabunge. Huo ndiyo mwongozo wangu.

Mheshimiwa Mlinga ajali hiyo ambayo unasema imesababishwa na ubovu wa barabara na hilo nalo siwezi kulisema kwa sababu hatuna uhakika na hiyo ajali yenyewe mpaka tutakapoletewa taarifa kamili na Serikali tukaweza kutoa mwongozo wake.

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo majibu ya miongozi iliyoombwa, Katibu tuendelee. *(Makofi)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mjadala unaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein. Tutaendelea na Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura na baadaye tutakwenda kwa Mheshimiwa Jackson Rweikiza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah Rahman Rahim*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo siku ya leo kuchangia hotuba iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nami nitajikita zaidi katika ukurasa wa 10 - 12 katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze na historia fupi ili wale ambao wana mtazamo finyu waweze kuelewa historia ilisemaje au historia inasemaje. Nasema Taifa la Zanzibar lilianza miaka mingi sana, ni Taifa lenye historia ndefu

na ilianza kabla hata ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo miaka 2,000 iliyopita. Ukitaka kuipima historia ya Zanzibar basi itakuchukua muda mrefu, lakini mimi nitaanza hapa kwenye karne ya 18 na 19 ambapo walio wengi wanaweza kukumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watakumbuka kwamba Zanzibar ilikuwa ni *center* ya biashara kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati, Zanzibar ilikuwa ni Taifa lenye Mabalozi wake miaka hiyo lakini Zanzibar ilikuwa na mfumo madhubuti wa kiuchumi na kiulinzi. Kwa hiyo, Zanzibar lilikuwa Taifa kubwa na litaendelea kuwa Taifa, historia inasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwarejeshe kidogo waelewe ninaposema kwamba Zanzibar lilikuwa Taifa na lilikuwa na nguvu za kijeshi na kiuchumi. Zanzibar katika karne ya 18 ilikuwa tayari ina jeshi lake kubwa na ina manuwari za kivita. Zanzibar ilikuwa na Jeshi la Ardhini lililokuwa linaongozwa na Jenerali Sir Lloyd William Matthews ambaye alifariki na kuzikwa Zanzibar na kaburi lake lipo pale pale Zanzibar na jeshi hilo lilikuwa linaitwa *Blue Jacket.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa na Jeshi la Baharini ambalo lilikuwa na manuwari kumi za kivita. Kulikuwa na manuwari inaitwa *Liverpool* ambayo ilitengenezwa India mwaka 1826 ikiwa ina uwezo wa kuchukua mabaharia 150 na mizinga 74 lakini kulikuwa na *Prince Regency, Victoria, Shaalam, Coral lean, Rahman, Pied Montez, Mustapha, Atenamise* na *Crew.* Zote hizi zilikuwa ni manuwari za kijeshi, katika karne ya 18, Zanzibar tayari ni nchi na ina vifaa kama hivyo vya kijeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Zanzibar ilikuwa na majemedari wa kivita ambao walipigana vita. Waliosoma historia wanaweza kukumbuka kwamba Zanzibar kulitokea vita baina ya kabila la Mazrui na mpaka kufikia Kisiwa cha Pemba kikatekwa, lakini majemedari hawa ni miongoni mwa majemedari waliopigana vita hiyo na kukikomboa Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na jemedari wa mwanzo Jenerali Mohamed Juma, Jemedari Khalef bin Nassor, Jenerali Mohamed bin Nassor, Jenerali Hamad bin Ahmed, Jenerali Abdallah Sleyum, Jenerali Khalid bin Said, Jenerali Nassor Sleyum, Jenerali Hemed Sleyum na Jenerali Jen Tagai. Wote hawa walikuwa ni majemedari wa kivita ambao walikuwa katika majeshi ya Taifa la Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuchumi Zanzibar ilikuwa ni Taifa ambalo linajiendesha kibiashara. Mpaka karne ya 18 na 19 Zanzibar ilikuwa inaweza kufanya biashara zake na Bara Hindi, Uarabuni, Uchina, Japan na walikuwa na mikataba ya kibiashara katika nchi hizo. Kwa upande wa Afrika Mashariki na Kati Zanzibar ndiyo ilikuwa kitovu cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naileta historia hii ili tuelewe na kwamba Zanzibar wakati huo ilikuwa tayari na sarafu yake ikitumia sham, rupia, noti zake zenyewe shaba, pesa ya Mnyasa, *blue butter,* shanga, mtama pamoja na *cowrie.* Kwa hiyo, Zanzibar ilikuwa ni eneo kubwa la kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize wakati huo Tanganyika ilikuwa wapi? Hata hilo jina Tanganyika lilikuwa halipo. Tanganyika imezaliwa tarehe 4 Mei, 1885 na baada ya Mjerumani kuchukua eneo la maili 600 la eneo la Mrima. Kwa hiyo, hapo ndiyo jina Tanganyika likapatikana wakati huo Tanganyika jina halipo hawana hata ngarawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kuyaeleza haya ili kuiweka historia sahihi. Nakuja sasa kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye ukurasa wa 11 hapa alipozungumza kwamba katika kutatua kero za Muungano vikao vimefanyika baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuweza kutatua changamoto katika masuala hayo hususani masuala ya fedha, biashara, ajira katika taasisi za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile akaendelea kwamba, wamekutana na kuzungumza katika sekta zinazohusu fedha, biashara, viwanda, uwekezaji, ujenzi, uchukuzi, maliasili na utalii. Kama haya yamezungumzwa na kero za muungano zimeanza karne na karne ni lipi ambalo limepatiwa ufumbuzi katika haya? Hakuna hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni juzi tu, Mawaziri na kamatio zao za viwanda wa Zanzibar na wa Tanganyika hapa, wamekutana wameshindwa kutatua tatizo la sukari. Kuna tani 460,000 Zanzibar za sukari zinataka kuuzwa, Serikali ya Muungano imekataa, lakini wakati inakataa kununua sukari ya Zanzibar Serikali hii inaenda kuagiza sukari Brazil. Ndugu zetu wa damu, ndugu zetu ambao tumeungana hawawezi kununua sukari kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wanaenda kununua sukari Brazil. Kisingizio eti ukinunua sukari ya Zanzibar wataagiza sukari kutoka nje na badala yake watachanganya wauze Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hata kama ni hivyo, iwe kweli ni hivyo, kwani kuna ubaya gani kununua hiyo wakati unaangalia wewe ile *marker price* tu. Kama bei ya Brazil na bei ya Zanzibar ni sawa kuna ubaya gani? Lengo la hili si kweli kama hapa hotuba ilivyoeleza kwamba, wana nia ya kutatua, lakini lengo lake ni kuikandamiza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isiwe na mapato yake ya ndani, hili ndio lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, mwangalie *market price,* kwanini usinunue sukari? Mbona sukari inayotengenezwa Mtibwa mnanunua wakati kile ni kiwanda vilevile ambacho kinatokana na kiwanda cha sukari cha Zanzibar? Sasa hii kwa nini mnunue? Mtoto halali, lakini mama haramu, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lengo hapa la hii hakuna lengo la kutatua kero ya Muungano na lengo lake ni kuhakikisha kwamba, Zanzibar haipati mapato. Matokeo yake ni nini...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Kaa chini, acha kelele hapa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf tafadhali subiri. Mheshimiwa Kessy?

**TAARIFA**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa mzungumzaji, analalamika sukari ya Zanzibar; hiyo sukari haiwatoshi hata Wazanzibari wenyewe, wanataka kufanya huku bara ndio dampo la kupitisha mali ya magendo kutoka Zanzibar. Nampa Taarifa tu mzungumzaji ajue hilo, sukari kule Zanzibar haiwatoshi Wazanzibari, leo wanaagiza sukari ya magendo ili kwamba, sisi tuwe ndio dampo la wafanyabiashara wa Zanzibar, haikubaliki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mie Mwongozo wake wala siusikilizi kwa sababu, hata masuala ya biashara hajui, wala hiyo Zanzibar haijui, wala hajui chochote huyu, huyu *aljununi fununu* humu ndani humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala sukari ya Zanzibar haiwatoshi Wazanzibari wenyewe anajuaje yeye? Zanzibar inatumia sukari tani ngapi? Usinipotezee muda, huna unalojua, unataka sifa wala Uwaziri hupewi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee wasinipotezee muda wangu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, Kiwanda cha Mahonda kina uwezo wa kuzalisha tani 8,000 tu kwa mwaka wakati mahitaji ya Zanzibar peke yake ni tani 17,000 mpaka tani 20,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa ajielekeze kwenye hoja kuliko kupotosha Taifa kwamba, Tanzania Bara haitaki kununua sukari kutoka Zanzibar, sukari Zanzibar bado kuna upungufu wa zaidi ya tani 9,000. Kwa hiyo, naomba kuweka rekodi sawasawa na mzungumzaji abadilishe hoja yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri nakuheshimu sana, unajua fedha hujui biashara. Kwa nini mnaagizia mitumba wakati mnazalisha pamba hapa Tanzania na inawatosha kuzalisha nyie? Njoo kwenye biashara tukufundishe biashara, wewe ni mtu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hata kama sisi tunaagiza sukari kutoka nje, tunaiuzia Tanganyika muangalie *market price.* Ikiwa *market price* ni sawa kwa nini msinunue Zanzibar mkanunue sukari Brazil wakati Zanzibar ipo imejaa kwenye ma-*godown? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndio hoja yangu. Kwa hiyo, lengo ni kuikandamiza Zanzibar isipate mapato yake kiuchumi. Kwa hiyo, ajenda hii iliyozungumzwa hapa

kwamba, mnakaa SMZ na SMT kuzungumzia kero za Muungano, halina ukweli wowote na lengo lake hii ni kuikandamiza Zanzibar isipate maendeleo kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini? Serikali ya Zanzibar sasa hivi ime-*stuck* na wanailazimisha *ZRB* kukusanya mapato ya milioni 200 kila mwezi kutoka kwenye vyombo vya moto tu, hivi Zanzibar kuna magari mangapi, vespa ngapi, pikipiki ngapi ambazo watatozwa faini wapate milioni 200? Matokeo yake kuwa na chombo cha moto Zanzibar sasa hivi ni laana. Ndugu zetu wa damu hawa kuinunua sukari ya Zanzibar hawataki ma-*godown* yamejaa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, amezungumzia hapa, katika ukurasa wa 17 na ukurasa wa 18 kwamba, Msajili wa Vyama anasimamia vizuri suala la demokrasia ya vyama vingi, ili iimarike. Siamini katika hili na ninaamini kama Msajili wa Vyama ndiye anayeuwa Vyama vya Siasa hapa Tanzania na hususan Vyama vya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Msajili wa Vyama anaiandikia CHADEMA kwamba, wajieleze kwa nini asikifute kwa sababu wameandamana. Kwani kuandamana haramu kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yeye badala ya kusimamia vyama vikaenda mbele yeye ndio anavikandamiza vyama, CHADEMA amewafanya hivyo, *CUF* amepandikiza mgogoro yeye mwenyewe, *CUF* haina mgogoro, yeye ndiye anayesababisha mgogoro huu. Yeye msajili alivyo mnafiki kamwandikia Katibu Mkuu kwamba, hatatoa ruzuku kwa sababu, ana mgogoro. Akamwandikia Ibrahim Lipumba kwamba, hatatoa ruzuku kwa sababu chama kina mgogoro.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yusuf naomba ukae. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**MWONGOZO**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo. Naheshimu sana michango ya Mheshimiwa Mbunge, lakini naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68 na Kanuni ndogo ambayo inaturuhusu kuomba Muongozo na Kanuni ya 64 ambayo, inatuongoza tunapochangia ndani ya Bunge kutumia lugha zenye staha ambazo sio lugha za kuudhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatosha tu na inafaa kabisa kwa mchangiaji ajenge hoja, lakini kutumia lugha hizo ambazo kwa kweli, si lugha ambazo ni za Kibunge, ningeomba sana niombe Muongozo wako kama lugha hizi za kumwambia mtu ni mnafiki, ni nini, ni lugha za Kibunge na zinaruhusiwa ndani ya Bunge? Kama sio lugha za Kibunge kwa kweli, ningeomba sana zisitumike na lugha hiyo ifutwe na mchangiaji aendelee tu kutumia lugha za Kibunge na ajenge hoja inavyotakiwa. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, niachie mwenyewe nitamjibu huyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf, kwa vile ni Muongozo huo, nitaomba ujielekeze kwenye hoja na uache lugha ambayo si rasmi ndani ya Bunge ya kuita watu kwa majina ambayo ni ya kuudhi na ujielekeze kwenye hoja na ufute kauli zako zote ambazo zina maudhi. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, neno mnafiki, namuomba Mheshimiwa Waziri kama hajui arudi katika Biblia, arudi katika *Qur-an*, arudi katika tafsiri, neno unafiki maana yake ni nini. Arudi huko ataona, kama hajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu vizuri maana ya unafiki, nitafsirie; mmoja kati ya alama za mnafiki ni anapoahidi asitekeleze.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf naomba uendelee na hoja tafadhali, rudi kwenye hoja rafiki yangu Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye hoja kwamba, Msajili huyu kamwandikia barua lipumba kwamba, hatatoa ruzuku kwa sababu chama kina mgogoro. Akamwandikia barua hiyohiyo Seif Sharrif Hamad kwamba, hatatoa ruzuku kwa sababu, chama kina mgogoro. Kwa nini leo msajili huyu anarudi anampa Ibrahim Lipumba zaidi ya bilioni 1.3 pesa za ruzuku wakati alishaandika kwa maandishi kama hatoi? Kama sio unafiki ni nini? Kaandika yeye mwenyewe, sasa hiyo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hajengi siasa za vyama na badala yake anaua vyama na lazima tumwambie...

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kifungu cha 68(8), kumpa Taarifa anayechangia. Msajili wa Vyama vya Siasa ana haki Katiba ya kuangalia namna ya kutoa ruzuku ifanye kazi ya chama. Msajili wa Vyama vya Siasa anapokea barua kutoka kwenye chama *system,* kwa maana ya chama taasisi sio kwa mtu binafsi ambaye sio kiongozi wa chama. Msajili wa Vyama vya Siasa aliandikiwa barua na uongozi wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kuomba atoe ruzuku ili chama kiweze kushiriki kwenye chaguzi ambazo zilitangazwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitendo cha Mheshimiwa Msajili wa Siasa kutoa ruzuku kwa Chama cha Wananchi *(CUF)* ni haki kwa sababu, kazi ya ruzuku ni kujenga chama ndani ya *CUF* na ndani ya Tanzania. Kwa hiyo, anayeendelea kuchangia akasome vizuri Sheria ya Vyama

vya Siasa, akasome vizuri majukumu ya Msajili wa Vyama vya Siasa, akasome vizuri Katiba ya Chama aweze kuchangia sawasawa na weledi. Ahsante. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ahsantee!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa; nataka kumpa Taarifa huyu, nataka kumpa Taarifa huyu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf naomba aendelee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Ninyi sio Wenyeviti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib naomba uketi kwanza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI**: Kaa, Khatibu Kaa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib naomba usubiri kwanza apokee taarifa ya kwanza, Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi unipe.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo siipokei kwa sababu, huyu *yakuuluna maala yafaaluuna.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf naomba uendelee kuchangia hoja.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa haipokelewi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf naomba umalizie hoja yako.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokisema mimi ni kuandika barua yeye mwenyewe halafu akarudi akatoa pesa. Kama aliandikiwa barua kwa nini, asirudishe barua zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye mwenyewe ndiye alisema; mimi nazungumzia hoja yake mwenyewe, maandishi yake mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf muda wako umekwisha. Nashukuru asante.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu haujaisha unanibana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Sabrina Sungura. Mheshimiwa Sabrina Sungura. *(Makofi)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa afya na uhai na leo hii kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijielekeze kwenye mchango wangu kwenye mambo mbalimbali ambayo yameainishwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu na ningeomba nianze na suala la kwanza kuanzia kwenye suala la Mahakama, lakini pia, mambo ya ndani, magereza na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa masikitiko yangu kwa kile ambacho nilikiona kimetokea Ijumaa iliyopita tukiwa Mahakamani Kisutu. Tulishuhudia kwamba, ile

tunayoita miongoni mwa *cardinal principle* za *Criminal Law* kwamba, *alignment to the Court* kwa *accused* ama *suspect* inavunjwa waziwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia kabisa kwamba, mtuhumiwa ana haki ya kufikishwa Mahakamani kwa wakati, lakini kulikuwa kuna sababu mbalimbali ambazo tunaambiwa kwamba, magari yameharibika hivyo, wale watuhumiwa hawawezi kuletwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunakuwa tunavunja ile misingi ambayo tumejiwekea kwenye sheria. Kwamba tunategemea Jeshi la Magereza liweze kujipanga vizuri na liwe linafanya kazi kwa wakati na tusiwe na visingizio vidogovidogo, itakuwa inatuharibia sura ya Wizara, lakini na pia sura ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwenda moja kwa moja sasa kwenye Mahakama ya Mafisadi, ile ambayo inaitwa *The Corruption Economic and Organised Crime, High Court Division.* Tulisema mafisadi papa na wale ambao ni mafisadi *size* ya kati kwa makosa yatakayoanzia bilioni moja wanatakiwa wapelekwe pale, lakini kumekuwa kuna upungufu wa watu wanaopelekwa kwenye Mahakama ile kwa sababu, kuna watu ambao hawafikii kile kigezo cha bilioni moja kwa hiyo, wanakuwa hawana sifa ya kwenda Mahakamani pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kama Mahakama ambayo tumeianzisha, tumeweka watendaji, tumeweka Majaji, tumeweka Maafisa wa Mahakama na maofisa wengine, inakuwa Mahakama ile tunaona kama haijiendeshi kwa makusudio ambayo yaliwekwa kwa sababu, watuhumiwa wanakuwa ni wachache sana. Hivyo, tungependa kuiomba Serikali iweze kupunguza kile kiwango kilichowekwa, ili watu wengi waweze kwenda kuchajiwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna changamoto. Changamoto ya kupata *report* za Mkemia Mkuu wa Serikali,

zimekuwa zinacheleweshwa sana, kitu ambacho kinasababisha watuhumiwa wengi kuweza kucheleweshwa kesi zao. Hata ukiangalia katika hotuba ya Kitabu chetu cha Waziri Mkuu, ukurasa wa 62, ukiangalia idadi ya kesi ambazo zilipelekwa Mahakamani na idadi ya kesi ambazo ziliamuliwa kwa kweli, zinaonekana ni chache sana, hivyo, kunakuwa kuna shida hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili ambalo ningependa kuchangia ni suala la kufungiwa kwa mabenki yetu. Nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma, tulishuhudia benki mbalimbali zikiwa zimefungiwa kwa kukosa mitaji. Hata hivyo, tunaangalia *initial capital* ya benki hizi ambazo wakati wanaanza ku-*operate* walianzisha kwa milioni 250, lakini wakapewa *limit* ndani ya miaka mitano waweze kufikia bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilichotokea hapa ni kwamba, waendeshaji wa taasisi hizi za kibenki wameshindwa kufikia mitaji ile na kusababisha benki hizi kufungwa. Kwa hiyo, kwa akili ya harakaharaka hapa sisi tuko watu 360 humu ndani, hivi ni nani ambaye anaweza akapewa milioni 250 halafu akaambiwa azalishe mpaka bilioni mbili ndani ya miaka mitano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza tukaona hapa kwamba, kuna changamoto kubwa sana na waathirika wa suala hili wanakuwa ni Watanzania ambao ni wafanyabiashara wa kawaida kabisa ambao wanaambiwa walipwe 1,500,000/= halafu wasubiri *process* ya *insolvence* mpaka itakapokamilika. Ukiangalia hata katika sheria *process* hii ndefu na inachukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, tungejaribu kuyafikiria mabenki haya, ili pale tunapowawekea *conditions* za kujiendesha basi wawe na viwango ambavyo watafanya kazi na vitakuwa ni viwango stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwenda kugusia suala la maji. Pale Kigoma Ujiji Manispaa kuna mradi mkubwa sana wa maji, lakini pia tuna changamoto ya

umeme. Tuna pampu takribani 13, lakini mpaka sasa pampu zinazo-*operate* ni nne, pampu tisa zimekaa pembeni, changamoto kubwa ni umeme. Wakisema wa-*operate* pampu zote maana yake ni kwamba, shirika lile la maji litakuwa linajiendesha kihasara kwa sababu, utahitajika umeme ambao utakuwa ni *2.5 megawatt* kwa mwezi, kiasi ambacho ni kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *the only solution* ambayo tunaitegemea ni *whether* tuunganishwe na gridi ya taifa, ili ule mradi uweze ku-*run* ama Serikali iweze kutenga pesa kwa ajili ya kununua *solar system,* ili tuweze kupata maji safi na salama na watu waweze kupata maji kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, basi tungeomba Serikali ilifanyie mkazo suala hili kwa sababu, wananchi wetu wanaathirika sana, hususan wale wanaofanya ibada za asubuhi, mchana na usiku wanakuwa muda mwingi sana wanahitaji maji. Kwa hiyo, tukikosa maji kwa kweli, inakuwa ni kikwazo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna changamoto ya maji katika Mji wetu wa Uvinza, kuna kituo cha afya kiko pale, mama mjamzito anapoenda kujifungua anatakiwa aende pale na dumu tano za maji, bila hivyo pale hupokelewi wala huzalishwi. Sasa kwenye mazingira kama haya tungeweza kuiomba Serikali, kwenye bajeti ya mwaka huu waweze kututengea kiasi kidogo cha pesa, ili angalau katika eneo lile la kituo cha afya kichimbwe kisima ambacho kitaondoa kero ya akinamama kuweza kwenda na madumu ya maji, ili waweze kupata huduma za kuzalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, ningependa kujikita kwenye dawa za kulevya. Kwa kiasi fulani ningependa kuipongeza Serikali kwamba, suala hili kwa kiasi fulani linapungua, lakini bado tuna changamoto, vijana wakati unga unazuiliwa vijana wengi wame-*diverge,* wanatoka kwenye unga wanaingia kwenye ugoro kwa maana ya tumbaku, lakini pia na mirungi. Kwa hiyo, Serikali sasa na yenyewe ijaribu kuangalia kwamba, huu ugoro ambao vijana

wengi wanatumia una madhara gani na kuweza kutoa elimu kwa umma ili kuweza kuzuwia hujuma kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, ningependa kuchangia kuhusiana na masuala mazima ya ardhi. Katika mradi unaoendelea wa upanuzi wa *Airport* ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ama ya Mkoa wa Kigoma kwa ujumla, kumekuwa kuna wakazi ambao wanakaa maeneo yale karibu na *airport* ambao kuna ambao walipata upungufu wa fidia, lakini pia, kuna wale ambao hawakulipwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikuja ikaahidi kwamba, itafanya malipo ya mwisho kwa wale ambao walipata fidia pungufu na wale ambao hawakulipwa kabisa wangekuwa *included.* Hata hivyo, mara baada ya malipo kubandikwa ilionekana waliopata fidia zile ni wale ambao walisahaulika na wale ambao walipata pungufu hawajaweza kupatiwa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwenye Sheria zetu za Ardhi, yaani Sheria ya *Land Acquisition Act,* inataka pale Serikali ambapo inachukua ardhi ya wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali kwa manufaa ya umma, basi fidia stahiki na ya haki iweze kutolewa kwa wakati, ili wananchi wale waweze kujipanga na maisha mengine yaendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali wakati tunaenda kwenye Bunge hili la bajeti, tunaenda kupitisha bajeti mbalimbali za Wizara; ningeomba waweze kuwaangalia wale wananchi wote ambao walipata fidia pungufu kutokana na ujenzi wa *airport* unaoendelea waweze kulipwa fedha zile na shughuli mbalimbali ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la ajira kwa vijana, kumekuwa kuna shida kubwa sana kwawenzetu wa bodaboda, lakini pia na Askari Polisi. Wiki tatu zilizopita nilishuhudia tukio ambalo ni la kusikitisha sana Dar-es-Salaam, maeneo ya Buguruni. Vijana wa bodaboda wakati wanaendesha bodaboda kwa jinsi ambavyo *traffic* wetu wamekuwa wakilenga kuwakamata na pale ambapo

wanashindwa kufanikiwa kufikia vijana wale basi inafikia hata hatua *traffic* wanashika usukani ule wa mbele na kutaka kama kuugeuza hivi ili waweze kusimama wale vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni yule kijana alirushwa kutoka kwenye bodaboda kwenda mpaka barabarani na gari nyingine ikapita ikapitia kichwa moja kwa moja akapasuka na akafariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanasikitisha sana na vijana wengi nchi nzima wanalalamika, lazima tuwe na njia za staha ambazo zitatufanya tuweze kuwakamata hawa vijana hata pale wanapokosea lakini sio njia ambazo zinapelekea mpaka kwenye mauaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto na tungeomba wenzetu wa Mambo ya Ndani waweze kuona ni kwa jinsi gani wanaweza wakaongea na askari wetu polisi na kuwapa mafunzo kwamba lazima tufanye kazi kwenye njia ambayo itakuwa ni ya kibinadamu, lakini na njia ya staha ambayo haiwezi kupelekea vifo wala majeruhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye viwanda, nimeangalia mpango wa Serikali, nimeona kuna viwanda ambavyo vimeanzishwa na mashirika ya umma na taasisi nyingine takriban viwanda 110, lakini katika viwanda vyote hivyo vilivyoanzishwa kwenye mkoa wangu wa Kigoma sijaona kiwanda hata kimoja. Kwa hiyo ningependa kuishauri tena Serikali zipo sababu mbalimbali zinazopelekea mikoa ya pembezoni isiweze kupata viwanda uki-*compare* na Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani na Tanga. Sisi kwa sababu ya umbali tunapata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sabreena. Tunaendelea na Mheshimiwa Jasson Rweikiza baadaye Mheshimiwa Hawa Ghasia na Dkt. Chegeni wajiandae.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi kuchangia asubuhi ya leo. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya jana ambayo imesheheni mambo makubwa yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Yeye mwenyewe Waziri Mkuu anafanya kazi nzuri ya kusimamia Serikali kuzunguka nchi nzima na kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi nzuri sana ya Serikali yake. Serikali inafanya kazi nzuri sana, kila mtu humu ni shahidi kazi inayofanyika kubwa sana. Kujenga reli ya kisasa ya kimataifa ya umeme, ndege zimenunuliwa zinakuja, barabara zinajengwa, madini hata kesho wanafungua ukuta mkubwa pale Mererani kuzuia wizi wa madini, sekta ya umeme, sekta mbalimbali zinashughulikiwa na zinapiga hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivyo bado kuna nafasi ya kufanya vizuri zaidi na nimesimama hapa kuchangia maeneo mawili, maji na kilimo. Katika maji vijijini kila Mbunge anaposimama hapa hasa Wabunge wa vijijini wanazungumzia maji vijijini, bado kuna tatizo kwenye maji vijijini. Niombe sana lile wazo tulilokwishalisema humu ndani, la kuanzisha Wakala wa Maji vijijini lianzishwe mara moja. Tuanzishe wakala wa maji vijijini. Maji vijijini bado ni changamoto kubwa, wananchi vijijini wana changamoto kubwa sana ya kupata maji salama na safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kule kuna maeneo mengi ambayo ukiona maji wanayotumia wananchi utashangaa na kuogopa. Wanatembea kilometa tatu, kilomita nne kupata maji hayo, hayo maji yenyewe yanafanana na chai ya maziwa, ndio wanayotumia, ndio wanayokunywa, ndio wanayopikia. Sasa tukianzisha Wakala

wa Maji tutapambana na hali hii tutaweza kupata maji mazuri kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposimama juzi hapa kuzungumzia maji lilikuwa swali nikajibiwa kwamba tayari kuna pesa kwenye mfuko wa maji zaidi ya shilingi bilioni 160. Sasa kama kuna fedha lakini hazitumiki na yenyewe haina tija. Wakala aanze, hiyo fedha bilioni 160 ianze kutumika katika vijiji vyetu. Wakala aanze, atafute fedha, ajenge miradi ya maji vijiji. Kila Halmashauri ilikuwa na miradi 10 ya maji, mingi ya hii haijakamilika, asilimia kubwa haijakamilika hakuna fedha, Wakala wa Maji uanzishwe kusudi tupate ufumbuzi wa tatizo la maji vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa mfano kwamba *REA* imekuwa na mafanikio makubwa na *REA* ni Wakala wa Umeme Vijijini. Tuwe na Wakala wa Maji Vijijini tupate kufumbua tatizo la maji. Kule kwangu kwa mfano kata ya Ruhunga maeneo ya Rugaze kule Vijiji vya Rugaze, Kibirizi, Rubweya, Kyamolaile kuna sehemu nyingine nyingi, maji ni changamoto kubwa sana na ufumbuzi ni huo tu tupate Wakala wa Maji atafute fedha, kwenye bajeti kwenye vyanzo vingine, misaada na mikopo kutoka nje, kusudi tatizo la maji liweze kupata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ninalotaka kuzungumzia ni kilimo, ukisoma Ilani ya CCM ya mwaka 2015, kuna makambi ya kilimo. Ukienda Dar es Salaam au miji mingine lakini Dar es Salaam hasa kuna vijana wengi sana maeneo ya mbalimbali Buguruni pale, Ubungo ukienda Mwenge, ukienda Tandale, Mbagala, Temeke, kila maeneo kuna vijana wengi sana ambao hawana kazi wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wale wanauza pipi, wanauza kandambili, wanauza vitambaa vya mikononi na vijana wenye nguvu vijana wenye miaka 25, miaka 30, miaka 18 wanauza pipi, hawana kazi ya kufanya. Ukiwaambia waende kulima mashambani hawatakwenda kwa sababu jembe la mkono ni tatizo, wanaogopa jembe la mkono na wana haki ya kuliogopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema ndio maana ikaingia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi wa mwaka 2015 kwamba tuanzishe kambi za kilimo za vijana. Maeneo mengi Tanzania yana rutuba, maeneo mengi ya Morogoro kule Kilosa, Mvomero, ukienda Rukwa, ukienda Kigoma hata Dodoma hapa shida ni maji tu. Maeneo yana rutuba sana na maeneo makubwa ambayo hayajalimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema vijana wapelekwe kule ukisema kila kambi vijana 100, ukawapa trekta moja au mbili ya mkopo au *power tiller* kadhaa na msimamizi wa kuwasimamia bwana shamba ambaye amesomea hayo mambo ya kilimo kidogo, wakaanza kulima alizeti, wakaanza kulima maharage, mahindi, pamba na mazao mengine ya muda mfupi na ya muda mrefu, hawa vijana baada ya miezi sita watakuwa matajiri. Baada ya miezi sita kwa trekta moja au mbili nchi hii itakuwa na chakula kingi sana shida ya chakula itakwisha, Tanzania itakuwa tajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Bungeni humu miaka mitatu iliyopita nikaona Naibu Waziri mmoja anaenda kwa Waziri wa Kilimo wakati huo, anamwambia amepata maombi ya nchi nafikiri ilikuwa Ghana au Nigeria, wanaomba kununua chakula, akamjibu chakula hakipo kwa sababu kimeshauzwa Kenya, ile *reserve* ya chakula imekwisha. Sasa tungelima chakula kwa njia hii ya makambi ya vijana ambao ni wengi sana ardhi ipo tungepata mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi ambazo hazilimi nchi za jangwa kama huku kaskazini au Uarabuni hawalimi wale lakini wanakula na wana fedha nyingi sana. Tulime kwa wingi sana kwa vijana hawa kwa kutumia trekta na *power tiller* na vifaa vingine, tupate mazao mengi sana, tupate ufumbuzi kwanza kwa ajira kwa vijana hawa na ufumbuzi wa kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifanye makosa ambayo tuliyofanya huko nyuma miaka ya 1974 tulipoanzisha vijiji vya ujamaa tufanye kwa mpango mkakati mzuri. Moja, tunapoanzisha mkakati huu wa Makambi ya Kilimo kwenye

Wizara husika kama ni ya Kilimo kama ni ya Masoko au kwingineko Serikalini, kuwe na vitengo maalum vya kutafuta masoko ya mazao haya nje. Huko *Dafur Sudan* huko, nchi za jangwani huko ambako hawalimi, nchi za Uarabuni huko, kuwe na mkakati maalum wa kutafuta masoko ya kuuza hayo mahindi, maharage, alizeti, korosho na mengine, kuwa *aggressive* kuuza mazao haya kwa bei nzuri na kwa wakati ili vijana hawa wapate fedha wanayohitaji ambayo wameifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo mwanzo, kilimo hiki kiratibiwe vizuri kuwe na Bwana shamba au Bibi shamba na *researchers officers* ambao watasaidia vijana hawa katika kulima kisasa, kutumia pembejeo, mbolea na madawa na kadhalika. Tusitegemee mvua, tusitegemee mvua, nchi hii maeneo mengi ina mvua mara mbili kwa mwaka. Hata pale ambako penye mvua moja kama Dodoma kuna mabwawa ambayo ukizuia ukapiga tuta pale mbele unazuia maji mengi sana huku nyuma, unamwagilia mwaka mzima au angalau miezi nane kwa mwaka wapate tija ya kilimo ambacho nakizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itaondoa kilimo ambacho tumekizoea cha mkulima mmoja mmoja ambacho ni vigumu kumhudumia mkulima mmoja mmoja kumpelekea pembejeo, mbolea, madawa ni vigumu sana. Wakiwa kikundi cha 100 au 200 ni rahisi kuwahudumia na huduma ikawa nzuri ya kupeleka pembejeo na kuondoa mazao ukapeleka kwenye soko. Nchi zote duniani zilizoendelea Marekani, Ulaya wameendelea kwa kilimo. Tu-*modernize* kilimo chetu kwa vijana hawa wakapata ajira na nchi itapata neema kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia viwanda, uchumi wa viwanda, viwanda vingi vinategemea kilimo, kama mahindi, pamba na kahawa ambavyo baadaye unaweza kuvi-*process.* Kwa hiyo, baadhi ya viwanda tena vingi vitatumia mazao haya haya kuongezea uchumi wa viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rweikiza. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia, baadaye Mheshimiwa Dkt. Chegeni na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka ajiandae.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo najielekeza katika masuala matatu, Suala la kwanza ni suala la Hospitali ya Rufaa kanda ya kusini, ambayo tayari ujenzi wake ulishaanza, mapokezi tayari, *OPD* umeshakamilika, ukuta umejengwa lakini kwa zaidi ya miaka miwili mfululizo pesa zinawekwa kwenye bajeti lakini hazitolewi. Sasa kama makusanyo ni matatizo basi wote tugawiwe sawa, sio wengine wanapewa asilimia 80, wengine asilimia 60, wengine sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni suala la uwanja wa ndege wa Mtwara. Kwa zaidi ya miaka mitatu umekuwa ukisindikiza viwanja vingine. Tumekuwa tukiwekewa pesa tukiambiwa kwamba utawekewa taa na utafanyiwa ukarabati kwa sababu upembuzi yakinifu umekamilika, lakini kila mwaka pesa ile inatengwa na inatoka sifuri. Kwa hiyo, nataka niombe kama hakuna pesa ambayo inatakiwa kupelekwa katika kitu chochote aidha hospitali au uwanja wa ndege wasituwekee kiini macho halafu hatuwekewi kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo ndio ningetaka nichukue muda mrefu ni suala la pembejeo la zao la korosho. Korosho kwetu sisi wananchi wa Mtwara, Lindi na Ruvuma, ni uchumi lakini pia ni siasa. Katika miaka mingi iliyopita katika mkoa wetu wa Mtwara tumekuwa na

utaratibu wa kuwa na Mifuko yetu ya ngazi ya Wilaya na Mikoa kwa ajili ya pembejeo za mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 Mheshimiwa Waziri wa Kilimo akaja akawatangazia wananchi kupitia mkutano wa wadau wa korosho kwamba pembejeo zinatolewa bure na akaelekeza wale ambao waliokuwa wamechangia kupitia katika Mifuko yao werejeshewe zile pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mbunge ambaye aliomba tupewe pembejeo bure na hata kwenye kikao vya wadau baadhi ya wananchi walikuwa wanapinga wakiamini kwamba suala hili halitakuwa endelevu. Cha kusikitisha mpaka sasa hivi hatujui pembejeo za korosho zitapatikana kwa utaratibu upi mpaka dakika hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upuliziaji wa zao la korosho unatakiwa kuanza mwezi wa tano mara nyingi na kila baada ya siku 21 na unatakiwa urudie mara tano mfululizo kila baada ya siku 21 na ukichelewa mara ya kwanza maua yanapotea na uzalishaji unashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametuambia hapa kwamba kwa mara ya kwanza kilimo kimeongezeka kwa asilimia sita ukuaji wa pato linalotokana na kilimo imekuwa kwa asilimia 3.6, kwa mara ya kwanza. Kilichochangia ukuaji huo ni zao la korosho, kutokana na uzalishaji kuongezeka lakini pia kutokana na bei ya korosho kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote tumekuwa tukisema kwamba uchumi wa nchi unakua kwa asilimia saba mfululizo kwa zaidi ya miaka 10, lakini ukuaji ule hauonekani kwa wananchi kwa sababu sekta zinazokuwa si sekta ambazo zinaajiri wananchi wengi na sekta inazoajiri wananchi wengi ni kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu na kwa ufahamu wangu na kwa uchumi wangu ambao niliusomea,

nilitegemea Serikali yangu kwa kuwa zao la korosho mwaka jana lilifanya vizuri, kwa hiyo, mipango ya pembejeo na maandalizi mengine yangefanyika mapema na wakulima wangekuwa na uhakika kwamba kwenye pembejeo za korosho wanazipata kwa utaratibu upi na wanazipata lini. Sasa zao ambalo limezalisha vizuri ndio ambalo mwaka huu tumeamua hatutaki kuwekeza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nioneshe masikitiko yangu. Zao la korosho na mazao mengine tulipitisha sheria hapa tukaanzisha Mifuko ya kuendeleza mazao yakiwemo korosho, kahawa, pamoja na pamba na mazao mengine. Mfuko wa Korosho mpaka sasa hivi tunavyozungumza una zaidi ya bilioni 88 za msimu 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho, ikiwa ni pamoja na ubanguaji, utoaji wa miche bora, suala la pembejeo na suala la utafiti katika kituo chetu cha Naliendele, lakini pesa hizo mpaka sasa hivi hatuelewi. Pesa hizo tulitunga sheria hapa ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2011. Sheria haijafutwa na Bunge hili, tunaanzaje kuzuia pesa hizo wakati sheria hatujabadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa mwaka 2016/2017 zao la korosho, korosho zilizalishwa tani 265,237,845 zenye thamani ya Sh.871,462,989,287. Msimu wa 2017 uzalishaji umeongezeka mpaka tani 313,530,700 zenye thamani ya shilingi trilioni moja, kutoka bilioni 871 mpaka trilioni 1.189. Wananchi wamepata zaidi ya trilioni moja, hiyo trilioni moja imeenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa mkoa wa Mtwara peke yao wamepata bilioni 705,399,000,000. Halmashauri msimu wa mwaka 2017 zimepata bilioni 8.2, msimu 2016/2017 walipata bilioni 11 kwa sababu viwango vya tozo vimepungua. *TRA* yenyewe ilipata msimu wa 2016 zaidi ya bilioni 103 kwenye zao la korosho. Hivi kwa mafanikio haya nilitegemea Serikali yangu itumie kila aina ya juhudi kuhakikisha kwamba zao hili sasa linawezeshwa ipasavyo ili kuhakikisha kwamba uzalishaji unaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nioneshe masikitiko yangu, tangu mwaka 2017 mwishoni mwezi Desemba, tumeenda kumtembelea Waziri wa Fedha Wabunge wote wa Mtwara zaidi ya mara mbili. Tumeenda kwa Katibu Mkuu, mara ya kwanza wakatuambia kwamba pesa zipo msiwe na wasiwasi tatizo ni kwamba hii sheria tangu imetengenezwa haina kanuni. Tumekaa tukapitisha kanuni. Tukaambiwa Bodi hawana mpango kazi wala mpango wa manunuzi, wametengeneza imeenda. Sasa hivi tunaambiwa inatoka milioni kumi na bilioni kumi yenyewe kizungumkuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoka kwenye korosho, anaijua korosho naomba korosho isimfie mikononi mwake. Anafahamu katika utaratibu wa kawaida sasa hivi meli za kuleta pembejeo zinapaswa kuwa zimefika. Hata hivyo, ninachoomba Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha waende Mtwara, waende Lindi, waende Ruvuma...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Wakawaambie wananchi kwamba pembejeo mwaka huu hawatapata kwa sababu walituahidi watazitoa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia. Tunaendelea na Mheshimiwa Dokta Chegeni baadaye Profesa Tibaijuka na Mheshimiwa Ally Seif Ungando wajiandae.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba hii nzuri ya Bajeti. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli ameonesha dira nzuri sana na imeonesha kwamba ni kwa kiwango gani uchapaji wake kazi umekuwa ukiongezeka. Kwa maana hiyo hata Mheshimiwa Rais nadhani anamsoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu hotuba yake hii amelenga maeneo yote husika na jinsi ambavyo uchumi wa nchi hii na mustakabali wa nchi hii katika ustawi wake unavyokwenda. Kwa kweli nimefarijika na napenda tu nichangie hotuba hii kwa kukupongeza la kwanza na ninaiunga mkono moja kwa moja hotuba hii ya kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tano Mheshimiwa Waziri Mkuu imekuwa na changamoto nyingi sana. Kila mmoja anaweza kuiona kwa sura yake na kwa muono wake lakini naomba nikiri kwamba kazi wanayochapa Serikali ya Awamu ya Tano haina mfano. Wamefanya uwekezaji ambao ni *world class record*. Haijawahi kutokea katika kipindi chote cha miaka yote Tanzania toka kuumbwa kwake kuwa na uwekezaji mkubwa kwa kipindi kifupi. Hii ni dalili njema kwamba tunaumia kwa kipindi kifupi tutanufaika kwa kipindi kirefu kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imejilenga katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji mpaka sasa hivi katika *public sector* ni zaidi ya trilioni 48.5 lakini deni la Taifa ni trilioni 46. Nasema kwamba umewekeza mtaji mkubwa kuliko deni la Taifa. Bado tuko vizuri na hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza kwamba sisi bado tunakopesheka. Naomba tukope kwa kuwekeza hata ile miradi ambayo ina tija kwa Watanzania, tusikope kwa miradi ambayo hatuna tija nayo. Naona kwa hili mmejielekeza vizuri sana nakupongeza sana wewe pamoja na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote haya ningependa kuzungumzia suala moja ambalo ni tatizo sasa linaanza kujitokeza. Kuna suala la mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Simiyu wilaya mbalimbali za Mkoa wa Simiyu. Mheshimiwa Rais mwaka jana mwezi wa kwanza alikuja na

akatoa maelekezo kwamba mradi ule uanze mara moja kwa sababu mahitaji ya maji ni ya msingi sana kwa wananchi wa Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mwekezaji kwenye mlima wa Ngasamo, Mheshimiwa Rais akasema kwamba yule mwekezaji kwa vile haendelei na uwekezaji basi leseni yake ifutwe. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mwaka mzima sasa umepita toka Rais atoe maelekezo lakini hakuna kinachoendelea. Tumeongea na Waziri wa Maji anasema kuna mambo ya madini, Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa hapa ni kwamba hakujakuwa na Mwenyekiti wa Tume ya Madini, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu tuone mamlaka inayohusika ateuliwe huyu Mwenyekiti wa Tume ya Madini ili kusudi leseni iweze kufutwa na mradi uweze kutekelezeka. Bila kufanya vile hatutaweza kusonga mbele, kwa sababu pesa hii inatoka kwa wahisani na moja kati ya sharti lao ni kwamba lazima kuwe hakuna *encumbrance* yoyote kwenye uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alibebe hili aongee na Mheshimiwa Rais kama inawezekana huyu Mwenyekiti wa Madini basi ateuliwe mara moja ili kazi ifanyike kwa sababu kazi haziendi kama ambavyo tulikuwa tunatarajia na wananchi wa Mkoa wa Simiyu wanasubiri kwa hamu sana mradi huu ambao ni wa kihistoria. Naomba tuendelee kuiunga mkono miradi kama hii, najua kuna maeneo mengi wana miradi kama hii inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wilaya mpya bado ni changamoto. Wilaya ya Busega ni moja ya wilaya mpya ambazo hazijakomaa. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka juzi alikuja yeye mwenyewe akatembelea Wilaya ya Busega, akaona jinsi tulivyo hatuna jengo. Tunajenga jengo la halmashauri halijakamilika huu ni mwaka wa tatu, hatuna hospitali ya wilaya na miundombinu, hata Mkuu wa Wilaya hana ofisi anatumia Ofisi ya Mbunge kama ofisi yake. Sasa

vitu kama hivi ningeomba tuweke kipaumbele kwa sababu palikuwa na miradi mingi mingi midogo midogo bila kukamilisha ambayo imeshaanza tayari. Ningeomba kupitia bajeti hii wilaya ambazo bado zinahitaji kuimarishwa basi zikamilishwe ili tuweze kusonga mbele tumalize moja twende na lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa suala la wilaya hizi mpya hususani Busega na Itilima kwa Mkoa wa Simiyu na wilaya zingine katika nchi hii ziangaliwe kwa kuwekewa miundombinu ambayo ni muhimu sana stahiki ili ziweze kufanya kazi na kutoa huduma kwa Watanzania kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya bado kuna suala la uwekezaji katika viwanja vya ndege. Kiwanja cha Ndege cha Songwe kimeshajengwa lakini kimebaki kukamilika kidogo tu lakini pale hakuna taa za kuongozea ndege kutua pale. Ni uwekezaji mdogo kama bilioni nne hivi. Tunaomba sana Serikali miradi kama hii iweze kukamilishwa kwa sababu leo hii kwa Tanzania tuna viwanja vinne vikubwa. Kiwanja cha Dar es Salaam Julius Nyerere *International Airport*, kiwanja cha Mwanza, Kiwanja cha Songwe na kiwanja cha Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hata Mwanza, tunalilia kwamba uwanja wa Mwanza uweze kujengwa jengo la kushukia abiria. Mpaka leo ni miaka nenda rudi bado hatujatekeleza. Ningeomba tuangalie *priority* ya kiuchumi, ukiweza kuimarisha Songwe ikaweza kufanya kazi vizuri, ukaimarisha Mwanza ikafanya kazi vizuri, ukaenda na Mtwara ukaimarisha tayari tutakuwa na viwanja ambavyo vitaongeza mapato makubwa kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kama Serikali mjaribu kuangalia vipaumbele ni vipi ambavyo tuweze kuvifanya vitakavyoongeza tija zaidi halafu tu-*service* viwanja vingine vidogo vidogo kadri ya fedha inavyopatikana,

tusisubiri sana fedha ya wahisani ikiwezekana pesa zetu za ndani zitumike kuweza kukamilisha miundombinu ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tunalo na ni tatizo kubwa kidogo na hasa sisi wenyeji wa kanda ya ziwa. Mwananchi wa kanda ya ziwa anategemea uchumi wake kwenye kilimo, uvuvi na ufugaji. Leo hii suala la wavuvi haramu hakuna anayeunga mkono suala la uvuvi haramu lakini bado kitendo kinachofanyika kuhusu kuwanyang'anya vifaa vyao tunaamini wavuvi wao wananunua nyavu kutoka kwenye viwanda na maduka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya maduka ilikuwa ndio chanzo cha kuweza kuyawajibisha zaidi kuliko mnazuia haramu. Maana yake mvuvi yeye anavua apate riziki yake apate kipato chake lakini anatozwa faini ambazo ziko nje ya utaratibu, ananyanyaswa, jamani nadhani kama CCM sisi tunasema kwamba hatutii watu umaskini tumekuwa tunatia watu utajiri. Ningeomba sana sana Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili tuliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazao kwa mfano pamba mwaka huu kuna uzalishaji mkubwa sana wa pamba katika mikoa inayolima pamba. Tunaomba kuwe na utaratibu mzuri ili zao hili sasa mkulima anufaike nalo, bila kuwa na utaratibu mzuri tutazidi kuwakatisha tamaa wananchi ambao siku zote wamekuwa wakijitoa muhanga kulima pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafugaji, migogoro ya wafugaji na hifadhi za Taifa bado ni tatizo kubwa sana. Hata jana hapa kulikuwa na mjadala kuhusu tembo, suala sio dogo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wananchi wanalia kwa sababu wanyama waharibifu kama tembo, viboko wanavamia makazi ya wananchi na kuharibu mazao ya wananchi, lakini wananchi wamekuwa ni waaminifu kulinda rasilimali hizi. Tunaomba na Serikali iweze kuwasaidia angalau kuweza kuona kwamba wanalindwa na wao. Tembo

wanaua watu, tembo wanaharibu mali ya watu lakini bado Serikali haiwajibiki kikamilifu, haiwezi kuwasaidia wananchi kwa uharaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tembo anapotokea kuvamia maeneo ya wananchi, unapoomba msaada wa vikosi vya kuweza kuzuia, inachukua muda mrefu sana. Niombe Wizara husika wajaribu kuongea na watu hawa wahusika wote na tuweze kuwa na mustakabali mzuri wa utumiaji na ulindaji wa rasilimali za Taifa. Wakulima na wananchi wanapenda tulinde rasilimali zetu hizi lakini naomba na Serikali iwajibike kwa kiwango kikubwa sana kuona thamani ya mwanadamu katika suala hili lote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la barabara, wilaya mpya zinapoanzishwa zinakuwa hazina miundombinu ya barabara. Tunaomba ile kilomita tano kwa kila halmashauri mpya itekelezwe na tungeenda angalau kwa kwenda kwa mpangilio kwamba mwaka huu labda halmashauri kama ni kumi, kumi na tano zikamilike, mwaka ujao hizi zikamilike, lakini naona unakuta muda mrefu unakwenda hakuna ambacho kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa na bahati nzuri anaijua vizuri sana Busega kwa sababu alikuja Busega na wananchi wa Busega wakamkarimu vizuri na wakampa jina la Chifu Masanja, maana yake Masanja ni mtu ambaye anayekusanya watu, ni mtu wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarimu wa watu wa Busega, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi awafikirie kidogo ili mambo yao yawanyookee. Alipokuwa pale mzee alitoa kauli nzito nzito, yeye sio mtu wa kubabaisha, ni mtu wa kauli nzito na vitendo kama alivyo Rais wake. Hebu aende kwa vitendo ili wananchi wa Busega wapate kumbukumbu nzuri ya maneno yake na uchapakazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija suala zima la UKIMWI, Mwenyekiti wa Kamati ya Ukimwi, Mheshimiwa Mukasa

ameniomba nizungumze kidogo. Kwa vile suala hili liko katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa watu ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI naomba wapewe msaada mkubwa, Serikali iwasaidie. Najua kuna baadhi ya halmashauri zimeshaainisha namna ya kuweza kuwasaidia na kushughulika nao, lakini naomba kama jitihada za kiserikali ziongezwe zaidi. Hawa watu wanahitaji msaada mkubwa zaidi na naomba Serikali iweze kuliangalia kwa nafasi ya pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda ni wa kuondoa umaskini kwa Mtanzania. Ni watu wachache ambao wanaweza kufikiri vinginevyo, lakini naamini kabisa kwamba tukiweza kuunga mkono jitihada ya Serikali ya Awamu ya Tano haya yanayotokea mengine ni mihemko tu na sidhani kama mtu anatoka Zanzibar anasema kwamba sukari haiwezi kuja Bara wakati anazalisha tani elfu nane peke yake na mahitaji ni zaidi ya tani elfu kumi na saba mpaka tani elfu ishirini. Sasa mambo mengine haya tunayaibua bila kuwa na sababu yoyote ya msingi na wanasema kama huna takwimu usiseme kitu, unaibua kitu ambacho hakina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sisi Watanzania wote kwa umoja wetu, mali iliyoko Bara ni kama iliyoko Zanzibar, iliyoko Zanzibar ni kama iliyoko Bara na ndiyo Muungano wetu uliposimama katika misingi hiyo. Tunapoanza kusema unajua mali ya Zanzibar haiwezi kuja huku wakati takwimu yako siyo sahihi, naomba Waheshimiwa Wabunge tujaribu kuliangalia hili na tujaribu kuwa makini zaidi, tusichanganye wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chegeni. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na baadaye Mheshimiwa Ally Seif Ungando ajiandae.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba niungane na Wabunge walio wengi walionipa pole katika mkasa ulionipata huko kwetu Wilaya ya Muleba kufiwa na Katibu wa UWT Bi. Paulina Francis aliyekuwa shujaa wa chama tawala na kwa kweli Wabunge wa Kagera tulio wengi humu ametusaidia, kwa hiyo, nasema kwamba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na waliotangulia kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Timu yake, Waziri wa Nchi na Manaibu na Makatibu Wakuu wao kazi wanayofanya inaonekana na kwa kweli ni nzuri inatia moyo na ni kazi ambayo inakwenda kwa ufanisi mkubwa, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nitakayoyasema ni kwa nia na mantiki ya kuboresha kwa sababu kazi ya Bunge ni kutathmini kazi za Serikali, kutoa maoni na kutoa ushauri, kwa hiyo, ieleweke hivyo lakini kazi ni nzuri. Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa muda mfupi ameonesha kwamba mambo yanawezekana. Kama alivyosema Mwalimu Nyerere *it can be done, you play your part*. Kwa hiyo, sasa sisi hapa kazi yetu tuna-*play our part* kwa kuonyesha zile changamoto ambazo tungeomba Waziri Mkuu kwa nafasi yake na nyingine ni za kisekta aandamane na wale watendaji wengine kuziboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mantiki hiyo basi naomba kabisa nianze na sekta muhimu sana, mimi ni mwakilishi wa wakulima, wavuvi na wafugaji. Wafugaji bado suala lao la ardhi ni kizungumkuti katika mikoa ya ziwa. Nasimama hapa tusisahau tulipotoka. Sasa hivi baada ya kuondolewa kwenye hifadhi kwa sababu ya kuzilinda, wengi wanahangaika na suala la ardhi ya ufugaji bado halijakamilika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweke nguvu yake mwenyewe kuhakikisha kwamba tunahitimisha jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa pia niko hapa kuwakilisha wavuvi, Mheshimiwa Chegeni ambaye amenitangulia kuzungumza hapa amezungumzia sintofahamu na kwa kweli dhahama iliyowakuta wavuvi naomba nipaze sauti kwa kusema kulinda ziwa ni lazima na ni wajibu wa kila mtu, lakini tunavyolinda ziwa nayo ni muhimu kwa sababu tunapigana na umaskini hatupigani na maskini. Wavuvi walio wengi kipato chao ni cha chini, nyavu zao ziliharibiwa kwa fujo na kwa kukomoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kabisa katika suala hili la kukomoana, Watanzania tuna tabia mbaya ya kukomoana. Mtu anapopata madaraka anamkomoa mwenzake hii haitaleta maendeleo. Kwa hiyo, nataka niseme kabisa kwamba wavuvi walikomolewa, sasa katika kukomoa wavuvi unasababisha ajira zikapotea. Kwa hiyo, hii dhana ya ajira kwa vijana, vijana walio wengi mikoa ya ziwa hususani Muleba Kusini wote wako ziwani ndiyo wanapata ajira. Sasa unaharibu zana zao za kazi badala ya kulinda ziwa, yaani mtu anaweza kusema kwamba ni *total confusion* sasa hapo unataka nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta kwamba hili suala la watu kupata nafasi na kuzitumia kukomoa wenzao napenda kabisa niseme kwamba linatuharibia pale ambapo tungekwenda vizuri zaidi. Kwa hiyo, waliohusika na ukomoaji huu naomba wachukuliwe hatua stahiki kusudi isije ikajirudia tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala la kahawa, wakulima Mheshimiwa Waziri Mkuu atambue kwamba wakulima wamenituma wako kwenye msiba mkubwa sana wakulima wa kahawa, kwa sababu utaratibu huu wa stakabadhi ghalani ambao ni utaratibu mzuri lakini una mazingira yake. Nikizungumza tu kama mtaalam wa sekta hizi ni kwamba kahawa iko tofauti na korosho. Unapouza kahawa wewe unayeuza kahawa ndiyo unahangaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba ni *bias market*, wale wanaonunua kahawa kuna kahawa nyingi duniani imefurika inabidi uwabembeleze. Unapouza korosho ni *sellers market* wewe mwenye mzigo ndiyo unatamba. Sasa naunga mkono kabisa nia ya Serikali ya kufufua ushirika. Katika hilo na kwa uelewa wangu naliunga mkono kwa dhati, lakini sasa ushirika tunaufufua vipi hatuwezi kuufufua kwa kukomoa wakulima sasa na kuwaambia kwamba lazima wote wauze kahawa yao kwa ushirika ambao haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake lazima tukiri kwamba ushirika ulishakufa wengine vyama vya msingi vingine vilishafungwa, kuna buibui na popo kule kwenye stoo, sasa hatujajipanga tunasema kwamba wanunuzi binafsi wasinunue. Naungana kabisa na dhana kwamba wanunuzi binafsi hawawezi kuendeleza wakulima wadogo wadogo, hili nalijua, nalijua tu kama *economist* nalijua kabisa, lakini sasa tutafufuaje ushirika wetu kusudi uwe na tija na uweze kuleta huduma stahiki kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muleba kule kwetu na Kagera kwa ujumla na naamini sehemu nyingine nyingi hata na majirani zangu Kigoma nasikia nao wako hoi. Sasa katika hali hiyo tunataka kusema kwamba suala la kufufua ushirika lisitangazwe kama tukio ni mchakato unaohitaji ulezi wa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo lisimamiwe na Waziri wa Sekta najua kwamba anafanya kazi yake kwa bidii, lakini anahitaji nguvu za Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata na za Mheshimiwa Rais katika kuliongoza suala hili liende vizuri. Hali ilivyo sasa hivi wametangaza shilingi elfu moja kwa kilo wakati watu wanaweza kuuza elfu mbili jamani hata na sisi Wabunge humu posho yetu ikipunguzwa ghafla tutakubali? Kwa hiyo, hii ni dhahama kabisa, hivyo, naomba suala hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kabisa kwamba suala la miundombinu ni muhimu, suala la maji

limeshaongelewa, nami naona kwamba tuweke mfuko wa maji, tuweke fedha stahiki lakini sina budi pia kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie suala la barabara. Barabara hizi baada ya *TARURA* kuundwa tunaweza kujikuta katika hali ambapo wanaweza wakachukua fedha zote wakaweka kwenye barabara moja au daraja moja nyingine zikasimama kwa sababu hakuna usimamizi wa Halmashauri. Kwa hiyo suala la *TARURA* kuripoti kwenye Halmashauri limezungumziwa na wengi na naomba niliunge mkono na nilisisitize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu barabara ya kwenda Lubya wameshaitisha tenda mara tatu; mara ya kwanza wakasema kandarasi hakupatikana; mara ya pili kandarasi alipatikana baadaye wakasema mwenzake amejitoa; mara ya tatu mchakato unaendelea. Kwa hiyo, badala ya kupata barabara ambayo Mheshimiwa Rais ameisimamia, ni ahadi yake, sasa tupo kwenye mchezo wa kuchezeana na kukomoana. Nataka nisisitize suala la kukomoana kwamba halitajenga ustawi mzuri wa Taifa hili, litaturudisha nyuma na ndio tatizo ambalo naliona katika sekta nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kabisa niseme kwamba ajira kwa vijana ni muhimu, lakini katika biashara zao lazima wale wa Serikali wawalee wale vijana. *TRA* hawawezi kuja wanafunga kila duka bila kuuliza wanakuja na minyororo wanafunga biashara. Sasa unapofunga biashara inamaanisha kwamba unaharibu ajira, kodi lazima zilipwe lakini sasa uweke utaratibu, *you must go through the pain* ya kuweka utaratibu sio kutafuta *shortcut* kwa kufunga badala ya kulea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba vyombo vyote vya Serikali Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye ndiye ana sera na naona kuna Katibu Mkuu wa Sera hapa Profesa Kamuzola, watusaidie kusaidia kwamba *regulatory authorities* zote hazikomoi bali zinalea/zinajenga. Wazungu wanasema Roma haikujengwa kwa siku moja, mambo

mengine ni polepole, kodi lazima zilipwe lakini pia kodi ziwe na mahesabu ambayo yamehakikiwa na *auditors. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za Ulaya kila mtu analipa kodi, lakini kila mtu anaweza *audited accounts* kwamba kipato changu ni hiki na kodi yangu ni hii, lakini sasa unakuta mtu hajawahi kufanya biashara hata kidogo lakini anaona kwamba kila biashara ina faida, sio kila biashara ina faida. Kuna biashara zingine zina hasara, kazi ya Serikali ni kuzilea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio mchango wangu lakini naunga mkono hoja na namalizia kwa kumpongeza Waziri Mkuu na kumkaribisha kuja Muleba, Muleba Mheshimiwa Waziri Mkuu nimemkaribisha lakini bado hatujamwona, tunamsubiri kwa hamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Seif Ungando, na baadaye Mheshimiwa Dkt. Kamala na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa wajiandae.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie. Kwanza awali ya yote nishukuru vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi hii kwa sababu sasa Kibiti tunalala usingizi. Hii ni kwa sababu Kibiti ilifikia muda hata mtu anayegonga mlango unamjua kipindi cha usiku unashindwa kwenda kufungua mlango, lakini nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vimefanya kazi ipasavyo Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuiomba Serikali yangu Tukufu kwamba iangalie sasa jinsi gani ya kuboresha maslahi ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Hii ni kwa sababu hawana nyumba za kuishi, vitendea kazi vyao magari

machache kwa hiyo, naomba kila jitihada wapatiwe vyombo vyao ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kwa kuunga mkono hoja kwa sababu hotuba hii ya Waziri Mkuu kwa kweli imegusa maisha ya mtu wa hali ya chini kwa sababu ukiangalia katika sekta zote amezigusia kwa hiyo tuna kila sababu ya kumpongeza jinsi gani anavyofanya kazi na hii ndio kiu ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na afya, katika Wilaya ya Kibiti tunashukuru tumepata fedha ya kukarabati kituo kimoja cha afya Mbwela, lakini kila penye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto bali tuna upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta hii ya afya lakini tuna baadhi ya maboma wananchi walijitolea lakini bado hayajakamilika. Kwa hiyo, naomba mtuangalie kwa jicho la huruma wananchi wa Kibiti mtukamilishie maboma yetu ili yaweze kutoa huduma kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa wa madawa katika vituo vyetu vya afya kwa sababu ule Mfuko wa *CHF* unachangia, lakini moja ya sera ya afya kama mama mjamzito, mtoto chini ya umri wa miaka mitano na mzee zaidi ya miaka sitini matibabu bure. Anapokwenda kwenye kituo kile cha afya inabidi apewe dawa kwa yule mwananchi ambaye anachangia. Kwa hiyo, tuombe Serikali nayo iongeze fungu katika kupeleka dawa katika Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo ndugu zetu na jamaa zetu ambao wanaishi na VVU. Tunafahamu kwamba unapoanza kutumia dawa za VVU lazima upate lishe bora, lakini familia nyingi ambazo hazina uwezo wa kupata lishe hii bora. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma watu hawa wenye makundi maalum, wapewe hata ruzuku ili waweze kupata lishe bora na wanapopata lishe bora wakati wa kutumia dawa hata ule uambukizi unapungua. Kwa hiyo, tusipofanya hivyo maana yake itakuwa maambukizi yanaendelea lakini tukiwapa lishe bora hata yale maambukizi yataweza kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Kibiti pato letu kubwa tunategemea kilimo na tuna kilimo cha aina mbili; tuna kilimo cha biashara na tuna kilimo cha mazao ya chakula. Mazao ya biashara tunategemea zao la korosho, sisi kule kwetu Kibiti korosho ndio dhahabu, ndio makinikia lakini zao hili la korosho linafanya vizuri lakini zipo baadhi ya changamoto ningeomba Wizara husika kwamba sasa watu wanasema kesi ya shamba inaishia shambani, tunaomba aje kule Kibiti yapo makandokando ili tumweleze makandokando hayo ili tuweze kuyamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushukuru kwamba sasa hivi tumepata miche ya korosho bure na kweli wananchi wa Kibiti tumepanda mikorosho mingi ambayo itafanya Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na kipenzi chetu Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo zao la ufuta, ningeomba Waziri mwenye dhamana kwamba sasa aangalie jinsi gani zao hili nalo liuzwe kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa sababu tumeona kwenye zao la korosho, stakabadhi ghalani kwamba mkulima anapata fedha nyingi zenye tija. Kwa hiyo, ningeomba basi na zao hili la ufuta nalo liuzwe kwa mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo mwananchi mkulima anaweza akafaidika na zao lake hilo la ufuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani katika Wilaya yetu mpya ya Kibiti. Mbali na upungufu wa watumishi hao lakini tuna changamoto ya vifaa vya kutendea kazi vikiwemo pikipiki hata Ofisi zao hakuna ambapo sasa yule Afisa Ugani anashindwa kutimiza wajibu wake kwa kukosa vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu elimu, nashukuru Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwamba elimu bure, lakini kila penye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto. Changamoto kubwa ambayo tuko nayo sisi wananchi wa Kibiti moja tuna upungufu wa Walimu, nyumba za Walimu, madawati na madarasa. Kwa hiyo, ningeomba sasa leo Serikali ituangalie kwa jicho la huruma sisi wananchi

wa Kibiti basi ni kale kasungura kidogo na sio Kibiti mtupatie ili tuweze kufikisha lengo la wananchi wetu kupata elimu bure katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu, nafahamu kwamba tuna barabara yetu kubwa ambayo inatoka Bungu kwenda Nyamisati. Barabara hii inatumika na wananchi wa Wilaya mbili na ndugu/jirani yangu hapa Mheshimiwa Dau, Mbunge wa Mafia. Barabara hii kwa kweli ningeomba tuiangalie kwa jicho la huruma kwa sababu kipindi inaponyesha mvua inashindikana kupitika. Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, ningeomba sasa basi mtufikirie ili tuweze kupata barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami ili wananchi wa Mafia na Kibiti waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ujenzi wa gati Nyamisati, nachelea kusema kwamba tatizo nini, kwa sababu tunaambiwa mkandarasi tayari ameshapatikana lakini mpaka leo ujenzi wa gati unashindwa kuendelezwa pale Nyamisati, wakati gati hii ya Nyamisati ikijengwa wananchi wa Mafia jirani zangu watafaidika, lakini na mie vilevile ambaye naishi katika Wilaya ya Kibiti (Nyamisati) nitafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia gati lazima tupeleke kivuko cha kisasa kutoka Nyamisati kwenda Mafia kwamba usafiri unaotumika kwa kweli siku Mwenyezi Mungu anakileta mtihani wake nachelea kusema sijui kitatokea nini kwa sababu hali ya vivuko vyetu ambavyo wanavitumia sio salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo tuna matatizo ya maji katika Wilaya yetu ya Kibiti kwamba upatikanaji wa maji ni kama asilimia 38 tu na vijiji vingi havina maji lakini hata ile miradi ambayo tayari imekamilika bado inasua sua katika kutoa huduma yake kwa sababu tunafahamu maji sio biashara, maji ni huduma. Kwa hiyo niiombe Serikali itenge ruzuku kidogo ipeleke katika miradi ya maji ili iweze kukarabatiwa, ilipe gharama za bili za umeme na kuweza kulipa gharama za vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo iko baadhi yake ni miradi mikongwe, ipo muda mrefu ambayo inatakiwa ifanyiwe ukarabati ili iweze kutoa huduma. Miradi hiyo ni kama wa Jaribu, Bungu, Nyamisati ambayo miradi hiyo yote ingefanyiwa ukarabati na miradi ya Lualuke, Mkenda na Muyuyu ingeweza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Waziri wa Nishati namshukuru sana sasa hivi Kibiti suala lile la umeme kukatikakatika limekuwa historia maana Kibiti tulikuwa umeme kama *indicator* ya gari, unazima unawaka lakini sasa hivi Kibiti tuna umeme wa uhakika ambao tumeunganishwa na Gridi ya Taifa, kwa hiyo sisi kama wananchi wa Kibiti tuna kila sababu sasa ya kutumikia umeme huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ombi kwa Waziri mwenye dhamana kwamba sasa Kibiti tunaomba tupate na Ofisi ya *TANESCO,* kwa sababu kutoka Kibiti kwenda Ikwiriri kuna takribani kilometa 30...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ungando.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Dkt. Kamala na baadaye Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia hoja muhimu iliyo mbele yetu. Naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongezi kwa Serikali yetu na kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika na inafanyika kwa *speed*

ambayo ni kubwa na walio wengi hawakutarajia kama tunaweza kufanya mambo haya kwa *speed* tunayoenda nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tulipoweka mtaalam mshauri ili ashauri nchi za Afrika Mashariki ni kwa namna gani tuendeleze mfumo wetu wa reli, yule mtaalam alitushauri nchi za Afrika Mashariki akasema hizi reli zenu mlizonazo ni vizuri muendelee nazo kwa sababu nyie ni nchi maskini, nyie hamhitaji zinazoenda kwa kasi na hamna fedha za kufanya hayo mambo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tuliokuwepo wakati ule pale Arusha tulikataa na tukamwambia huyo mtaalam mshauri kwamba ni kweli uchumi wetu haujakaa vizuri nchi za Afrika Mashariki, labda hatuhitaji treni zinazokimbia sana kama unavyosema labda bado sisi ni nchi maskini, lakini hatuwezi kukaa hivyo milele, tunabadilika kila siku. Kwa hiyo, tukakubaliana kwamba tutajenga sasa *standard gauge* kwa nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali yetu kwamba tumeonesha njia, nchi zote za Afrika Mashariki tulikubaliana kwamba sasa tujenge *standard gauge* lakini Tanzania tumeanza sio tu tunajenga *standard gauge* lakini pia tunajenga *standard gauge* ambayo tutatumia nishati ya umeme. Hilo ni jambo kubwa nawapongeza sana wanaohusika na tuendelee kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea mambo machache, la kwanza, kuna malalamiko ya wananchi Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, jukumu mojawapo ni kushughulikia malalamiko ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi. Malalamiko yao mengi lakini kwa leo nitazungumzia malalamiko ya wananchi wa Kata ya Kakunyu ambayo yamechukua zaidi ya miaka 18 bila kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mgogoro mkubwa na umechukua muda mrefu, mgogoro wa Ranchi ya Misenyi

pamoja na vijiji vinavyozunguka Ranchi ya Misenyi. Mgogoro huo umechukua muda mrefu, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa wakati umefika tuweze kupata ufumbuzi na ukiangalia kwa umakini.  Mgogoro huo umechangiwa na mambo matatu ambayo tukiamua tunaweza tukayapatia ufumbuzi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza lililochangia sana mgogoro huo ni kwamba, tulipoamua mwaka 2002 kwamba *Ranch* ya Misenyi na *Ranch* nyingine ambazo kuna maeneo makubwa yasiyotumiwa vizuri yawekwe kwenye *blocks* ndogo ndogo na wagawiwe wafugaji wadogo wadogo, lakini utekelezaji ulivyoanza haikufanyika hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia uamuzi uliofanyika ni mzuri, lakini utekelezaji ulipoanza haikufanyika hivyo, hawakugawiwa wafugaji wadogo wadogo badala yake waligawiwa watu wala hawajawahi kuona ng'ombe na wengine wala sio wafugaji na wengine wala hawapo ni marehemu lakini waligawiwa *Ranch.* Sasa mgogoro ukaanzia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kukatokea uamuzi, ulikuwa mzuri tu kwamba ile Ranchi ya Misenyi kwa maeneo ambayo ranchi ilikuwa haiyatumii, basi lazima *NARCO* iyagawe katika *blocks* ndogo kama nilivyosema haikufanyika hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ilikuwa ni kwamba ukiangalia ile ramani ambayo *NARCO* walikuwa wanaitumia na ambayo bado wanaitumia ingawa hawataki kuionesha, ramani ile wanayoitumia wao unapofika Mto Kagera unapovuka tu ramani wanayoitumia *NARCO* inaonesha kuanzia Mto Kagera mpaka kwenye mpaka wa Uganda hakuna mtu anayeishi na hakuna kijiji wala kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanapokaa kwenye meza yao wanagawa wanavyotaka, jambo ambalo

sio sahihi. Maana unapovuka Mto Kagera unakutana na Makao Makuu ya Wilaya, unakutana na Kata nyingi tu na vijiji vingi tu lakini ramani wanayoitumia kugawa *blocks* zinazotuletea matatizo, yenyewe inaonesha unapokatiza tu Mto Kagera hakuna vijiji, kata wala mtu. Sasa kwa utaratibu huo lazima migogoro ya namna hii iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi, leo hii nimeona nishauri ufumbuzi. Nitashauri mambo manne; jambo la kwanza, ni kwamba mipaka ya Ranchi ya Misenyi na Vijiji vinavyozunguka ranchi hiyo ni Mto Kiboroga na Mto Kyaka Kuru, hii ndio mipaka inayoeleweka kwa mtu yeyote yule. Kwa hiyo, ufumbuzi wowote ule ambao hautabainisha kwamba mipaka ya ranchi ni Mto Kiboroga na Mto Kyaka Kuru unakuwa hujatoa ufumbuzi wowote. Kwa hiyo, huo ni ufumbuzi wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi wa pili, iwekwe barabara ya ulinzi na kukagua mipaka kuanzia Mutukula hadi Kakunyu maana ukiwa na mpaka ambao huwezi kuukagua ni kazi bure. Ukiangalia upande wa Uganda wao wana barabara nzuri tu ya kukagua mpaka wao, unapokwenda upande wa Tanzania hakuna barabara. Kwa hiyo, barabara hii ni barabara ambayo lazima tuipe kipaumbele, tuitengeneze kwa haraka na itatusaidia kufanya mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imelia, sababu nyingine sitaendelea nazo nimalizie na mambo mengine matatu ambayo nataka kuyaongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni muhimu, tulikaa Wabunge wa Kagera na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, tumekubaliana katika kikao mambo ya msingi ambayo yakitekelezwa yatamaliza migogoro ya ardhi Karagwe, Muleba na Misenyi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu amuelekeze huyo Mkuu wa Mkoa amletee makubaliano tuliyokubaliana ili aweze kutusaidia kumaliza mgogoro huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile iliundwa Kamati nzuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu na akatoa hadidu za rejea nzuri tu. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwamba atatuletea taarifa ya Kamati hyo, lakini hiyo taarifa siioni na wala haiji Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu taarifa hiyo ije ili tuweze kumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa alichangia kuhusu zao la kahawa, nami nizungumze kidogo tu. Zao la kahawa, kuna maamuzi ambayo yamefanyika, ni utaratibu mpya, mzuri tu. Niseme mambo mawili kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, uuzaji wa kahawa ni biashara na mtaalam wa uchumi Adam Smith alishasema, uchumi huendeshwa na mkono usioonekana *(invisible hand).* Uchumi hauendeshwi na mtutu wa bunduki, wala mizinga. Kwa sababu hiyo, ufunguzi wowote tunaouweka kuendesha uchumi, uuzaji wa kahawa, lazima tulijue hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo napenda kulitoa hapa kwa haraka ni kwamba kama huna muda wa kusoma vitabu, maana duniani vitabu viko vingi. Chagua vichache vya kusoma. Kuna kitabu kimoja kinasema, *Why Nations Fail?* Moja ya sababu kitabu hicho kinasema *Nations fail,* yaani Mataifa mengi hushindwa kuendelea kwa sababu ya kutojenga mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaposema unabadilisha mfumo wa kununua kahawa, hujajenga mifumo ya kununua kahawa, ujue utapata matatizo. Kwa sababu unaposema Vyama vya Ushirika kuanzia sasa vinunue na vinunue vyenyewe tu, aah, shughuli ipo. Kwanza ni lazima ujenge hivyo Vyama vya Ushirika viwe tayari kununua hiyo kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata taarifa kwamba wametangaza bei, wakasema watanunua kwa Sh.1,000/= na Profesa amesema hapa, lakini sio wakulima wa kahawa

ninaowajua. Hao ninaowajua, hamtakaa mwone kahawa yao. Najua tutajidanganya kwamba tuna wanajeshi, tuna nini, watashughulika, watapambana, hiyo ni kupoteza muda bure, kwa sababu wakulima na wao wanajua soko liko wapi. Mkulima siku zote atapeleka kahawa yake kule ambako anajua atapata soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kamala. Tunaendelea na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa na baadaye Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Peter Lijualikali, wajiandae.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa nafasi niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu. Kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na kazi nzuri anayoifanya katika kusimamia. Kwa namna ya kipekee nimpongeze sana dada yangu, Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na ndugu yangu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Mavunde, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kwenye eneo la kilimo. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema kwamba Watanzania walioajiriwa katika Sekta ya Kilimo ni kati ya asilimia 65 mpaka 75. Pamoja na ajira ya Watanzania wengi katika eneo hili, lakini bajeti inayopelekwa kwenye eneo hili ni ndogo sana ikilinganishwa na mahitaji halisi ya kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tulikuwepo kwenye Makubaliano ya Maputo na Maraba ambapo katika makubaliano haya tulikubaliana kwamba asilimia 10 ya bajeti itengwe kwa ajili ya Sekta ya Kilimo. Katika hali ya kusikitisha kabisa, katika eneo ambalo linaajiri watu wengi, hata asilimia tano ya bajeti iliyotengwa kwenye eneo la kilimo haitokani na Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nichukue fursa hii kumshauri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama tunataka tuwasaidie wale wakulima na kama kweli tuna *target* ya kweli kwenda kwenye uchumi wa viwanda, ambapo katika uchumi huo *raw material* ya kutosha inapatikana kwenye eneo hili la kilimo zaidi ya asilimia 85, tutakuwa tunajidanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *we are serious enough* tu-*invest* kwenye eneo hili ili tuwe tuna uhakika kwamba tunaweza kuwasaidia wakulima na ile dhana ya kwenda kwenye uchumi wa viwanda itapatikana kama wakulima wengi watapata fursa za kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano tu, mwaka 2017 kumekuwa kuna mgogoro mkubwa sana. Wakulima wamejitoa, wamelima sana lakini matokeo yake wamepata hasara, tumeshindwa kununua yale mazao kwa sababu tulikuwa hatuna masoko ya uhakika. Naishukuru Serikali kwa kuruhusu kwamba sasa hivi mahindi tunaweza tukauza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* wameomba kwenye bajeti yao shilingi bilioni 86, lakini cha kusikitisha inaonekana Serikali haitaweza kuwapa hata robo ya ile hela waliyoomba. Sasa tutakwenda kweli tunakokusudia? Kwa hiyo, uchumi ule wa viwanda hauwezi kupatikana kama hatutakuwa *serious* kwenye kuwekeza kwenye eneo hili la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha sana, haya ni masikitiko ambayo tunayo wawakilishi wananchi; mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu alikaa na Mawakala wa

Pembejeo lakini mpaka leo halijatoka tamko lolote la Serikali kwamba ni lini watawalipa wale Mawakala wa Pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Waziri Mkuu alipokuja kwenye kusoma hotuba yake hapa, angesema mpaka sasa hivi tumeona Mawakala kadhaa ndio ambao wako *supposed* kulipwa kwenye hili eneo. Sasa Mawakala wanakufa, mali zao zinataifishwa na mabenki kule, hali inazidi kuwa mbaya. Kwa hiyo, nataka Waziri Mkuu atakapokuja kuhitimisha namwomba sana azungumzie hili kwani mawakala wanataka kumsikiliza kule nje, atoe kauli ili waweze kujua kwamba Serikali yao imeamua kuwasaidia kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubali kwamba tunataka tuwekeze kwenye eneo la kilimo, lakini tunawekezaje kwenye eneo hili? Nataka nizungumzie kidogo suala la pareto. Pareto inalimwa nchini hapa, lakini cha kusikitisha kabisa, ile hatua ya mwisho ya kuitengeneza ile pareto ili tupate bidhaa, haifanyiki hapa nchini. Yale *material* yanachukuliwa yanapelekwa Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema tuwekeza sana kwenye eneo hili. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuwahamasishe wakulima katika maeneo mbalimbali, walime pareto kwa wingi ili ile *final product* ipatikane hapa ndani ya nchi. Ikipatikana itatusaidia kama Tanzania kupata hela nyingi katika maeneo haya. *Refining* ifanyike hapa hapa Tanzania. Tukifanya hivyo kwenye eneo hili, tutakuwa tuna uhakika wa kutengeneza ajira ya kutosha ambayo wananchi wetu watapata kutoka kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba ili twende kwenye uchumi wa viwanda, lazima tuhakikishe Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda inafanya kazi *simultaneously.* Wasipofanya kazi kwa pamoja, uchumi wa viwanda utakuwa hadithi katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni eneo la maji. Maji ni uhai. Ukizungumza hapa, hakuna Mbunge ambaye hana tatizo la maji. Sasa sisi kama Wabunge tumekuja na hoja mbalimbali kuhusu kesi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza, sisi kama Wabunge tuliomba Serikali iongeze Sh.50/= kwenye kila lita ya *petrol.* Kwa masikitiko makubwa, katika hotuba ya Kamati ya Kilimo ya mwaka 2015/2016, Bunge lako hili liliazimia kwamba Sh.50/= iongezwe pale, lakini maazimio ya Bunge yanashindwa kutekelezwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, atakapokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu atuambie, kwa nini wanashindwa kutekeleza maazimio ambayo Bunge lako Tukufu limepitisha hapa? Maji ni uhai, lakini kwa masikitiko makubwa sana tuna tatizo. Serikali ilikuwa inatakiwa ipate shilingi bilioni 500 kutoka kwenye Serikali ya India kwa ajili ya kupeleka maji katika miji 17. Serikali inapata kigugumizi gani cha kutokusaini ule mkataba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yangeenda kwenye ile miji 17, nina uhakika kabisa tungepunguza *gap* kubwa la matatizo ya maji katika maeneo haya. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, kwa sababu *Head Prefect* wa Serikali ndio Waziri Mkuu; aje atuambie Serikali iko tayari sasa hivi kusaini mkataba wa shilingi bilioni 500 ili miji 17 iweze kupata maji ya uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia, kwamba imefika wakati sasa uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini uwepo, kwa sababu maji yana tija. Kwa mfano, bajeti ya mwaka 2017 nyingi ambayo tumefanikiwa katika maeneo imetokana na Mfuko wa Maji. Mfuko wa Maji ulitengewa shilingi bilioni 158 na mpaka sasa hivi zimeshatumika shilingi bilioni 130 ambazo zinatokana na Mfuko wa Maji. Asilimia 66 ya bajeti ambayo imetoka kwenye maji inatokana na Mfuko wa Maji. Kwa hiyo, kuna haja ya kuongeza hela kwenye Mfuko huu ili watu walio wengi waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongeza hii shilingi 50, nina uhakika kabisa tutapata shilingi bilioni 316. Tukiamua kila shilingi bilioni kumi tukaipeleka kwenye kila mkoa, baada ya miaka mitatu kutakuwa hakuna kabisa tatizo la maji. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali, sisi ndio wenye wananchi; ukiongeza hiyo Sh.50/= sisi ndio tutakwenda kuwaambia wananchi kwa nini tunataka Sh.50/= iongezwe kwenye maeneo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu, sisi kama CCM, Serikali ya CCM, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tuichukue ajenda ya maji kama ndiyo ajenda ya kufa na kuzikana kusudi tuweze kuwatua akinamama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni eneo la...

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji; Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa sio mhudhuriaji sana wa Vikao vya Bunge kutokana na majukumu yake, lakini leo na jana yuko hapa kwa ajili ya hotuba yake, lakini naona yuko *busy* sana na Waheshimiwa Wabunge, mara zote wakitoka, mmoja anaingia kwenye kiti chake. Kwa hiyo, usikivu ambao anaagiza Mheshimiwa pale kwa Waziri Mkuu, hataweza kuupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo taarifa yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa. *(Kicheko/Makofi))*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa kwa sababu Mbunge mwenzangu anataka Mheshimiwa Waziri Mkuu asikilize zile hoja, sisi Wabunge tunasema nini? Waziri Mkuu ndio *Head Prefect* wa Mawaziri wote, atusikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maazimio *very sensitive* ya Bunge ambayo Bunge lako Tukufu limepitisha, hasa la kuongeza Sh.50/= kwenye tozo ya maji. Wabunge wote kilio chao cha msingi ni maji. Nimesema tu kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunataka tuichukue agenda ya maji kama ndiyo ajenda kuu katika Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni eneo la mifugo na uvuvi. Kuna baadhi ya Wizara kazi yake ni ku-*consume* tu. Wizara ya Miundombinu yenyewe inapewa hela na kutumia tu, lakini kuna baadhi ya Wizara zikiwezeshwa zitakuwa zinapewa hela na zenyewe zinatoa hela. Kwa hiyo, ufike wakati tuziangalie Wizara kama ya Mifugo na Kilimo, kwamba kama ikiwezeshwa vizuri *to some extent* tunategemea kupata hela *(returns)* kutoka kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekuwa ni utaratibu wa kila mwaka kwa hizi Wizara hatowezeshwa fedha za kutosha. Kwa hiyo, ufike wakati tuzisaidie hizi Wizara. Eneo hili ndilo ambalo linatengeneza ajira kwa urahisi kuliko maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo la mwisho ambalo nataka nilizungumze kuhusu maziwa. Hili eneo la maziwa ni *very sensitive.* Kama tunaweza ku-*protect* maziwa yanayotoka nje ya nchi, tutakuwa tumeisaidia nchi yetu kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya kuvilinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgimwa, malizia sentensi yako ya mwisho. Muda wako umekwisha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuvilinda viwanda vya ndani ni lazima tu-*protect* viwanda vyetu kwa kuongeza kodi kwa bidhaa za nje. Kwa masikitiko makubwa asilimia 80 ya maziwa yanayokuwa *imported* kutoka nje ya nchi, yanaliwa na viongozi na taasisi za Serikali. Kwa hiyo, badala ya kusaidia kuvilinda viwanda vyetu vya hapa nchini, sisi tumekuwa ndio tunachangia kuvi-*promote* viwanda vya nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, litoke tamko kama lililotoka kwenye *furniture* kwamba sasa umefika mwisho wa kutumia maziwa kutoka nchi ya nje, hasa kwenye ofisi zetu za Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgimwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Cecilia Paresso na baadaye Mheshimiwa Peter Lijualikali na Mheshimiwa Neema Mgaya, wajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu iliyowasilishwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Tanzania ni nchi ambayo imeingia katika Mfumo wa Vyama Vingi na hayo yametamkwa na yapo katika Katiba yetu. Kama tunatambua Mfumo wa Vyama Vingi, maana yake tunaamini kwamba Serikali inatambua vyama vilivyopo ambavyo vinaunda huo Mfumo wa Vyama Vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Mkuu ameeleza kwamba tuko kwenye Mfumo wa Vyama Vingi takriban miaka 23 leo; na vyama hivi vimeendelea kukua kadri miaka inavyoendelea. Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani inaonesha jitihada kubwa sana za kuua vyama hivi kwa kuvinyima haki yake ya msingi ambayo inapaswa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema haya? Uwepo wa vyama hivi unatambuliwa na sheria, ufanyaji wa

kazi wa vyama hivi umetamkwa katika sheria. Maana yake Vyama vya Siasa vinatakiwa viendelee kufanya kazi ya siasa kwa kuhakikisha vinaendelea kupata wanachama kadri inavyowezekana na kadri ambavyo miaka inazidi kwenda. Haya yamesemwa na Waziri Mkuu katika hotuba yake ukurasa wa 10, amesema:

*"Katika kipindi hiki tumeona ushiriki wa Watanzania katika siasa ukiendelea kuongezeka na uhuru wa kujiunga na vyama vya siasa umeendelea."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza, kama Vyama vya Siasa ili viendelee kupata wanachama, maana yake ni lazima vifanye mikutano ya hadhara kunadi na kueleza sera zake, ndivyo ambavyo mwananchi ataamua sasa ajiunge na chama hiki au aende chama hiki au asiwe na chama mpaka pale ambapo ataweza kuridhika kuamua kujiunga na chama. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Usipoteze muda na wewe.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mbunge anayezungumza kuwa kunadi sera mwisho wake ni kipindi cha kampeni tu. Sasa hivi wananadi sera gani wakati watekelezaji ni sisi wa CCM, tunatekeleza sera yetu ya uchaguzi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina sababu ya kumjibu. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa ya nini sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia, endelea.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naeleza kwamba ili Mheshimiwa Waziri Mkuu tukuelewe kwenye kauli hii kwamba vyama hivi vinaendelea kufanya kazi yake, halafu huku mmebana uwepo wa mikutano ya hadhara, ni kwa uhakika mnalidanganya Taifa hili na mnawadanganya Watanzania. Utaendeleaje kupima kwamba Chama cha Siasa kinakua kama hakifanyi mikutano ya hadhara ikaongeza wanachama? Vyama vya siasa ni kama Makanisa...

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Leo mtu anajiunga, kesho anatoka. Ndivyo hivyo.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe mzungumzaji anayezungumza taarifa kwamba mikutano ya hadhara kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani haijapigwa marufuku. Kwa hiyo, wanaweza kuendelea kufanya mikutano ya hadhara kwenye Majimbo yao na kuendelea kuvuna wanachama. Ukiangalia wako wanachama wengine wanataka kujiunga katika Vyama vya Upinzani, wamevuna mpaka Mbunge. Kwa hiyo, waendelee kufanya mikutano ya hadhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpe taarifa hiyo tu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu wanisikilize vizuri, naongelea Vyama vya Siasa. Siongelei Mbunge wala Diwani. Kwa hiyo Mheshimiwa Vuma naomba unisikilize vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama mnakataza Vyama vya Siasa visifanye mikutano ya hadhara, hamwezi leo kuja hapa Bungeni na kutuambia kwamba vyama hivi vimeendelea kufanya vizuri miaka 26 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma, waasisi wa nchi hii walituaminisha Watanzania kwamba tuna maadui watatu wa nchi hii; umasikini, ujinga na maradhi. Kwa yanayoendelea leo, jambo lingine limeongezeka kwa Serikali iliyopo madarakani, adui mwingine ni Vyama vya Siasa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema haya? Kwa sababu leo tunashuhudia Waheshimiwa Wabunge mbalimbali na Madiwani mbalimbali kila siku ama wanaripoti Polisi au wanakamatwa wanaingia Polisi, wanakaa ndani, waliowaweka ndani wakiridhika kwamba sasa wamekaa ndani kwa muda, wanaachiliwa wanaendelea. Kila leo, ama kuripoti Polisi au kwenda Mahakamani. Hapa tuna Wabunge wengi wana kesi kila kukicha, wanahudhuria Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba Vyama vya Siasa vya Upinzani ni adui mwingine ambaye mmemwongeza. Kwa nini nasema haya? Tumeshuhudia pia kwenye chaguzi ndogo zilizofanyika za marudio, kwanza tumefanya Uchaguzi Mkuu 2015, wananchi wameamua kwa ridhaa yao kuchagua mwakilishi wa chama chochote ambacho walikipenda kwa wakati huo na wakawaweka madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani tuna Wabunge wanaotokana na CCM, tuna Wabunge waaotokana na CHADEMA, tuna Wabunge wanaotokana na *CUF,* tuna

Wabunge pia wa *NCCR* na *ACT.* Ni ridhaa ya wananchi kwenye maeneo yao wakawachagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kiongozi mmojawapo wa CCM anazunguka kuwarubuni na kuwanunua baadhi ya viongozi na Wawakilishi hao ambao wamechaguliwa na wananchi, wanasema wanaunga jitihada wanaingia upande wa pili...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** ...labda inawezekana ikawa ni haki yao, lakini...

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji. Kwanza hana uhakika na anachokizungumza kwa sababu watu wanaohamia CCM ni watu wenye akili timamu. Wengine ni Madaktari na wengine wana elimu za juu. La pili, kazi ya chama chochote ikiwemo cha kwake, ni kuua chama kingine. Kwa hiyo, sioni kitu cha ajabu hapa*. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecillia.

**MHE. CECILLIA D PARESSO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba muda wangu ulindwe, lakini nafikiri uelewa wake ndiyo umempeleka huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana yake ni kwamba hawa... *(Makofi)*

**MHE SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuoni ajabu. Hata wakati wa Firauni, walikuwa wanamuunga mkono Firauni ingawa anafanya mambo ya kifirauni. Kwa hiyo, hatuoni ajabu. Kwa hiyo, mama endelea tu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecillia. *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeipokea hiyo taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba hawa ambao wanarudi upande wa pili inatulazimu kurudi kwenye uchaguzi. Hapa Bungeni tulipitisha shilingi bilioni 4.7 kwa ajili ya Tume ya Taifa Uchaguzi kwa uchaguzi wa dharura endapo itatokea Mwakilishi yeyote amefariki au kwa namna yoyote ameacha nafasi ile. Leo baada ya hizi chaguzi ndogo, tumetumia shilingi bilioni 6.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajiuliza, hivi tunafanya kazi ya kurubuni na kununua wahame upande wa pili; tunarudi tena kutumia fedha za walipa kodi kwenda tena kufanya uchaguzi, huku kuna Watanzania wengi ambao hawana huduma muhimu za kimsingi za kijami! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajiuliza…

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya mwisho hiyo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taarifa ya mwisho, utanisamehe sana Mheshimiwa Cecilia, kuhusu kununuliwa kwa Wabunge ama Madiwani. Nataka nimpe taarifa kwamba wao walimnunua Mheshimiwa Nyalandu, hamkuona kwamba ni gharama kubwa zitatumika kwenye Jimbo la Uchaguzi aliloondoka Mheshimiwa Nyarandu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumzia hapa ni bajeti tunayoitumia bila ulazima wowote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu, naomba unilinde ninapochangia. Kama kuna Mbunge anataka kunijibu, asubiri akipata nafasi na yeye ajibu ninayoyasema. Halafu najiuliza, haya ninayochangia hapa, kama hamjayafanya kwa nini mnahangaika, si msubiri niseme? Kwa nini mnahangaika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia, naomba uendelee na hoja tafadhali.

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Nimesema taarifa ile ya mwisho, naomba.

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Aah! Taarifa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kanuni inaruhusiwa siyo!

**MWENYEKITI:** Mngempa muda tu akazungumza Mheshimiwa Cecilia akamaliza.

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya sema hiyo taarifa yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa anayechangia kwamba tuna *evidence* za *video* na *audio* kwa upande wa Chama cha Mapinduzi wakitongoza

Madiwani ili wahamie upande wa pili. Sasa kama kuna *evidence* kwamba CHADEMA ilimtongoza Mheshimiwa Nyarandu ahamie CHADEMA, waseme. Vinginevyo naku-*support* kwamba wanafanya ubadhirifu wa fedha za Watanzania masikini kwa kununua viongozi na kurudia uchagua *unnecessarily*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tafadhali naomba Mheshimiwa Cecilia...

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Tafadhali, subiri. Kaa chini, Mheshimiwa Cecilia, tafadhali naomba ujikite kwenye hoja. Haya mambo ya kununuana, binadamu mwenye akili hawezi kununuliwa. Tafadhali endelea. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haya, sawa. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wewe mbona umenunuliwa?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni utumiaji mbovu wa fedha za wananchi. Kama tulitenga fedha za dharura endapo kutatokea chaguzi, shilingi bilioni nne, leo tumetumia shiligi bilioni 6.9, kwa nini tusingefikiria kuendelea ku-*save* hizi hela na kuzielekeza kuliko kurudisha wananchi kufanya chaguzi tena kwa sababu watu wameamua kununua watu na warudi upande wa pili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata chaguzi za marudio zilipofanyika, tumeshuhudia ukiukwaji mkubwa wa taratibu nzima za uchaguzi. Uchaguzi huu tulipofanya tumeshuhudia ilikuwa ni uchaguzi kati ya chama kilichosimamisha mgombea; mfano mimi nilienda Siha, nilienda uchaguzi mdogo wa marudio Jimbo la Arumeru Magharibi, tumeona ni uchaguzi kati ya CHADEMA na Jeshi la Polisi. Nilishuhudia Wakala anatekwa Kituoni, Polisi yupo, hakemei, hasemi kitu;

hakuna anayezungumza, maana yake tumeingia kwenye uchaguzi kati ya Vyama vya Upinzani na Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu inaonekana mmeongeza adui mwingine ambaye hamtaki kumsikia wala hamtaki kuona Vyama vya Siasa hasa vya upinzani vikifanya kazi yao, ushauri wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Serikali yako, ni kuleta marekebisho ya Katiba hapa Bungeni tufute Vyama Vingi ulimwengu ujue, dunia ijue kwamba Serikali ya Awamu ya Tano haitaki kabisa Mfumo wa Vyama Vingi, turudi kwenye mfumo wa chama kimoja. Nadhani hiyo ndiyo itakuwa njia sahihi na mtaendelea kufanya mnayoyafanya kwa kadri ambavyo mtataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waasisi wa nchi hii...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia, subiri, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuheshimu uhuru wa kuongea na kulinda uhuru wa Mbunge kutoa maoni yake nataka kuwashauri Wabunge tunapoongelea Taasisi ambazo ziko kikatiba na ambazo zinafanya kazi kubwa sana kwa ajili ya wananchi tuendelee kuheshimu kazi hizo zinazofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu wangu ambao nimeona, hakuna uchaguzi ambao unaweza ukafanyika bila kuhitaji usalama kuimarishwa. Uhalifu wowote unaoweza kufanyika ndani ya nchi au katika nchi yoyote ile duniani, iwe wakati wa uchaguzi ama siyo wakati wa uchaguzi, unahitaji kuwahakikishia wananchi usalama wao kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu umeonesha kwamba mwongeaji chama chake kinaposhiriki kwenye uchaguzi ndiyo kunakuwa na matukio makubwa sana ya uhalifu. Kuna uchaguzi mmoja tulifanya ambapo chama chako hakikushiriki, hakukuwepo na matukio ya aina yoyote ya utekaji wala ya maumivu ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Jeshi la Polisi tupo kwa ajili ya kuwahakikishia wananchi usalama na hatuwezi tukaacha wananchi wakakatana mapanga kwa kigezo cha masuala ya uchaguzi wala ya siasa. Lazima tuwahakikishie Watanzania usalama kwa wakati wote, iwe wakati wa uchaguzi ama siyo wa uchaguzi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge mridhie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa...

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri na nasema ukweli kwenye mambo ambayo yanatakiwa yafanyike. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nafikiri ameshakuelewa. Mheshimiwa Cecilia naomba uendelee.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Wewe Mheshimiwa Waziri utapewa muda wa kujibu hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba tu kumwambia Mheshimiwa Mwigulu kwa sababu unaingia kwenye *Cabinet,* naomba upokee ushauri wangu kumwambia Mheshimiwa Rais Magufuli, tufute Vyama vya Upinzani nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waasisi wa nchi hii walituachia tunu za Taifa zikijikita katika umoja, amani na haki, lakini leo tunashuhudia katika nchi hii hakuna umoja. Umoja ule ambao umejengwa na hawa viongozi ambao walitutoa nchi kwenye utumwa na kwenye ukoloni wakatufikisha hapa tulipo, umoja ule haupo. Kwa nini haupo? Kwa sababu tunashuhudia matamko mbalimbali ya viongozi wakiligawa Taifa. Wakiona wananchi hawa wamevamia ardhi, wanasema hawa msiwabomolee kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia malizia kwa dakika moja, nakuongeza

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa msiwabomolee kwa sababu walinipa kura; lakini wengine wanabomolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwalimu Nyerere alituachia tunu ya umoja, lakini leo tunu hii inavunjwa, tuliachiwa amani na mmeendelea kuimba kwamba amani ipo, hakuna amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wana hofu. Leo tunashuhudia wananchi wanaopotea, wapo wanaouawa na wako wanaotekwa. Amani ambayo ni tunu ya nchi hii, haipo tena. Kumekuwa na vitisho vingi. Naona leo tunalijenga Taifa kwenye hofu. Watanzania wana hofu. Tunu ambayo tumeachiwa na Waasisi wetu leo inavunjwa na viongozi na Serikali iliyoko madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeachiwa tunu ya haki. Haki hii inatiliwa msisitizo kwenye Katiba ambayo ni sheria mama. Katiba inatoa msisitizo wa haki ya Mtanzania kuongea kuonesha hisia zake ama kwa kuandamana ama kwa kuandika kwenye mitandao au kwa kusema chochote ilimradi asivunje sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wanatishiwa, wanakamatwa, wanakuwa na hofu ambazo zimejengwa na watu walioko madarakani, wanachukuliwa hatua kinyume na taratibu, hakuna utawala wa sheria, hatuheshimu wala hatulindi tunu tulizoachiwa na Waasisi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Cecilia Paresso. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Lijualikali, baadaye Mheshimiwa Neema Mgaya halafu Mheshimiwa Agness Marwa, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Awali ya yote, nitoe pole kwa familia ya Diwani, Marehemu Godfrey Luena ambaye aliuawa kwa

kupigwa mapanga nyumbani kwake. Natoa pole lakini nataka niiambie familia yake kwamba Luena hajafa, Luena anaishi. Kile ambacho alikiamini kitaishi, ambacho alikipigania kitaishi hakitafika kwake Kilombero. Tunamheshimu Luena kwa kazi aliyoifanya na tunaamini kazi yake haitapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana hekima ya upinzani wa nchi hii ni upumbavu kwa Serikali ya CCM. Kwa bahati mbaya sana, hekima yetu ni upumbavu; hekima yetu ni tafsiri kwamba ni waoga. Ni bahati mbaya, lakini hekima yetu haitalala, itafanya kazi siku zote ingawa inaonekana ni upumbavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Taifa letu kuna jambo ambalo kwa kweli linaniuma sana. Nichukue mfano tu, watu wana-*post* kwenye mitandao kwamba Mheshimiwa fulani anaumwa au anakaribia hivi, watu wanasema bora aende, bora afe, tumechoka. Kama sisi ni watu wazima wenye akili timamu, wenye upendo wa Taifa letu, unapokuwa na Taifa ambalo kiongozi mkubwa wa Taifa anaumwa halafu wananchi wanasema bora afe; hii inatoa tafsiri mbaya kwa Taifa. Taswira ya nchi yetu inaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema haya maneno kwamba kuna shida, huu ni upumbavu. Tunaposema kuna uonevu katika nchi hii, kwa sababu tumesema, tunaonekana sisi ni waoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye hajui hapa, Bunge lililopita Mheshimiwa Nape na wenzake walisema usalama wa nchi ni mbovu, Kamati ya Bunge iundwe, ile Kamati ikafanya kazi kubwa, ikaenda huko, mpaka leo majibu hakuna. Kwa nini hamna majibu? Hekima hii ni upumbavu kwenu. Mnadhani kuwa mambo ni mazuri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA BUNGE KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba niendelee kutumia kanuni ya 68(1) kuhusu utaratibu. Tumejiwekea utaratibu ndani ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge tunao uwezo wa kuchangia hoja zetu kwa kutumia kanuni na taratibu tulizonazo. Hata hivyo, kanuni zinatuelekeza, tunapochangia ni lazima tuhakikishe kwamba tunachangia michango yetu ndani ya Bunge kwa kutumia lugha ambayo inaruhusiwa ndani ya Bunge na wala isiwe lugha ya kuudhi ambayo inaweza kudhalilisha watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko hapa ndani ya Bunge haiwezekani kwamba tukiwasilisha Hotuba ya Waziri Mkuu katika Serikali yetu, halafu Mheshimiwa Mbunge anasimama hapa ndani anatumia maneno ambayo ni ya kutudhalilisha sisi Serikali nzima hapa ndani ya Bunge kwa kutumia lugha ambayo siyo yenye tafsiri sahihi katika lugha ambazo zinatakiwa kutumika ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu umeelezwa waziwazi kwenye kanuni ya (64). Utaratibu huu wa kikanuni unavunjwa. Naomba sana Mheshimiwa Mbunge asiendelee kutumia lugha zinazovunjwa utaratibu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Kwa utaratibu huo Mheshimiwa ambaye unachangia sasa hivi, naomba urudi kwenye hoja bila kutumia lugha ambayo inaweza kuwaudhi ama kuwafanyia mambo siyo mazuri watu wengine.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mama yangu, nimwambie kwamba lengo langu haikuwa kumuudhi mtu yeyote kati yenu, ama yeyote aliyepo humu ndani, siyo lengo langu. Nami sijafundishwa kumuudhi mtu

yeyote. Nimejaribu kutumia labda neno ambalo naweza nikaeleweka, ila kama limekuudhi, nisamehe. Naamini kwamba umenielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani watu wazima tumekaa wote hapa, tunaona kabisa viashiria vya nchi kuharibika, tunajifanya hatuoni. Ninyi ndio wazee wetu. Tulitegemea muwe wa kwanza kuona haya mambo kwamba yanaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunahubiri mshikamano, umoja na upendo; na mwenzangu Mheshimiwa Mwakyembe alikuja kwenye Kamati, akasema sasa hivi tuna mpango tulete sijui kampeni ya uzalendo kwanza. Unawezaje kuwa na uzalendo kwenye Taifa ambalo Diwani wangu anauawa, kiongozi wangu wa chama anafanyiwa uhuni, mpaka leo kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona mfano, haya magazeti, jambo hilo hilo likiandikwa kwa ajili ya Mheshimiwa Mbowe kwa maneno hayo hayo, Serikali inakaa kimya; Mheshimiwa Waziri anaona raha, anatulia. Jambo hilo hilo, neno hilo hilo likiandikwa kwa kiongozi wa Serikali, gazeti linafungiwa. Huu umoja unatoka wapi? Huu upendo mnaotaka kuhubiri unatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu jambo baya; hata hii sheria wanayosema ya mtandaoni, watu wote ambao wamekamatwa nayo ni watu ambao wanaaminika wanaongea jambo ama wame-*post* kitu ambacho kinakwenda kinyume na Serikali, lakini jambo hilo hilo mtu wa CCM aki-*post*, husikii shida yoyote. Sasa tutajidanganya hapa; amani, amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikia niwaambieni, nchi zozote zile ambazo mambo yameharibika, haikuanza tu siku mambo yakaharibika, mambo yanaanza hivi. Wazee mpo hapa mnaona mambo yanaharibika kwa sababu mnadhani mtakuwapo milele, mnaacha mambo yaende. Mtaharibu nchi yetu ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa. Niongelee sasa kuhusu elimu. Taifa lolote lazima likitaka maendeleo liwekeze kwa watu. *Investment* ya nchi ya kwanza ni kwenye aina ya watu inayotengeneza Taifa. Hii nitasema siyo kwamba nafurahia, Taifa ambalo tunazindua ndege watu wanakwenda kukimbilia kupanda eti kupiga picha. *Come on!* Hii nchi gani? Yaani Watanzania tumekuwa, yaani, khaa! Haya bwana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti, asilimia 70 ya fedha ambazo zimeingia kwenye elimu ni fedha za wafadhili. Fedha zetu za walipa kodi hazijaingia kwenye elimu. Maana yake ni kwamba Taifa letu halijawekeza kwenye elimu. Kama Taifa haliwekezi kwenye elimu, tunawekeza kwenye *Bombadier* na vitu vingine, *its okay*. Tutakuwa na *Bombadier,* tutakuwa na *standard gauge,* vitu vizuri vizuri vitakuwa vinaonekana, lakini vina-*bring impact* gani kwa watu wetu?

**MHE. GUDLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye...

**MHE. GUDLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mlinga ameshamaliza muda wake, tuendelee na Mheshimiwa Mgaya na Mheshimiwa Agness Marwa ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ya kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuhakikisha kwamba anaisimamia Serikali yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa mambo mengi, mazuri, makubwa yaliyofanywa ndani ya miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kufufua Shirika la ndege la Tanzania, lakini vile vile naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuweza kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ndani ya nchi yetu. Tumeona bajeti ya dawa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 252 hadi shilingi bilioni 269. Jamani hili siyo jambo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imeanza ujenzi wa reli ya kisasa ya Kimataifa *(standard gauge),* naipongeza pia. Tumeona barabara za juu zikitengenezwa *(flyovers).* Vilevile Serikali hii ya Awamu ya Tano imeweza kuimarisha ulinzi wa rasilimali zetu zikiwemo madini pamoja na maliasili. Hivi kesho Mheshimiwa Rais anakwenda kuzindua ukuta ambao utakwenda kulinda *Tanzanite* yetu ili isiendelee kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba kuna elimu bure, tunaona takriban shilingi bilioni 20.8 kila mwezi zinakwenda kuhudumia Shule za Msingi na za Sekondari. Naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yote mazuri yanafanywa kwa sababu ya amani na utulivu tuliokuwa nao ndani ya Tanzania. Mambo haya yasingeweza kufanyika kama kuna vurugu na fujo na kama kunakuwa hakuna amani. Naamini amani ipo na utulivu na ndiyo maana mambo haya makubwa namazuri yanaweza kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba anasimamia amani ya nchi yetu; na yeyote anayethubutu kutaka kuharibu amani ya nchi hii ni lazima ata-*deal* naye *perpendicularly. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazuri na upungufu pia upo. Nataka nizungumzie sasa changamoto ambazo ziko ndani ya Mkoa wetu wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu sisi tuna changamoto ya madarasa. Madarasa mengi bado ni chakavu, lakini vilevile tuna uhaba wa Walimu wa Sayansi kwa Wilaya zote; Wanging'ombe, Makete, Njombe na Ludewa. Tunaomba Serikali itusaidie tuweze kupata Walimu wa sayansi kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Wilaya ya Ludewa tuna changamoto ya Walimu wa Shule za Msingi. Tunahitaji Walimu 521 ili kuweza kukidhi idadi ya Walimu katika Wilaya yetu ya Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie suala la Afya. Nakiri kwamba Mkoa wetu wa Njombe tunapokea pesa za dawa zaidi ya asilimia 90, tunaishukuru Serikali, lakini kwenye ile hospitali yetu ya Makambako mnaichukulia kama Kituo cha Afya. Labda niikumbushe Serikali; hospitali yetu ya Makambako ilipandishwa hadhi kuwa hospitali tangu mwaka 2013, hivyo basi, tunaiomba Serikali irekebishe ili tuweze kuletewa dawa kwa kiwango cha hospitali na siyo Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunatambua kwamba Mkoa wa Njombe ni Mkoa mpya, Serikali sasa ione umuhimu wa kujenga Hospitali ya Wilaya katika Wilaya yetu ya Wanging'ombe, lakini vile vile tunaomba Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Njombe Vijijini Jimbo la Lupembe. Ile Hospitali ya Kibena ambayo sasa hivi inatumika kama Hospitali ya Mkoa, tunaomba ipatiwe ukarabati tujengewe *fence* kwa sababu mbwa wanasumbua sana

wagonjwa nyakari za usiku na Wauguzi. Kule kwetu mbwa ni wengi, kwa hiyo, tunaomba mtusaidie katika ukarabati wa *fence* hiyo ya hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kilimo. Kwa sasa Mkoa wetu wa Njombe nafikiri na Mikoa mingine ya Tanzania bado kuna changamoto kubwa sana za pembejeo za kilimo. Pembejeo za kilimo zimekuwa ghali na ilhali mazao bei imeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itazame suala hili la pembejeo za kilimo, wakulima wetu wapate pembejeo za kilimo kwa bei nafuu ili kuweza kuuza mazao yetu kwa bei nzuri, kwa sababu kama pembejeo za kilimo ziko juu, moja kwa moja itaathiri uzalishaji, lakini vilevile na bei za mazao zitaendelea kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 na 2016 kuna Mawakala wetu wa pembejeo za kilimo kutoka Mkoa wa Njombe bado hawajalipwa pesa zao. Naiomba Serikali itoe tamko ni lini Mawakala hawa watalipwa pesa zao hizo za pembejeo za kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kwenda kuzungumzia suala la maji. Suala la maji bado ni sugu Makambako Mjini, Njombe Mjini; baadhi ya maeneo kama Makete na kule Lupembe zaidi ya vijiji asilimia 50 havina maji. Pale Makambako na Njombe kuna tatizo kubwa kipindi cha kiangazi, maji hayapatikani kabisa, ukizingatia kwamba Makambako Mjini na Njombe ni Miji ambayo inaendelea kukua na mahitaji ya maji yanazidi kuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaomba, kuna ule mradi wa fedha za India ambao uko kwenye bajeti, tunaomba sasa zile pesa zitoke ziende zikatumike ili kuweza kuimarisha huduma ya maji katika miradi ile ya maji. Kwa mfano, kama mradi wa Mbukwa wa maji kule Wanging'ombe ili wananchi wetu waweze kuondokana na tatizo hilo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumza suala zima la barabara za Mkoa wa Njombe, nimekuwa nikisimama mara kwa mara ndani ya Bunge hili Tukufu nikiomba barabara za Mkoa wa Njombe. Kama nilivyosema kwamba Mkoa wa Njombe ni mpya, sisi lami yetu tunayo moja tu ambayo inatoka pale Makambako kupita inakwenda Songea. Kwa hiyo, kwa uhalisia, Mkoa wa Njombe bado hatuna barabara kabisa ambazo ziko kwenye kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, basi naiomba Serikali iweze kutujengea barabara zifuatazo: Barabara ya lami kutoka Kibena - Lupembe kutokea Makete ambayo inakwenda kuunganika na Mkoa wa Morogoro. Vilevile kuna barabara ya Njombe – Makete - Kitulo kwenda kutokea Mkoa wa Njombe. Pia kuna barabara ya Njombe - Iyai kwenda kutokea Mkoa wa Njombe; na tuna barabara nyingine ya Njombe – Itoni - Ludewa kwenda Manda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtujengee kwa viwango vya lami ili kuweza kufungua milango ya biashara. Sisi watu wa Njombe tunalima sana, kule Makete kuna mazao ya mbao na viazi. Viazi vyote vinavyoliwa Mjini Dar es Salaam huko vinatoka Njombe. Tunaomba sana Serikali ione umuhimu wa kutengeneza barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema. Tunaendelea na Mheshimiwa Agness Marwa na baadaye Mheshimiwa Maftah Nachuma ajiandae.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi hii. Kwa kweli utendaji wake umetukuka, kuna haja ya kumsifia na kumfagilia sana sana. Pia nampongeza sana Mheshimiwa wetu Waziri Mkuu. Mheshimiwa Rais tunamwita *Bulldozer,* sijui yeye tutamwitaje? Maana ni baba zaidi ya Baba. Anapiga

kazi kuliko chochote. Yeye tumwongezee tumwite Tingatinga. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu, anastahili pongezi za hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia katika Wizara ya Uvuvi. Hili suala la uvuvi kwa kweli linawaumiza wananchi wengi sana na limewakosesha wananchi wengi sana ajira kwa uonevu ambao uko wazi kabisa na Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi anapaswa akae na Watendaji wake au wale wadau wa uvuvi ili wamweleweshe kwa undani zaidi, inawezekana kuna mambo mengine hayajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi nilikuwa ni mvuvi. Kwa uvuvi wa dagaa ukisema ile milimita nane, ni milimita nane ile inavua wale furu wadogo wadogo, siyo dagaa. Labda kama sasa tunaambiwa tusile dagaa, dagaa wawe chakula cha samaki. Kwa hiyo, hili suala kwa kweli halikubaliki kabisa kwa kuwaonea hawa wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai kwamba uvuvi haramu ni kweli kabisa haukubaliki, nasi tunahitaji tule samaki wakubwa. Sasa imefikia hatua uonevu umepitiliza, umekithiri, umevuka mipaka. Hawa watendaji wanatakiwa waangaliwe kwa undani zaidi. Naweza kusema nao pia ni Wapinzani kwa sababu siyo kweli kwamba yaani wao wanawaonea tu wananchi wakati wao wanafanya utekelezaji wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye suala la afya. Kwenye suala la afya, nazidi kusisitiza katika bajeti ya Serikali muiangalie sana Hospitali yetu ya Rufaa, Hospitali yetu ya Mkoa wa Mara ili izidi kuboreshwa na iishe kwa haraka zaidi ili kusudi wananchi wa Mkoa wa Mara na majirani zetu wapate huduma nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Hospitali ya Wilaya ya Bunda, Hospitali ya *DDH*. Kulikuwa kuna malipo ya wafanyakazi ambao baada ya kwenda kuwasikiliza, nilikuta wana madai. Yale madai yalikuwa ni kipindi kile cha uhakiki wa vyeti, bahati nzuri naishukuru sana Serikali yangu sikivu

ilisikiliza na wakaanza kulipwa mishahara. Ila walipoanza kulipwa mishahara kulikuwa kuna malimbikizo yao ya miezi kama mitano, minne hivi ambayo hawajalipwa na mpaka leo hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimsikia juzi juzi tu Mheshimiwa Rais akisema ametoa pesa ambazo zinatakiwa zilipe madeni au mabaki ya watu au wafanyakazi wanaodai madeni yao. Hao wafanyakazi wa *DDH* ni kati ya wale wanaodai hayo madeni. Basi naiomba Serikali iliangalie sana hili, wakalipwe hayo madeni yao wafanyakazi wa *DDH* hospitalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwenye suala la madini. Bado nampongeza tena na tena Mheshimiwa wetu Waziri Mkuu maana tulizunguka naye kwa kweli kwa vijiji vya Mkoa wa Mara sana, mpaka alikula ugali wa mtama kwenye nyumba ya bibi mmoja hivi wa Mkoa wa Mara, ule ugali wetu mkubwa pamoja na furu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyofanya. Nilifika naye mpaka kule kwenyeJimbo langu la Nyamongo. Nasema Jimbo la Nyamongo kwa sababu mimi ndio Rais wa Wabunge wa Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, Majimbo yote yangu. Tulifika naye kule, akaenda kuangalia matatizo ya wale wananchi. Baada ya kuangalia matatizo ya wale wananchi kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukua hatua za haraka kuongea na wale wawekezaji na kufanya mambo mengine ambayo yanatakiwa wale wananchi walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu, hili suala limetumia muda mrefu sana na ndiyo maana leo nalisisitiza hapa, naamini Serikali yangu ni sikivu, basi wale wawekezaji ambao tunawapenda sana Tanzania kwa sababu wanaongeza kipato cha nchi, lakini sasa wasipitilize wakawa wao wameota mapembe. Kule kwetu tunaita kuota *mbhekela* yaani kuota mapembe. Kwa hiyo, tunaomba wasiote mapembe kwa maana ya kwamba

wasifanye uonevu sana kwa wananchi, basi wawalipe fidia yao wale wananchi wa Nyamongo kule mgodini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niende kwenye suala la maji. Naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi iangalie sana Mkoa wetu wa Mara na hasa katika Wilaya yangu ya Serengeti, Bunda, Tarime, Musoma Vijijini, Rorya na kwingineko kwa maana ya kwamba suala la maji limekuwa ni muhtasari ambao unaandikwa na mtoto wa darasa la kwanza. Kwa maana ya kwamba sisi tuna Ziwa la Victoria ambalo linatuzunguka lakini maji yanatoka pale kwetu Musoma, yanatoka pale kwetu Ziwa Victoria yanapelekwa wilaya nyingine au mkoa mwingine, wakati sisi pale pale ndiyo wenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, wewe ndio mke wa kwanza, lakini mke wa pili anapewa nyumba ya urithi wakati wewe mke wa kwanza ndio unapaswa kupata urithi wote. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ingalie sana hili suala la maji kwa kweli kwani Mkoa wa Mara tuna haki kabisa kwanza ya kuenziwa kutokana na kwamba sisi ndio tulikuwa na Mwasisi wa Taifa hili au Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa hiyo, tunapaswa kuenziwa kwa kutokosa umeme wa *REA,* ukipita tunatakiwa tupate, maji tunatakiwa tupate, basi hata ikiwezekana Mkoa wetu wa Mara uwe Mkoa wa maonyesho kwamba huu ndiyo Mkoa aliotoka Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine ni kuhusu Serikali kuangalia Watendaji wa Vijiji na Kata wa darasa la saba waliotolewa kazini. Naomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi; Mheshimiwa Waziri Mkuu amfikishie Mheshimiwa Rais haya maombi yetu kwamba hawa Watendaji wa darasa la saba ni tumetoka nao mbali sana. Wengi wao wanakaribia kumaliza muda wao na wengine wanakaribia kustaafu. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, warudishwe kazini hao Watendaji wa Darasa la VII kwa sababu sasa watakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametutoa mbali, kwa sababu hawa Watendaji ndio waliotusababisha kujenga Shule za Kata, kujenga hospitali zetu na vituo vyetu vya afya. Kwa hiyo, tunapowaacha njiani namna hii, ni kama vile tumewatia jiti wakati wamesimama, tena jiti lenyewe la machoni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu hili suala tunapaswa kuliangalia kwa undani zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuangalia sana kwa undani hili suala la watu wanaoishi na VVU. Kwa kweli mmetoa msaada mkubwa sana, Wizara ya Afya imewapa kipaumbele hawa wagonjwa wa VVU, lakini kipekee kama inawezekana kwa sababu sasa hivi ni watu ambao wanajitambua sasa; katika mikoa yote na wilaya zote ukiwemo Mkoa wangu wa Mara wana vikundi vyao vya ujasiriamali mdogo mdogo. Basi zile asilimia kumi ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri, waangaliwe angalau nao wawe wanakopeshwa. Wanafanya biashara zao au shughuli zao ndogo ndogo ili kusudi waweze kujiwezesha kwa vitu vya dharura ambavyo vinatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nawashukuru sana ndugu zangu wa Upinzani kwa sababu kwa kweli wameongea kitu kizuri sana hata mimi kimenigusa. Sasa kutokana na kwamba na wao ni kati ya watu wanaohamasisha, tusitumie vibaya pesa za Serikali, kuliko kusema tena tuanze huu mchakato wa Katiba kwa sababu ni mchakato ambao sisi Wabunge tutakaa chini na watu wengine kuongelea habari za Katiba, tutakuwa tunalipwa hapa chini. Nafikiri wazo alilooongea pale Mheshimiwa Cecilia Paresso, kwa kweli ni zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nawashauri na kuwaomba kwamba sasa wao wahame tu kwenye hicho Chama chao, wahamie CCM haya mambo yaishe, ionekane moja kwamba CCM ni chama kimoja, kwa sababu inaonekana hata wao wameshakubali kwamba CCM ndiyo chama kimoja, kuliko tukaanza malumbano huku ndani, mara tuandike sijui barua, mara vitu gani, au mmoja kati

yao ajitolee basi aandike pale barua aitume kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, akishaituma pale kwa Msajili wa Vyama vya siasa, basi itakuwa ime...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agness, muda wako umemalizika, naomba ukae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Unaogopa taarifa eeh!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Maftah Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nasoma *degree* ya kwanza pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nilisoma *course* moja, *African Political Thought.* Wakati ule napitia kile kitabu, kuna Mwanazuoni mmoja anaitwa Okodiba Noli, aliwahi kusema kwamba *"a state is political organization with territoriality recognize boundaries and independent government."* Akiwa na maana ya kwamba nchi yoyote ni taasisi ya kisiasa ambayo ina watu wake, ina mipaka yake lakini kubwa zaidi, ina Serikali ambayo ni *independent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia mafuhumu zaidi ya maelezo ya Mwanazuoni huyu, anamaanisha kwamba katika nchi yoyote lazima kuwe na Serikali ambayo kazi yake kubwa ni kulinda rasilimali na kulinda watu wake. Naomba nitumie fursa hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri inayofanya

ya kuhakikisha kwamba inalinda amani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na leo hii sisi kama Wabunge tuko katika Bunge hili tukishiriki mijadala hii ya Bunge kwa amani na utulivu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Jeshi la Ulinzi na Usalama na Jeshi la Polisi kwa kuweza kudhibiti hali mbaya ambayo imetokea miezi kadhaa iliyopita pale Kibiti. Sasa hivi sisi wananchi wa Kusini tunapita kwa amani kabisa. Hii ndiyo dhana ya kwamba nchi yoyote iliyokuwa huru lazima iweze kujilinda na iweze kulinda mipaka yake pamoja na raia wake, nalipongeza sana Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, naomba nichukue fursa hii pia kueleza baadhi ya mambo ambayo kimsingi yanapaswa kufanywa sawasawa wakati tunalinda rasilimali na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 25 mwezi wa Tatu pale Mtwara Mjini, kijana mmoja ambaye anajulikana kwa Abdillah Abdulahman, alikuwa katika ufukwe wa bahari wa maeneo ya Kianga akiwa anajitafutia kitoweo, sisi watu wa Pwani tunaita kumbwa, wale wadudu wa *sea shells;* wakati anajitafutia kitoweo hiki, ghafla wakatokea Jeshi la Polisi ambao tunasema ni kikosi kazi ambacho kimeundwa na Wizara ya Uvuvi na Maliasili, wakawa wamemwita yule kijana. Kijana kwa kawaida, kwa sababu Jeshi letu la Polisi linaogopeka kidogo, alivyoona anaitwa akakimbia. Askari wakaamua kumpiga risasi kisogoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi, wahakikishe ya kwamba wanafanya uchunguzi sawasawa kabla ya kuweza kuchukua hatua hizi za kuweza kuwamiminia watu risasi pale wanapofanya *operation* maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la Mahakama ambapo tulipitisha katika Bunge hili tarehe moja mwezi wa Saba mwaka 2017, tulipitisha sheria hapa ya Mahakama ya Mafisadi Tanzania. Jambo la kusikitisha kabisa,

ukipitia kwenye Halmashauri zetu, kwa mfano, pale Mtwara Mjini, wafanyakazi wa Halmashauri waliweza kutafuna zaidi ya shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasilisha taarifa hizi Serikalini kwa muda mrefu sana, lakini jambo la ajabu ni kwamba wanaotafuna hizi shilingi milioni 800 mpaka shilingi milioni 900 hawapaswi kushtakiwa kwenye Mahakama ya Mafisadi. Sasa ni jambo la ajabu sana! Halmashauri kutafuna pesa zaidi ya shilingi milioni 800, ni pesa nyingi sana, pesa ambazo zingeweza kujenga shule, zingeweza kujenga miundombinu, zingeweza kununua dawa, lakini zinatafunwa na wale waliotafuna hawaitwi mafisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwamba iletwe sheria Bungeni tuipitishe kwamba pesa za Serikali zikitafunwa kuanzia shilingi milioni 200, 300, 400 mpaka 600 bado wapelekwe kwenye Mahakama ile ya Ufisadi. Kuweka shilingi bilioni moja, ni nyingi sana, Halmashauri zetu zinatafunwa sana, tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yanavyofukuliwa makaburi katika maeneo mengine; makaburi yanafukuliwa kwenye vyeti, kwenye taasisi za kiserikali, lakini tulikuwa tunaomba sana wale waliotafuna pesa, mabilioni mengi miaka miwili, miaka mitatu, miaka mitano iliyopita, wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mahakama hii ya Mafisadi iweze kuwachukuliwa hatua. Kwa sababu Wanasheria wanasema kwamba sheria haiendi *retrospective,* lakini kwa sababu Taifa hili limetafunwa sana, Taifa hili tumekuwa masikini hapa kwa sababu ya watu wachache, wajanja wachache ambao tuliwapa dhamana ya kusimamia rasilimali zetu, lakini wamechukua pesa zetu na mwisho wa siku Tanzania tunasema ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukipitia kwenye sekta mbalimbali, kwa mfano, Sekta ya Utalii, mabilioni ya pesa yameweza kutafunwa sana. Jambo la ajabu sana, niliwahi

kuzungumza wakati nachangia mjadala wa taarifa za Kamati hapa; Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Utalii, ukipitia *Olduvai Gorge* ni eneo pekee ambalo binadamu wa kale alipatikana duniani, liko Tanzania, ni *Olduvai Gorge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma ukipitia taarifa za Serikali, *Olduvai Gorge* ilikuwa inakusanya karibu shilingi 1,700,000,000 kwa mwaka. Sasa hivi wajanja wachache wakahakikisha kwamba *Olduvai Gorge* wanaitoa kwenye eneo la malikale na kulipeleka kwenye Taasisi ya Ngorongoro na badala yake sasa hivi linakusanya shilingi milioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ufisadi. Watendaji wana *under estimate* pale kwa ajili ya kujinufaisha wao binafsi. Tunaomba Mahakama hii ya Ufisadi Tanzania, ifanye kazi yake ipasavyo. Tusiseme kwamba eti mpaka pesa ifike shilingi bilioni moja, basi mtu aweze kushtakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hapa nimezungumza pia wakati naanza utangulizi wangu kwamba mtengano wowote wa Kitaifa unataegemea na kugawana fursa hizi sawasawa kama Taifa. Leo hii Tanzania kila kanda ina hospitali ya kanda, isipokuwa kanda ya Kusini pekee, jengo linaanza kujengwa takribani miaka 10 iliyopita hivi sasa, mpaka leo halijakamilika pale Mtwara Mitengo. Mpaka leo jengo la Hospitali ya Kanda ya Kusini limejengwa zaidi ya miaka 10 halijakamilika, lakini maeneo yote kuna Hospitali za Kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshindwa kuzungumza maeneno haya kwa muda mrefu sana. Tumekuwa tukiongea kwa muda mrefu sana kwamba rasilimali hizi za Taifa zigawanywe sawasawa ili kanda nyingine na Kanda ya Kusini pia tuweze kupata Hospitali hii ya Rufaa, pesa ziweze kutengwa kwenye bajeti zinazokuja, nasi Wanakusini tuweze kunufaika na rasilimali hizi za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu sana; na ikumbukwe mwaka 2013 wananchi

wa Mikoa ya Kusini waliandamana sana wakidai rasilimali ziweze kuwanufaisha kama Watanzania wengine. Wapo watu waliokuja kupotosha Watanzania, wakasema kwamba Wanakusini wanahitaji gesi watumie peke yao, kitu ambacho hakikuwa sahihi kabisa. Tulichokuwa tunasema ni kama ilivyo kwenye korosho kwamba korosho zimekusanya mabilioni ya pesa, pesa zote zinapelekwa katika Mfuko wa Hazina na zinatumika kwa ajili ya Watanzania wote kununua dawa, kujenga barabara na miundombinu mingine ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema suala la umeme Kusini limekuwa ni kizungumkuti sana. Tunaipongeza Serikali kwamba imenunua mashine mbili ambazo zinaenda kutoa megawati nane; bado tatizo la umeme litakuwa ni endelevu, ni miezi zaidi ya saba hivi sasa, Mtwara na Lindi hatuna umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili linapelekea viwanda kutojengwa Mtwara. Pia limepelekea wawekezaji kukimbia Mtwara. Tunaiomba Serikali, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ije na mpango wa kudumu wa kuhakikisha kwamba Mikoa hii ya Kusini tunakuwa na umeme wa uhakika ili wawekezaji waweze kuja Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kama Serikali ingeamua kuondoa tatizo la umeme Kusini ingenunua mashine moja tu ambayo inatoa megawati 20; na tulikuwa tunapitia taarifa mbalimbali, Wizara ikaenda wataalam wakaenda kuangalia Ujerumani, kuna mashine moja ambayo itaweza kutoa megawati 20 za umeme ambazo zitaweza kusambaza umeme Mtwara na Lindi, inauzwa shilingi bilioni 50 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali kweli ingekuwa na nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba inataka kuondoa tatizo la umeme Kusini, basi ingeweza kununua mashine moja ya megawati 20, inauzwa shilingi bilioni 50, siyo nyingi. Kwenye korosho tunakusanya *billions of money* ambazo zinasaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie kwa jicho la kipekee kabisa, suala hili la umeme Kusini liweze kwisha. Hatutaki kurudi kule tulikotoka, wananchi wanadai sana. Ukifanya mikutano hadhara, kila mwananchi anazungumza suala la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Serikali iliyopita iliweka utaratibu kwamba pale kunapotoka rasilimali yenyewe, hii gesi basi wananchi wapate unafuu. Ikaweka punguzo la kuunganisha umeme, badala ya kuunganisha umeme kwa Sh.370,000/= ikawa Sh.190,000/= hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila mwananchi anakuja kwenye mikutano ya hadhara anauliza kwani hili punguzo ambalo Serikali liliweka kwa nini mmeliondoa wakati gesi ipo? Nami nauliza, gesi bado ipo, kwa nini punguzo ambalo Serikali iliweka kwenye umeme, leo hii Serikali inasema imeondoa punguzo hili? Naomba sana kwamba sekta hii isaidie Wanakusini ili Serikali iweze kusemwa sawasawa na wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuna suala hili la dawa za kulevya. Tunaipongeza Serikali, imeweza kuzuia dawa za kulevya nchini, ni jambo zuri sana, kwa sababu vijana wetu walikuwa hawaeleweki; ilikuwa inapoteza nguvu kazi. Serikali lazima iwekeze vya kutosha kudhibiti uvutaji na uenezaji wa dawa za kulevya Tanzania. Naiomba Serikali, pale inapofikia kuangamiza madawa ya kulevya, kama inavyochoma moto mashamba ya bangi, basi hata tukikamata *Cocaine* na *Heroin* tushuhudie zikiwa zinachomwa hadharani kama zinavyochoma bangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku Serikali imekuwa inatuambia kwamba imekamata kilo 10 kilo 20, gramu sijui ngapi za *Heroin* au *Cocaine,* lakini hatuoni zinaangamizwa au zinachomwa moto. Tunataka Serikali iangamize tukiwa tunaona kama tunavyoona kwenye bangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu, pia hotuba ya Waziri Mkuu imezungumza kwamba inatenga zaidi ya shilingi bilioni 20.8 kila mwezi kupeleka shule za msingi na sekondari kwa maana ya kugharamia elimu ya msingi. Ni jambo jema sana. Wakati huo wa nyuma kulikuwa na michango mingi katika shule ambayo ilikuwa inachangishwa na wazazi. Leo hii ukipita maeneo ya kusini, mzazi ukimwambia achangie hata chakula cha mtoto wake ili mtoto aweze kusoma akiwa ameshiba, kile anachofundishwa aweze kukielewa sawasawa, anasema na Serikali imesema elimu bure. Nani amekwambia uchangie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetamka hapa kwamba michango yote ipitie kwa Mkurugenzi. Mkurugenzi huyu mnamtwisha mzigo mkubwa sana. Haiwezekani leo mpaka mchango wa Sh.5,000/= wa shule ya msingi, shule zote zilizopo za msingi na sekondari akusanye Mkurugenzi. Tunarudisha nyuma elimu yetu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mkurugenzi huyu apunguziwe mzigo na Serikali itoe tamko kwamba suala la chakula cha mchana shuleni kuanzia shule za msingi mpaka sekondari ni jambo la lazima na wazazi lazima wahusike kuchangia chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili limezungumzwa na wenzangu hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Maftaha, malizia sentensi yako.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia suala la migogoro ya ardhi, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imeliona hili kwamba kuna migogoro mingi ya ardhi, ni kweli kabisa. Naitaka Serikali pale ambapo iliahidi kwamba italipa fidia, kwa mfano pale

Mtwara Mjini, Mji Mwema, basi ahakikishe kwamba inalipa fidia za wananchi wale siyo Serikali inakuwa na kauli mbili mbili kwamba, leo wanasema tutatoa fidia maeneo tuliyoyachukua, baadaye inasema Serikali haiwezi kutoa. Tutazungumza haya katika Wizara ya Nyumba, Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha. Waheshimiwa Wabunge huyo ni msemaji wetu wa mwisho kwa muda huu. Kabla sijampa fursa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ili kutoa maelezo kuhusu mwongozo wa Mheshimiwa Mlinga kuhusiana na ajali, naomba niwataje kabisa wachangiaji ambao wataanza jioni.

Tutaanza na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Gibson Olemeiseyeki, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Oran Njenza na Mheshimiwa Daimu Mpakate.

Sasa nampa fursa Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili aweze kutoa maelezo kuhusiana na mwongozo wa Mheshimiwa Mlinga.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze tu kwa kutoa pole kwa familia za ndugu, jamaa na marafiki waliopatwa na mkasa huo wa ajali. Nimpe pole sana Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa sababu tangu jana amehangaika sana na jambo hilo kwa sababu abiria wengi waliokuwa kwenye basi hilo wanatoka kwenye Jimbo lake. Kwa kweli tumeshughulika naye sana kuhakikisha kwamba huduma inapatikana kwa majeruhi pamoja na wenzetu ambao umauti uliwakuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mlinga kufuatana na mwongozo alioomba, nakubaliana kwamba anafanya kazi ya Kibunge kutetea wananchi na hata jana kwenye swali lake aliongelea masuala ya faini,

lakini niseme kwamba taarifa za awali tulizopewa, chanzo cha ajali hiyo siyo mashimo ya barabarani peke yake. Chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi. Kwa hiyo, yule dereva alikuwa anaenda mwendo kasi sana na alipokutana na shimo gari ile ikakata *beam* ile halafu ikawa imepoteza mwelekeo ndipo ikaenda kugonga lile basi la abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kama dereva angekuwa anaenda kwa mwendo unaostahili, kwanza yale hayakuwa mashimo uya kushindwa kupita kwa sababu magari yamepita siku nzima na yeye amekuja kupata ajali baadaye. Kwa maana hiyo, tatizo lilikuwa lile la mwendokasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama jana nilivyosema kwamba, tunapotoza faini, lengo letu siyo kupata ile fedha. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tanawakumbusha kutokwenda kwa mwendo wa kizembe, wa kasi ambao unaweza ukasababisha madhara hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa imeonekana kwamba watu wameshachukua kwa mazoea hayo mambo ya kutoza faini na inawezekana kwenye fikra zao wanaona pia kama vile sisi tunakusanya fedha, lakini hawaoni kwamba tunafanya hivyo kuhakikisha tunalinda usalama kwa sababu wamebeba maisha ya watu na wengine wanategemewa na wengine hawana hatia wanaenda kwenye ajali kwa ajili ya uzembe wa mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naelekeza Jeshi la Polisi popote pale watakapokamata dereva anaenda mwendo kasi, pamoja na hiyo ya kutoza faini, wamweke ndani na wasimwachie mpaka watakapompeleka Mahakamani ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akitoka kule kama rekodi zake ni za mwendo kasi kama nilivyosema jana, anyang'anywe leseni na asiendelee tena kuendesha magari ambayo yanasababisha ajali na kupoteza maisha ya watu kama hivyo ilivyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna rekodi nyingi za watu ambao wanakuja kupata ajali huku wakiwa na risiti ambazo walishaandikiwa za faini na kuona hawa walikuwa wanakusanya hela labda kama ambavyo watu wanachukulia na baadaye wanapoteza maisha. Kwa maana hiyo, hili ni jambo ambalo hatuwezi tukaendelea kulivumilia, tunapoteza maisha, tunapoteza Watanzania ambao hawakuwa na hatia. Wakamatwe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyombo vya mabasi yanayobebea abiria, kila basi liwe na madereva wawili ili ikitokea mmoja ambaye hajui kufuata sheria za barabarani akikamatwa, mwingine aweze kuendelea na safari; ili huyo awekwe ndani na baadaye aweze kupelekwa Mahakamani ili tuweze kuchukua hatua kali ambazo zitahakikishia tunaachana na uzembe huu wa kupoteza maisha ya watu bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye takwimu, zaidi ya ajali 1,500 zimetokana na mwendokasi. Ni kidogo sana kama ajali 89 kuanzia mwaka 2006 ndizo ambazo zinatokana na matatizo ya barabara. Kwa maana hiyo, hatuwezi tukasema ajali hizi zinatokana na ubovu wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi miundombinu katika nchi yetu siyo tatizo. Barabara katika nchi hii ukichukulia kwa ukanda wa Afrika Mashariki, nchi yenye barabara bora ni nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, tatizo limekuja baada ya kuwa barabara ziko bora namna hiyo, madereva wetu hawafuati sheria, wanaendesha kwa kasi, wanaendesha kwa uzembe, ndiyo matatizo kama hayo yanajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tutachukua hatua hizo. Leo hii nitakutana na Waziri wa Ujenzi ili tulijadili hili, ili kama yapo na yale ambayo yanasababisha uzembe ambao unatokana na sheria, tuwatume Watendaji wetu waandae mapendekezo, tunapeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili tuweze kurekebisha, sheria

ziwe kali zaidi kwa wale wanaofanya uzembe wa aina hii, kwa sababu hatuwezi tukaendelea kuvumilia watu wakipotea kwa sababu ya uzembe wa mtu mmoja mmoja ambaye hajali maisha ya watu anaowabeba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mkoa wa kagera walioguswa na jambo hili, pamoja na familia zote ambazo zimepatwa na jambo hili, wawe na moyo wa ustahimilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itachukua hatua kali kwa haya ambayo yamekuwa yakijitokeza ili tuendelee kukomesha tabia hii. Naona imeanza kurudi tena, kwa kipindi kirefu sana tulishaidhibiti kwa kiwango kikubwa na tutatumia na mawazo aliyatoa Mheshimiwa Mwamoto ya kuweza kwenda na kwenye teknolojia ili kuweza kupanua zaidi wigo wa kuwakamata hao wazembe wanaofanya matatizo ya aina hii na kuleta hasara na vilio vikubwa kwa jamii nyingi hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwigulu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo maelezo ya mwongozo ambayo aliouomba Mheshimiwa Mlinga kuhusiana na ajali hiyo, nami kwa niaba ya Bunge natumia fursa hii kuwapa pole wananchi wote wa maeneo ya Karagwe, Kyerwa na Igunga ambao wameguswa na ajali hii. Pia tunawaombea wale marehemu ambao wametangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu awapunzishe kwa amani na wale wote ambao wamepata ajali, basi Mwenyezi Mungu pia awaponeshe kwa haraka kwa nchi nzima.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Khatib Said Haji na baadae Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki ajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa mwanzo jioni yetu ya leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai wake nikaweza kusimama hapa na mimi kutoa mawazo yangu haya ambayo nitayatoa. Kabla ya yote nielezee tu kuridhika kwangu kwa jinsi unavyolisimamia vizuri Bunge hili. Kwa kweli shukrani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kabisa mimi leo nataka nianze na jambo moja ambalo ni kuhusu maswali tunayoleta Wabunge hapa Bungeni. Leo nataka nitumie fursa yangu hii ili kupitia Waziri husika anijibu maswali ambayo kuanzia Bunge la Kumi nikiwa Mbunge niliyapeleka kwenye Ofisi ya Maswali Bungeni sikupata majibu na katika Bunge hili tumekuwa na miaka miwili na nusu maswali hayo pia hayajajibiwa na mpaka sasa tamaa inakuwa ni ndogo. Hivyo naona ni bora nitumie fursa ya muda wangu huu wa kuchangia ili ikimpendeza na nimuombe Mheshimiwa Waziri wakati wa *winding up* ili anipe majibu ya mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kuuliza swali hili na najua liko katika meza ya maswali, Serikali yetu inatumia vigezo gani kuitambua BAKWATA kuwa ndiyo chombo kikuu cha kuwasemea na chenye mamlaka ya uislamu wa Tanzania. Niliuliza hili swali, Serikali inatumia sheria ipi ili kuitambua BAKWATA kwamba ndiyo Baraza Kuu la Waislamu Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza hili kwa kutambua

kwamba Tanzania haina dini na waasisi wa Taifa letu waliweka hilo wazi ili kuepuka mambo makubwa yanayohusu kuingiliana mambo ya dini na kiutendaji wa Serikali. Niliuliza hili kwa sababu waislamu tuna taasisi nyingi kama zilivyo dini zingine. Kuna taasisi nyingi ambazo kwa mujibu wa sheria yetu ya kiislamu ambayo Serikali si juu yake kuingilia utendaji wetu waislamu, kila muislamu ana maamuzi kwa taasisi na Jumuiya anayoiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha sana, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuitambua BAKWATA na kuipa mamlaka makubwa ikiwemo kusimamia hija za waislamu jambo ambalo si haki! Ikiendelea kusimamia mashtaka ya waislamu jambo ambalo pia si haki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu madhehebu haya yanatofautiana na ni jukumu la Waislamu kujiamulia madhehebu wanayoyataka niliuliza hili ili Serikali ituweke wazi, kwanini mmetambua BAKWATA pekee kama ndiyo chombo kikuu cha waislamu Tanzania jambo ambalo haliko kwenye kitabu chetu kitukufu cha *Qurani, Qurani* haitambui BAKWATA, *Qurani* haitambui uamsho, *Qurani* inatambua waislamu na imani yao ya kiislamu. Haya maamuzi tumeyafanya wenyewe waislamu. Kama ambavyo wakristo wana taasisi zao wanazozitambua, haifai kwa Serikali kujiingiza kuitambua BAKWATA. BAKWATA iwaachie waislamu wafanye maamuzi kwa jumuiya. Kwa hivyo natoa wito kwa Serikali kuanzia sasa iache kuitambua BAKWATA kama ndiyo Baraza Kuu la Waislamu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hilo sikujua kama siku moja hata Bunge letu litaingia kwenye mtego. Leo Bunge limewakaribisha BAKWATA kuweka mkutano wa mambo ya kiislamu ndani ya ukumbi wa Bunge hili, jambo ambalo leo hii kila taasisi ikitaka kupewa nafasi hiyo kwa sababu mmeanza kwa BAKWATA itakuwa tatizo, wengine hamtawapa. Kuna Wapentekoste watataka waje mle, Walokole, Walutheri, ndiyo kwa sababu mmeanza njia mbaya! Kuna Uamsho, ni jumuiya halali na mpaka leo

nadhani ina usajili watataka kuja humu, kuna mabaniani wanaabudu ng'ombe wataingia na ng'ombe humu ndani waabudi baa baa! Mko tayari? Haya ni mambo ya kuyaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili niliuliza, Serikali wakati walipomtaka Komandoo Salmin Amour ajitoe katika uhusiano wa Jumuiya ya Kiislamu *(OIC)* ilitoa ahadi kwa Watanzania Serikali ya Jamhuri itaangalia namna bora ya kujiunga ili jambo hili liwe la Kimuungano, Jumuiya ya Kiislamu *OIC.* Ahadi hiyo watu wanaitambua na wawakilishi wao wanatukumbusha tuijulishe Serikali. Kama limewashinda bado Zanzibar kwa maslahi ya kiuchumi, sio ya kidini tunaomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano iachie Zanzibar ijiunge na Jumuiya hii kwa maslahi ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la tatu nililouliza ambalo sikupatiwa jibu. Niliuliza hivi; kulikuwa na utaratibu ambao sio wa kisheria lakini ulikuwa ni utamaduni mzuri. Viongozi wa Mataifa ya nje wanapokuja Tanzania wanapewa nafasi ya kuzuru Zanzibar na sisi Zanzibar tulikuwa tunapata nafasi ya viongozi wetu kuwaambia baadhi ya mambo yetu. Utamaduni huu umeondoka, mtuambie ni kwa nini. Hayo matatu ni maswali ambayo sikupata majibu 2010, naomba leo Mheshimiwa Waziri unijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la vikao vya Makamu wa Rais vinavyohusu kero ya Muungano. Nasikitika sana, kama kuna mambo ambayo nadhani kwa maoni yangu ni mambo ya aibu ni Wanamuungano wa Tanganyika na Zanzibar kukaa Makamu wa Rais na baadhi ya Mawaziri kujadili kero ambazo siku zote hazipatiwi muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa tumeshuhudia, Mheshimiwa Yussuf akizungumzia kuhusu sukari ya Zanzibar kuzuiwa kuingia Tanzania Bara. Suala hili limezungumzwa kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili wamekuja Mawaziri

wamekaa na Mawaziri wenzao wa Bara na suala hili wawakilishi wa wananchi tumepewa tulisemee humu. Kwa hivyo, inapoonekana tunaposemea mambo ya Zanzibar wenzetu inawauma inabidi mvumilie sana kwa sababu kila kitu kina gharama zake. Leo nisingejibu hili lakini nimesikitishwa sana na Naibu Waziri wa Muungano kusimama na akajibu kwamba sukari ya Zanzibar haiwatoshi wenyewe Wanzanzibari, ni kidogo, iweje iletwe huku, jamani! Ni vingi vidogo Zanzibar lakini wananchi wa Bara mwavitumia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vingi vidogo, hata humu Bungeni vimo vidogo vingi, lakini tunavitumia na wala hakuna ubaya ndugu zetu wa damu, wajomba kuvitumia vya Zanzibar kama sisi ambavyo hakuna ubaya kuvitumia vya Bara. Leo ajabu kubwa eti sukari ya Zanzibar inakuwa ni aibu kuingia Bara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo hii Mheshimiwa Yussuf amesema pamba ya Tanzania haitoshi kutengeneza nguo lakini wazalishaji wa pamba wanaruhusiwa kuuza nje wakati tunaaagizia mitumba kuingia Tanzania, aibu iko wapi? Hapa linaloangaliwa na Mheshimiwa Yussuf amemuambia Naibu Waziri, tunazungumza biashara! Leo kiwanda kile kwa udogo wake na idadi ndogo inayozalisha mkikipa fursa ya kufaidi soko la Tanzania Bara kitajipanua na kuongeza ajira kwa Zanzibar. Ninyi kosa lenu mkiiona Zanzibar inaendelea, tatizo lenu nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali jana kupitia Waziri Mahiga alisema Zanzibar inafaidika na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kufaidika kuuza mazao yao katika Soko la Afrika Mashariki. Afrika Mashariki ipi tutaifikia ikiwa daraja la mwanzo ni Tanganyika hamtaki tuguse? Hebu niambieni, tutafika vipi Afrika Mashariki wakati ndugu zetu wa damu mnakataza bidhaa ya Zanzibar kuingia ndani ya Tanganyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu wa damu ikitokea Tanzania ina vita, juzi tumepokea majeneza ya askari

waliokufa kuiteteta heshima ya Taifa letu. Kati yao ilikuwa nusu kwa nusu tumepokea Zanzibar. Mimi binafsi akiwemo mmoja ndugu yangu wa damu. Tumepokea kwa kutetea maslahi ya Tanganyika na Zanzibar. Tanzania tunakuwa pamoja katika maumivu lakini katika kula mnatutupa, huu ni Muungano wa aina gani? Leo tukienda kutetea maslahi na heshima ya Taifa hili Wanzanzibari tunakufa pamoja na ninyi, lakini tukirudi hapa Mzanzibari kuchukua *packet* za sukari kuleta hapa mnasema tunatafuta njia ya kuleta magendo. Mnaidhalilisha Serikali ya Zanzibar kwamba Serikali nzima ya Zanzibar ni Serikali haramu inayofanya magendo. Hili jambo hatuwezi kukubali, binafsi kwa imani yangu simtambui Rais wa Zanzibar kama ni Rais halali, lakini natambua maslahi yanayokwenda Zanzibar kwa sababu yanasaidia wananchi wote wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani maziwa ya Zanzibar mmeyawekea vikwazo, maji ya *Drop* kutoka Zanzibar mmeyawekea vikwazo, kila kitu. Tulikuwa na Kiwanda cha Sigara Zanzibar mmekiua kwa vikwazo, leo mnaitakia nini Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu katika *Qurani* tukufu kuna sura inaitwa *Suratul-Falaq* amezungumzia namna ya uhasidi. Husda mbaya, kisiwa cha Zanzibar mnakiangalia kwa husda, haifai sisi ni ndugu wa damu. Leo hii hasidi huhusudi hata yule maiti kwa sanda aliyozikwa nayo. Hukaa akamwangalia; “hee, sanda yote nyeupe anazikwa nayo huyu” hasidi itamfaa nini sanda maiti na anazikwa? Inamfidia nini ndugu yangu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu rekebisheni, tafadhalini, Muungano huu ni tunu ya Taifa letu, lakini niwaambieni tena kwamba kile kidogo cha Zanzibar mkiruhusu kifaidi soko la Afrika Mashariki, kifaidi soko la Tanzania Bara, vilindeni mna vyombo vya dola mna Polisi, mna *TRA* zote zilizoko Zanzibar ni za Muungano, msituambie sababu kwamba italetwa kwa magendo wakati mnajua mna vyombo vyote vinavyosimamia ni vyombo vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama Kiwanda cha Zanzibar

kinazalisha *packet* 10,000 waacheni wafaidi soko la huku hata wanywaji wa Zanzibar hawafiki 1,000 lakini bia ya Tanganyika inawalewesha Wazanzibari. Wazanzibari hawana Kiwanda cha Bia, wakianguka kwa ulevi ni bia mliyotengeneza ninyi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo soko la nyanya limekuwa kubwa. Mwaka jana nyanya zilikuwa zinaliwa na ng'ombe. Mwaka huu sasa hivi kilo ya nyanya Zanzibar inafika shilingi 4,000. Mkulima wa Dumila hamuwezi kumzuia asipeleke Zanzibar kwa sababu hapa kwetu hazijatosha. Kwa nini iwe Zanzibar? Tunasema haya yanayofanyika siyo halali na sisi Wapinzani ndiyo tunaimarisha Muungano na ninyi wa Chama cha Mapinduzi kwa matendo yenu haya, uhasidi huu, hamuusaidii Muungano wetu. Tafadhalini sana msimchore Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Waziri wewe unafaa kuadhibiwa leo, kwa sababu kumbe ulijua haliwezekani kwanini unamuacha Makamu wa Rais anakaa vikao kujadili jambo ambalo wewe jibu unalo? *Why? It's a shame for you* Mheshimiwa Naibu Waziri, ungemuambia Makamu wa Rais kwenye vikao vyenu vya *cabinet* kwamba hili unalotaka kulisimamia Makamu wa Rais ni jambo lisilowezekana, akaacha kuhangaika Mama wa watu tunamheshimu sana Mheshimiwa Samia, kwa nini? *It's a shame for all CCM.* Kwaherini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Khatib. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Gibson Ole-Miseyeki na baadae Mheshimiwa Mary Deo Muro ajiandae. Mheshimiwa Gibson hayupo, Mheshimiwa Mary hayupo, tuendelee na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na ninampongeza Mheshimiwa Waziri Jenista, mwalimu wangu, mwalimu wa wangi lakini na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, mambo mengi aliyoyaahidi mwaka 2015 tumeona yakiendela kutekelezeka. Aliahidi ndege zitakuja na tumeshuhudia zikija, kwa kweli tunamshukuru sana.

Nashukuru pia kwa mambo yanayoendelea kutendeka katika Mkoa wa Kigoma. Tunashukuru sana kwa miradi ya barabara inayoendelea. Kwa hiyo, ninashukuru sana na ninaomba tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mara nyingi hata anapofanya ziara zake mbalimbali anasikiliza matatizo ya watu na kuyapatia majibu pale pale. Mwaka jana alikuja katika Wilaya ya Kasulu, kulikuwa na kilio kikubwa cha muda mrefu wananchi walikuwa wakililia Hifadhi ya Kagera Nkanda akayatolea majibu pale pale. Wananchi wa Wilaya ya Kasulu wanafurahi, sasa hivi wanalima, wanazalisha mahindi na maharage. Kwa hiyo, wanaendelea kumshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la maji. Nchi yetu imejaaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji ikiwemo bahari, maziwa, mito mikubwa na midogo lakini bado tuna tatizo kubwa la maji. Nilikuwa ninaiomba Serikali kwa kutumia vyanzo hivyo ambavyo tulijaaliwa na Mwenyezi Mungu iweze kuhakikisha maji yanafika vijijini. Wanawake muda mwingi wanatumia nafasi ya kwenda kutafuta maji badala ya kutumia nafasi hiyo katika uzalishaji mali. Kwa hiyo, naomba maji yaweze kufikishwa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kasulu hususan Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Vijijini bado kuna tatizo kubwa la maji na katika Mkoa mzima wa Kigoma

bado kuna matatizo ya maji, Kibondo, Kakonko na maeneo mengine yote. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba maji Kigoma yaweze kufika. Katika Wilaya ya Kasulu viko vijiji ambavyo vinapakana kabisa na Mto Malagarasi lakini kwa bahati mbaya vijiji hivyo havina maji. Naomba Kijiji cha Kitanga ambacho kiko mbali kabisa na kinapakana na Mto Malagarasi kiweze kupatiwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kuweza kufanya watoto waende kusoma bila kulipa ada yoyote na tunamshukuru Rais kwa kuja na sera hiyo. Pamoja na hayo bado yapo matatizo madogo madogo, watoto wameenda shule, wamekuwa wengi, vyumba vya madarasa vimekuwa vichache, nyumba za walimu hazitoshi. Kwa hiyo, naomba kwa kusaidiana na wananchi, Serikali iweze kuhakikisha madarasa yanajengwa ili watoto wetu waweze kupata sehemu ya kusomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ombi hapa, ipo shule moja ambayo kutoka Kasulu Mjini kuelekea katika kijiji hicho ni kilometa zaidi ya 100 na kijiji hicho hakina sekondari ya kata. Ili watoto waweze kupata elimu, wanatembea kilometa 50 kutoka Kitanga kwenda Helushingo kwenda kutafuta elimu ya sekondari. Kwa vile wananchi walishaonesha bidii ya kufyatua tofali na kuanza kujenga, naomba sasa Serikali iangalie ni jinsi gani itawasaidia ili waweze kukamilisha vyumba vya madarasa wanafunzi waweze kupata madarasa ya kusomea na waepukane na safari ndefu ya kwenda kutafuta elimu katika Kata ya Helushingo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Profesa Ndalichako, amekuwa akifanya ziara nchi nzima na tumeshuhudia ziara zake zimezaa matunda, pale alipopita madarasa yameboreshwa na ninamshukuru hata Kigoma Sekondari imeweza kunufaika na ziara zake, lakini na Chuo cha Ualimu Kasulu nacho kimeweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishukuru Mawaziri wote, ziara wanazozifanya kwa kweli, wanakopita

huku na kule tunaweza kunufaika. Mwaka jana Mheshimiwa Ummy alizunguka katika Mkoa wa Kigoma tuliweza kunufaika tukapata magari nane kwa ajili ya Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, ninaendelea kuwapongeza Mawaziri kwa ziara zao. Bado tunalo tatizo la watumishi katika vituo vya afya, katika zahanati na hata katika hospitali za Wilaya. Kwa mfano katika hospitali ya Wilaya ya Kasulu, wauguzi hawatoshi, waganga hawatoshi. *Nurse* mmoja anaweza akahudumia wodi moja akiwa yeye peke yake amuwekee mgonjwa maji, ahangaike kwenda kupima *temperature,* kwa kweli tunaomba Serikali iongeze watumishi katika hospitali ya Wilaya ya Kasulu na hata katika hospitali nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Wilaya mpya zile za Buhigwe na Kakonko nimeona tulitengewa shilingi milioni 500 katika Wilaya ya Buhigwe zimekwenda na hospitali ninaamini itaanza kujengwa, lakini na Kakonko zilishaanza kupelekwa kidogo kidogo. Ninaomba basi, pesa zilizosalia zipelekwe ili tuweze kupata hospitali katika Wilaya ya Kakonko na Wilaya ya Buhigwe ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Uvinza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wahamiaji haramu na wakimbizi; Mkoa wa Kigoma umapakana na nchi ya Burundi na DRC, kuna wimbi kubwa la wakimbizi wanaoingia wengine kihalali kwa kuletwa kwa sababu wanakuwa wameingia wakati ule wa vita na wengine ambao wanapita njia ya panya, kwa hiyo, Mkoa ule una wakimbizi wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano halisi, Kijiji cha Kitanga wanaingia wakimbizi wengi sana. Kwa mfano, pesa hizi zinazotolewa kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye maisha duni, pesa zinazotolewa na *TASAF,* wakimbizi ndio wanaonufaika. Nimeshuhudia wakimbizi 70 wakipewa pesa za *TASAF* wakati wananchi wa Tanzania hawapati pesa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kulalamika kuhusu wakimbizi wanaoingia Kitanga, lakini mpaka sasa hivi bado

wakimbizi wanaingia. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ninaomba kabisa kule Kitanga mtupie macho kule kwa sababu, wakimbizi wanaingia kwa wingi na ndio hao wanaoendelea kunufaika kwa kupata pesa hizo za *TASAF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa naomba niongelee kuhusu uwezeshwaji, jana nimeongea nilipokuwa ninauliza swali la nyongeza. Ninamuomba Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa sababu kule Kigoma tayari kuna vikundi vingi, kuna *SACCOS* nyingi, ninaomba basi kwa sababu mikoa mingine ilishafikiwa na mifuko ile ya uwezeshaji, naomba safari hii katika bajeti hii Mheshimiwa Jenista Mhagama macho yako uelekeze mkoani Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo ninaomba nishukuru, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Josephine, tunaendelea na Mheshimiwa Ally Keissy na Mheshimiwa Charles Kitwanga na Mheshimiwa Oran Njeza wajiandae.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo nami nichangie kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano imetusaidia vituo vya afya viwili vinajengwa, kila kituo kimepata shilingi milioni 500, tunaishukuru sana Serikali, kusema kweli inastahili pongezi za hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi ina miaka 42 haina Hospitali ya Wilaya. Unakuta Wilaya zinaanza miaka mitano iliyopita au miaka 10 iliyopita zina Hospitali za Wilaya, lakini Wilaya ya Nkasi ina miaka 42 tangu imeanzishwa haina Hospitali ya Wilaya, ni kutuletea vituo vya afya tu, ndugu zangu haiwezekani na sisi tunastahili kupewa Hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Nkasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji, kila mwaka napiga kelele hapa, kila Bunge napiga kelele kuhusu miradi ya maji. Miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ndio mmefanya kokoro yaani ni wizi wa hali ya juu. Nashukuru Naibu Waziri wa Maji alikuja na Waziri mwenyewe alikuja na amejionea jinsi wanavyoshirikiana namna ya kuziiba hela za Serikali kupitia kwenye miradi ya maji, hasa Wilaya ya Nkasi. Serikali naiomba iendelee kuchukua hatua wote waliohusika, hata kama wamestaafu, wako wapi, wachukuliwe hatua, hata kama wamehamishwa wachukuliwe hatua, ili hela za Serikali zirudi wananchi wafaidike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, tumepata barabara kule lakini barabara ndugu yangu haiunganishi Mikoa miwili ya Rukwa na Katavi. Barabara inaishia Kizi na inaishia Stalike, pale katikati hatujui itakuwaje hamna barabara ya lami. Serikali inasema kwamba Mikoa iunganishwe kwa lami, lakini Mkoa wa Rukwa na Katavi haijaunganishwa kwa lami miaka yote. Ukishafika Stalike hapo ndiyo mwisho wako na ukitokea huku kwangu mwisho wako kwenye Jimbo langu, Kizi ndio mwisho wa lami. Sasa pale katikati ndugu yangu hakuna lami, naiomba Serikali ifikirie sana kuipa lami hiyo barabara ili kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha *VETA;* namuomba Waziri wa Elimu, namshukuru sana Waziri wa Elimu na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kunipatia majengo yaliyokuwa ya wakandarasi kwa ajili ya Chuo cha *VETA* pale Paramawe. Watu wa *VETA* Kanda ya Mbeya wameshakuja kukagua wamekubali kabisa, walitaka tuwape eka 25 kwa ajili ya chuo hicho, sisi tumewapa eka 50. Sasa naomba Wizara ya Elimu iwape nguvu, iwape pesa kumalizia yale majengo, yako majengo 14 tena *grade one* kabisa yale majengo, wamefurahi. Kwa hiyo, naomba Chuo cha *VETA* kianzishwe haraka pale kuna kila kitu, umeme upo, maji yapo na tumewapa eka 50 badala ya eka 25. Kwa hiyo, ninaomba Waziri wa Elimu yuko hapa ananisikiliza, haraka iwezekanavyo ili Chuo cha *VETA* kianzishwe katika Wilaya ya Nkasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri Ziwa Tanganyika. Nafikiri hata asubuhi kuna swali moja liliulizwa kwamba namna ya kupeleka bidhaa Kongo; ndugu zangu bila cheleo cha kuvusha mali pale kati ya Ziwa Tanganyika haiwezekani. Hakuna usafiri wa kuaminika katika Ziwa Tanganyika. Meli tangu Mjerumani, ndugu zangu ninyi wote hamjazaliwa hapa, bado linadurumiza katika Ziwa Tanganyika, haiwezekani, haiwezi kusaidia kupeleka bidhaa Kongo au Burundi au Zambia, haiwezekani. Tunahitaji meli kubwa mpya kwa ajili ya kuhudumia Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea. Asubuhi ndiyo nazungumza hapa kuna Wabunge wengine ndugu zangu wanakuja humu Bungeni hawana Majimbo, anazungumza kabisa Mbunge sijui anatoka wapi, anasema Serikali naipongeza iligawa mbolea kwa uzuri sana nchi hii, ndugu zangu, huyu analima au halimi? Ana wakulima au hana wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuingilia Rais Magufuli, ndiyo tunamshukuru, ndiyo mbolea kufika vijijini kwetu. Yeye anazungumza kwamba waligawa mbolea vizuri na kusifu Serikali tangu mwanzo mpaka asubuhi wakati hajui lolote, hajui hata mbolea inatumika wapi au namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu tunazungumza mambo mengine kuhusu sukari na bidhaa mbalimbali. Haiwezekani mimi mkulima, Serikali ni sawa na familia nyumbani kwako, wewe unalima gunia 10 nyumbani kwako, matumizi yako nyumbani gunia 20 za mahindi, wewe utakuwa huna akili kiasi gani ukauze mahindi yako wakati matumizi yako gunia 20 na umelima gunia 10, utakuwa una akili au mwendawazimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuja hapa unazungumza habari ya sukari ya Zanzibar wakati hata sukari yenyewe wanasema ni magendo, kila siku mnakamatwa na karafuu mnavusha. Mnakamatwa na madumu kule Zanzibar, Tanga, mmegeuza huku Bara ndiyo uchochoro wa kuingiza bidhaa zenu. Madumu ya mafuta yanakamatwa kila kukicha,

inakamatwa sukari kila siku, Bagamoyo mnapakia sukari chini mnaweka mchanga juu, nani hajui, Serikali mnaifanyia mchezo. Dawa yao hawa kunyang'anya vyombo vyao na yule tajiri kumtia ndani, kutaifisha kila kitu, majahazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mzalishe kule, hawa ndugu zangu hawalipi ushuru. *Container* la *spare parts* za pikipiki hawa wanalipa shilingi 5,000,000wakati Dar es Salaam vijana wauza Kariakoo wanalipa shilingi 40,000,000 *container* la *spare* za pikipiki na hakuna pikipiki kule wanaingiza makontena na makontena wanayavusha kwa jahazi kuleta Bara huku, nani hajui? Leo mnageuza uchochoro huku kwetu? Mnataka kututania? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari mnalima tani 8,000 kwa mwaka, matumizi yenu tani 17,000 mtakuwa na akili sawasawa muuze sukari wakati ninyi wenyewe haiwatoshi au hamnywi chai? Kama hamna pesa ya kununua sukari mseme tuwasaidie, siyo kusema sukari inawatosha, inawezekana hawana pesa za kuweza kununua sukari, maana sukari tani 8,000 matumizi tani 17,000 sasa inakwenda wapi hiyo sukari? Mnaagiza sukari za magendo kutoka Seychelles, kutoka wapi Mauritius, mnaingiza sukari kutoka Brazil sukari hailipiwi ushuru, wala haina vigezo, haitakubalika, haikubaliki, sheria ni msumeno.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Toa Taarifa tu.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Khatib.

## TAARIFA

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wafanyabisahara wa Zanzibar kama

walivyo wa kutoka Kigoma, Morogoro, Mwanza wana haki ya kuuza bidhaa zao popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa Zanzibar. Kufaidi soko la Afrika Mashariki, kufaidi soko la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni haki yao. Kama sivyo leo mtukane hapa kwamba Zanzibar, kama hawana haki wafanyabiashara wa Zanzibar kuuza sukari yao, bidhaa zao katika soko la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwaahidi mkituhakikishia hilo tutatoka sote tunaojiamini sasa hivi, kwenye Bunge lenu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Taarifa ni ya kwake, maana hajui hata kulima huyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikiliza kwa makini, nakueleza hivi Mheshimiwa, mimi ni mkulima nalima gunia 10, mahitaji yangu ya kula nyumbani kwangu gunia 20, naweza kuuza gunia 10 zile? Nitakuwa na akili? Niue familia yangu? Wewe uuze sukari huku, baadae uje kununua sukari Bara upeleke Zanzibar una akili kweli? Ndio nilisema hujui biashara, mimi nimeanza biashara wewe hujazaliwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuambia haiwezekani na Waziri wa Fedha yuko hapa, ni lazima kuanzia Tanga mpaka kule Mtwara idhibitiwe barabara mipaka yeyote anayeingiza mafuta ya kula, anayeingiza sukari, anayeingiza *spare* za pikipiki, *spare* za gari, ataifishwe vyombo vyake na yeye mwenyewe kukamatwa. Haiwezekani, tunalipa kodi ushindani wa biashara utakuwa hakuna. Ushindani wanaagiza tani 20,000 Zanzibar ongeza tani 8,000 tani 28,000 matumizi yao tani 17,000 tani 11,000 mkamuuzie nani? Mnageuza dampo huku, hakuna cha dampo huku, ujanja ujanja huo hakuna bwana. Unaogea sabuni halafu unaitupa chooni sabuni unaokota unaenda kuogea tena, haiwezekani.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Toa Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa jinsi Mbunge anavyosema, nashauri pengine huu Muungano uwe mwisho kuanzia leo. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy naomba uendelee.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuzungumzi habari ya Muungano. Tunazungumza habari ya ulipaji wa kodi na ukwepaji wa kodi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mneemeke kwa kuleta bidhaa zenu ambazo hazilipiwi ushuru, ushidani wa biadhara uko wapi? Haiwezekani, kwanza ninyi nawauliza swali moja, mfumo wa kodi wa Kimataifa jiungeni, jiungeni na mfumo wa kodi wa Kimataifa, lakini mmekaa hamjiungi na mfumo wa kodi wa Kimataifa kwa sababu mmezoea kukwepa ushuru.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Keissy…

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Khatib alikuwa anazungumza hapa, mimi nilinyamaza nikawa kimya, sasa nakujibu mapigo...

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mtu mwenye busara unalima mikungu miwili ya ndizi, unakula mitatu, unauza ndizi zote watoto wako wale nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kessy subiri Taarifa ya Mheshimiwa Ally Saleh.

**T A A R I F A**

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji anayesema sasa hivi anapotosha Bunge. Anapotosha kwa sababu akisema kwamba ile bidhaa inayotoka nje inayokuja huku hailipiwi kodi wakati kule kuna Mamlaka ya Kodi ya Jamhuri ya Muungano anapotosha; hilo la kwanza, lakini la pili akisema kwamba ni uwendawazimu mtu kuuza kwa sababu hajajitosheleza naona labda yeye anatakiwa apimwe akili kwa sababu, inategemea mahitaji yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana umezalisha tani 8,000 za sukari, lakini ili uishi inabidi upate chumvi, inabidi upate mafuta, inabidi upate kitu gani, yeye mwenyewe mtu ndio anaamua auze kiasi gani halafu kingine atajua mwenyewe. Sasa hii huruma hii ya kwamba, sukari haiwatoshi kwa nini mnauza? Imetoka wapi mwaka huu? *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa yake na yeye naona akapimwe akili, maana anaacha watoto wake wana njaa anasaidia watoto wa jirani, akapimwe akili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaeleza namna ya ukwepaji wa kodi. Hawa jamaa wamezoea kutuletea bidhaa, nafahamu *container* la *spare* za pikipiki linatozwa shilingi milioni tano hadi milioni sita. Nenda *TRA* pale Dar es Salaam milioni 40 vijana wa Kariakoo wanalipa, tutalinganishaje biashara? Mnateremsha kwenye majahazi usiku, nani hawajui wengi mnaweka bidhaa chini mnaweka mchanga juu, nani hajui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima iwe macho kuangalia uhujumu wa namna hii. Kuanzia Mtwara mafuta…

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wamekamata mafuta Tanga, nani hakuona kwenye *television?*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kwa Mgumba huku.

## T A A R I F A

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzumzaji kwa sababu anazungumza vizuri kwamba Serikali ya Tanzania ya Awamu ya Tano imejipambanua kwamba ni Serikali ya viwanda. Hili suala tulikubaliana ili kulinda viwanda vyetu vya ndani ni vizuri kwamba kama kuna upungufu wa sukari tuwape wale wazalishaji kwa maana ya *Kagera Sugar* na watu wengine kama Kilombero. Tumekubaliana hivyo kama Serikali ya Tanzania, lakini sasa kule upande wa pili hawajafuata sera hiyo, wakawapa watu wengine wote waagize sukari hapa nchini.

Kwa hiyo, kwa maana nyingine tukiruhusu sukari hiyo ikija huku maana yake tuta-*discourage* uzalishaji wa viwanda vyetu hatutavilinda, nilitaka nimpe taarifa huyo mzungumzaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Keissy malizia kwa dakika moja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naipokea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara ya Fedha kuanzia sasa iwadhibiti watu hawa, kila siku kutolewa kwenye *television* mafuta yanakamatwa, inakamatwa sukari, sasa ni kutaifisha vyombo vyao na wenyewe wafunguliwe mashtaka, wafilisiwe mali yao, wataacha kuleta mchezo wa kukwepa kodi. Kukwepa kodi ni kosa ndugu zangu, tunahitaji barabara, tunahitaji dawa katika hospitali, tunahitaji kila kitu kutokana na kodi, hii nchi inaendeshwa kwa kodi, acheni kukwepa kodi ndugu zangu tuwe macho. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hueleweki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Kitwanga na baadae Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuifanya afya yangu iwe njema mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kutoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano. Juzi nilikuwa namsikiliza Profesa Patrick Lumumba wa Kenya anampongeza Rais wetu kama Rais na ametoa *term* mpya ya kiingereza, *The Magufulification of Africa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake na usimamizi mzuri, lakini niipongeze Serikali kwa ujumla wake kwa jinsi ambavyo inatekekeleza *the vision 2025,* hasa hii awamu ya pili ya miaka mitano – mitano na utekelezaji wake unaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge elimu tunaona sasa hivi inavyokwenda vizuri. Tunaona jinsi ambavyo barabara zinajengwa, tunaona ujenzi wa reli,

tunaona upanuzi wa bandari, tunaona jinsi tunavyoendeleza afya hospitali nyingi au *dispensary* nyingi katika vijiji vyetu. Vilevile tumeona ndege zinavyonunuliwa kuhakikisha kwamba tunainua uchumi wetu. Ndege siyo tu kwa ajili ya usafiri, lakini wale wenzetu walioko katika sekta ya utalii watakubaliana na mimi jinsi tunavyopata ndege ndivyo tutakavyokuwa na watalii wengi na watakaokuwa wanaleta pesa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tufanye nini, ili tuweze kuongeza kasi yetu hii ya uchumi. Kwanza kabisa Serikali iangalie upatikanaji wa *resource. Resource* siyo pesa tu ni pamoja na *human resource* na *time factor.* Nilikuwa nikisikiliza mazungumzo yalivyokuwa yanaendelea hapa, *I think we are wasting a lot of resource* inayoitwa *time. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha tunabishana vitu ambavyo viko *obvious* ni kwamba wote ni Watanzania na Watanzania wote tushirikiane na tulikubali kuungana. Tuendelee na hilo kwa msimamo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi ambacho niweze kukizungumzia ni usimamizi wa *resources* hizi na shughuli tunazozifanya. Tunaweza tukaona tunafanya vizuri sana katika Serikali Kuu, kwa sababu tuna Wakuu wa Mikoa, tuna Wakuu wa Wilaya, lakini tukienda kwa wenzetu wa TAMISEMI ambao wanaenda chini ambako tunataka tuone maendeleo ya mtu mmoja mmoja hadi vijijini hali yetu siyo nzuri sana. TAMISEMI ukienda pale Wizarani kwa kweli, wanafanya vizuri sana. Nimpongeze sana Katibu Mkuu pamoja na Mawaziri wanafanya kazi nzuri, *reaction* yao ukipeleka tatizo lako ni *instant,* lakini ni vipi huku chini tume-*fail?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tu namna ambavyo tunaweza tuka-*improve.* Wenzetu katika baadhi ya nchi wanasema ili uwe Diwani lazima uwe na elimu ya kiwango fulani, ili uwe Mbunge lazima uwe na elimu ya kiwango fulani, lakini sisi tukifanya hilo tutakuwa tunavunja Katiba yetu, lakini kuna upande mwingine kwa sababu kuna wanasiasa na kuna watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watendaji katika Halmashauri zetu, hawa Wakurugenzi tunawapataje? Wenzetu hawa walioko katika Wizara husika Wakurugenzi hawa wanapatikanaje? Au ni hawa wanaotuita sisi kuwa msiwasikilize wanasiasa, wakati Wakurugenzi wengi walikuwa wagombea wakashindwa kupata nafasi, kwa hiyo ni wanasiasa waliokosa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa sheria hii mpya iliyokuja, ukitoka kwenye utendaji ukaenda kwenye siasa, *you will never go back* kwenye utendaji, baki huko huko. Umeshindwa umeshindwa, umepata, umepata na ndivyo wenzetu wanavyofanya na lazima hili liwekewe mkazo, ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunakuwa na Serikali inayosimamiwa vizuri. Tunakuwa na sera nzuri, lakini usimamizi wake unakuwa na mapungufu. Hilo nadhani tutaliangalia zaidi na wenzetu wakiliangalia vizuri katika *area* ya *monitoring and evaluation*. Sasa *monitoring and evaluation* kwa kiswahili chake kizuri sina uhakika kwa sababu kiswahili kilianzia huko Pwani, kikapita Morogoro wakachakachua, hapa Dodoma wakachakua, kilipofika Mwanza mimi sikumbuki. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zaidi katika eneo la Watendaji na Madiwani. Madiwani wetu ni watu ambao wamepata Udiwani kwa sababu wana uhuru wa kuweza kutafuta udiwani na wakachaguliwa katika maeneo yao katika Kata zao au kwa kupitia Viti Maalum. Lakini Watendaji hapa kuna *issue*, na hapa Serikali yetu kupitia kwa Waziri Mkuu lazima tujipange vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kichwa changu na kichwa cha Jenista Mhagama ni vichwa viwili tofauti kabisa na uwezo wetu wa kufikiri uko tofauti kabisa, kwa hiyo ni vema tukapima, tukahakikisha kwamba pale anapofaa Jenista Mhagama aende Jenista Mhagama, pale anapofaa Kitwanga aende Kitwanga, lakini hii ya kubeba jumla jumla na wakati mwingine ndugu zetu ife, siwezi kukubaliana na hilo na bahati nzuri ukiwa msema kweli hata ukikaa pazuri watakuondoa tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa unatenda haki kwa kila mtu hata ukikaa Koromije watakuondoa wakupeleke Mtwara. Kwa hiyo, niweze kusema ukweli na iweze kueleweka na ijulikane kabisa hawa wanasiasa katika Halmashauri zetu tuwaacheni wako pale kihalali. Lakini watendaji wetu *let us choose the people who are right to every post*. Tujipime, tujiangalie, tujitazame. *If you are doing the right thing everybody will clap for you*. Kama unafanya ubabaishaji wako, watasema huyu naye. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yetu izungumzwe *as a system,* isizungumze kama *chunk of* shule ya msingi, shule ya sekondari, izungumzwe *as a system,* mfumo mzima *and let us produce real* na tusijali, wenye akili wapewe *resource* waweze kuitumikia nchi hii. Wanaozembea zembea wasipewe, *after all* nchi haiendelezwi na kila mmoja, watu watano wanaweza wakaendeleza nchi. *They think, they deliver, they influence others and the country move. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rudi kwenye Wizara yako.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Rudi na wewe huko ulikotoka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naku-*address* wewe nilinde tu hawa wasinisumbue. *(Kicheko)*

Labda niende kwenye Wilaya yangu kwenye Jimbo langu. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza *TARURA. TARURA* wameanza vizuri sana. Wakati tuna Idara ya Ujenzi tu katika Halmashauri zetu tulikuwa na matatizo kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kitwanga nakuongezea dakika moja.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Looh! nilikuwa na mambo mengi lakini sasa sijui nitasemaje. Nizungumzie maji katika maeneo ya Kanyerere, Koromije, Mamae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba tu nitaomba tena nafasi katika Wizara zinazohusika niweze kuchangia. Tuongeze tena, turudishe tena ziwe dakika kumi na tano jamani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kitwanga. Tuendelee na Mheshimiwa Oran Njeza baadae Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi na mimi naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kwenye miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtizamo tu wa kawaida ujenzi wa reli ya kati watu wanaweza kufikiri ni kitu kidogo sana kwa *Standard Gauge* au ujenzi wa viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege. Hiki ni kitu kikubwa kwa heshima ya nchi yetu na kwa kweli inatu-*position* mahali pazuri sana na *branding* yake kwa nchi yetu nafikiri inatuweka mahali pazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na timu yake. Amefanya kazi nzuri sana na anaendelea kufanya kazi nzuri sana na amefanya ziara Mbeya. Alipofanya ziara Mbeya pamoja na mambo mengine alitembelea kuna meli tatu zimejengwa pale kwenye Ziwa Nyasa. Aliona ni namna gani Watanzania wana uwezo mkubwa, meli mbili zimekamilika na zimeshaanza kazi na zimejengwa na Watanzania. Kwa kweli, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ulichokifanya siku ile ni kitu kikubwa sana na kimeleta hata *impact* kwa majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niwapongeze Mawaziri wote, wamejitahidi wamefanya ziara kwenye majimbo yetu na ziara zake matokeo yake ni mazuri sana. Wote walipokuja kwenye Jimbo langu wameacha matokeo mazuri sana. Sasa naomba nianzie kwenye

miundombinu ambayo ndiyo Serikali yetu imejikita kwa kiasi kikubwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa reli ya kati wa *Standard Gauge* ni kitu kimekuja kwa wakati muafaka, pia na uboreshaji wa bandari umekuja kwa wakati muafaka. Kwa sababu hivi vyote vinaifanya Tanzania iwe ni njia kuu kwa ajili ya kibiashara kwenda kwenye masoko ya kidunia. Napendekeza pamoja na ujenzi wa reli na uboreshaji wa reli ya kati, ningeomba vilevile Serikali ije na mkakati ni namna gani itaifufua *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa maksudi kabisa nilikuwa naangalia wenzetu majirani wanafanya nini leo hii. Nilikuwa naiangalia Msumbiji inafanya nini. Msumbiji ilikuwa katika dimbwi la vita. Usalama ulikuwa mdogo sana. Kwa hiyo, nchi jirani hazikutegemea sana zile bandari zake. Leo hii Msumbiji wanaboresha reli na bandari inaitwa Nakala. Hiyo Nakala ambayo itakuwa ni kati ya bandari kubwa katika ukanda wetu huu wa *Indian Ocean* itapitia katikati ya Malawi na vilevile inaenda kwenye Jimbo linaitwa Tete ambalo jimbo la Tete ni ndani ya Msumbiji hiyo na ni jirani sana na Zambia na ni jirani sana na Zimbabwe.

Sasa sisi kwa biashara yetu ya bandari ambayo kwa kiasi kikubwa nina imani zaidi ya asilimia 75 kwa ajili ya soko la nje inategemea sana sana *border post* yetu ya Tunduma, kwa ajili ya Zambia, Malawi, Congo na kwa kiasi kidogo Zimbabwe. Sasa hawa wenzetu hili soko tayari wameshaliangalia na wameshaanza ujenzi kuna *project* pale ya dola bilioni tano ambayo katika hizo bilioni 300 zinatoka *ADB (African Development Bank),* sasa ikikamilika hiyo je, sisi biashara yetu ya bandari kwa ajili ya nchi hizi za Zimbabwe, Zambia, Malawi na Congo itaathirika namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba Serikali iweke mkakati wa kuiboresha *TAZARA*. Kuna umuhimu sana wa kuiboresha *TAZARA,* kama bandari ina asilimia 75 inazitegemea hizi nchi ambazo leo hii nchi zote hizi zinaangaliwa na wenzetu wa Afrika Kusini, Angola na sasa

hivi Msumbiji tutakuwa tumejiweka wapi kwenye soko la usafirishaji. Kwa hiyo, naomba Wizara itakapokuja Wizara husika, ijaribu kuangalia ni namna gani itaboresha *TAZARA* lakini vilevile ni namna gani tujenge bandari kavu Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo bandari kavu kwa sababu kuna kilomita pale 120 za kwenda ziwa Nyasa, nazo tuangalie kwa ajili ya ushindani ili reli ile itoke Mbeya kwenda ziwa Nyasa kwa ajili ya ushindani ambao wameuonyesha hawa wenzetu wa Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye viwanja vya ndege, kuna Wabunge wengi wameongelea uwekezaji na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe. Ni kweli ni miaka mingi bajeti zimekuwa zikitengwa lakini mpaka leo uwanja hauna taa za kuongozea ndege, uwanja hauna uzio.

Mheshimiwa Mwenekiti, leo hii bidhaa kama maua, bidhaa kama viazi, bidhaa mbalimbali za matunda zinatoka Mbeya kupelekwa kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam kwa sababu hatuna taa kwenye uwanja wa ndege wa Songwe. Naiomba Serikali itoe hizo hela haraka kwa sababu kwa kiasi kikubwa kwanza ukiangalia hata abiria wengi wanatoka nchi zetu hizi za jirani. Tunapata pesa nyingi za kigeni, lakini vilevile tuna-*potential* ya ku-*export* vitu vingi kwa kutumia..., ndege kubwa zinahitaji kutua moja kwa moja kwenye uwanja ule, huwezi ukatumia ndege kubwa ukasema itue kwanza Dar es Salaam ndiyo ije Mbeya. Wenyewe wanataka wakichukua mzigo aende moja kwa moja New York au aende moja kwa moja Russia.

Kwa hiyo, tunaomba ule ukamilishaji wa ule ujenzi na kwa vile ilishatoka kwenye bajeti sioni kama kuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la uzio, ni muhimu sana kujenga uzio kwa ajili ya usalama. Tumeona kiwanja cha ndege cha Mwanza juzi hapa binadamu amehatarisha abiria na ndege na hilo linaweza kuja kutokea kwenye kiwanja cha Songwe kwa vile pembezoni mle watu

wanafuga ng'ombe, ng'ombe wana tabia ya kufukuzana. Sasa fikiria ng'ombe wanafukuzana halafu ndege ndiyo inatua, sijui hiyo hatari nani ataibeba.

Naomba sana Wizara itakapokuja hapa iseme ni namna gani katika hivi viwanja ambavyo ni *potential. Potential* kwanza ni vya mpakani, lakini vilevile ni soko kubwa pia ni viwanja vikubwa tuvimalizie ili biashara na tuweze kupata bei nzuri, tuweze kupata pesa nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la kilimo. Suala la kilimo kila mmoja kaongea kabisa uchumi wetu kwa kiasi kikubwa unategemea kilimo na kweli haipingiki. Lakini nilikuwa najaribu kusoma makala mbalimbali ambazo zinaonyesha ni namna gani kuna hatari ya upungufu mkubwa wa chakula mwaka 2030 mpaka 2050. Tanzania tumejiandaa vipi kwa hilo. Wenzetu ukisoma wamejiandaa sana, wana-*invest* sana ili waweze kukabiliana na hii hali na hiyo sisi tunaiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea kuhusu maji ni namna gani maji yatusaidie kwenye umwagiliaji, ni namna gani maji ya mvua tuweze kuyavuna, bila hivyo mwaka 2030 *target* ya wenzetu kwa kweli itatumaliza na Tanzania kwenye ongezeko la watu inaonekana *speed* yetu ni kubwa, tunaongezeka kwa haraka, lakini uzalishaji wa chakula ni mdogo sana. Kwa hiyo, naiomba Wizara ije na mkakati ni namna gani imejipanga kuhakikisha kuwa mazao ya chakula hayaitwi tu mazao ya chakula, nayo yawe katika orodha ya mazao ya biashara. Hii ya kusema kuna kahawa, cocoa, korosho ndio mazao ya bishara nafikiri ni mfumo wa kizamani, kwa sababu ni mazao ambayo tulikuwa tunategemea fedha za kigeni. Lakini kibiashara leo viazi, mahindi, maharage kwa kiasi kikubwa nafaka ndiyo wakulima wanategemea kwa kiasi kikubwa kama mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nafikiri tusije tukafanya makosa ya kuzuia haya mazao tena kuuzwa nchi za nje. Leo hii Kenya mahindi kwa kiasi kikubwa wananunua

kutoka Uganda. Sasa ukiangalia Uganda wanazalisha mahindi? Mahindi yanayozalishwa Uganda ni tani kama milioni mbili na laki nane tu, lakini Tanzania tunazalisha karibu tani milioni sita.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Oran, muda wako umemalizika.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Daimu Mpakate baadaye Mheshimiwa Victor Mwambalaswa pamoja na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mwalimu Bilago ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa siku ya leo kuchangia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, napenda kupongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini napenda kupongeza kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ikiongonzwa na Rais wetu John Pombe Magufuli. Pamoja na pongezi hizo ningependa kutoa mapendekezo mawili, matatu, naomba sana kwenye hili Waziri wa Fedha anisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 Serikali iliamua kuanzisha *export levy* kwenye zao la korosho, katika hili kulikuwa na utaratibu na sheria ilieleza matumizi halisi ya ile *export levy*. Katika matumizi hayo mojawapo asilimia 65 itarudi kwa wananchi wenyewe na asilimia 35 itaenda Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana naishukuru Serikali ilifanya vizuri ilitoa pembejeo za *sulphur* bure kwa wakulima wetu, ilitoa magunia kwa wakulima wetu bure. Lakini kisayansi tunaweza kusema kwamba siyo bure kwa sababu hakuna zao lolote la biashara ambalo linatoza *export*

*levy.* Lengo la *export levy* ilikuwa ni ku-*discourage exportation of cashew* na ku-*incourage* uzalishaji ubanguliwa wa korosho hapa nchini, hili lengo bado halijafa lipo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hiki ni kizungumkuti mpaka leo hii dalili ya *sulphur* hakuna wala magunia na ile pesa tukitaka tuzungumze ukweli, kila mkulima katika kilo moja ya korosho anachangia zaidi ya shilingi 500 jambo ambalo ni kubwa na kwa kila mkulima ukipiga hesabu mwaka huu uliopita tumepata zaidi ya bilioni 160. Ukipiga hesabu ya asilimia 65 ya bilioni 160 inatakiwa zaidi ya bilioni 100 irudi kwenye sekta ya korosho na huko kwenye sekta ya korosho tayari kuna sheria imesema matumizi ya ile pesa inaenda kwenye utafiti, inaenda kwenye ubanguaji, inaenda kuendeleza zao lenye na hata hizi korosho wanazopanda Singida, sijui wapi, Mbeya inatokana na pesa hii ambayo inazalisha mbegu wanapelekewa wenzetu ili kuzalisha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hili wenzetu na wenzangu tulioko kwenye Kanda ile tunayozalisha korosho ni kilio kikubwa na usione ajabu mwaka 2020 nusu ya hao wasirudi kwa sababu wakulima wanajua kwamba asilimia 15 au dola 160 kwa tani moja inakuwa *charged* kama *export levy*. Leo tunataka kuwanyima haki yao ya kuwapa pembejeo aidha kwa ruzuku au kama tulivyofanya mwaka jana kupewa bure. Naomba sana sheria ifuate mkondo wake, *export levy* imeeleza kwa urahisi, vizuri namna ya kutumia ile pesa kwenye zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ile siyo ya Serikali, pesa ile ni ya wakulima wa korosho. Kama nilivyosema mwanzo zaidi ya shilingi 500 kwa kilo moja imekuwa-*charged* kama *export levy*. Naomba sana jambo hili msitutwishe mzigo, wenzenu tutakuwa kwenye hali ngumu, biashara ya mwaka 2020 inataka kufia hapa kwa sababu jambo hili hakuna asiyelifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nitaweza kuongelea pamoja na hilo kwenye kilimo ni suala la ushirika. Mwaka jana nililiongea sana hapa nashukuru Serikali ni sikivu tayari imeunda Tume ya Ushirika kwa upande wa Mwenyekiti na Makamishna, lakini Tume hii inaishia mikoani, kwenye Wilaya ambako ndiko usimamizi wa ushirika upo hatuna watendaji, tunategemea watendaji ambao wameajiriwa na Halmashauri na wale wanapewa kazi kubwa ya kukusanya mapato tu ya Halmashauri, kazi ya ushirika hii hawafanyi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kuwa Serikali imedhamiria kufufua ushirika, basi ni vema Serikali iendeleze mtandao wa wafanyakazi mpaka maeneo ya Wilayani ili matatizo madogo yaliyotokana na mfumo wa stakabadhi ghalani inatokana na mfumo wetu mbovu wa kusimamia wanaushirika ndiyo maana tumefika hapo tulipo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nimeisifu sana hotuba ya Waziri Mkuu, imesema ina dhamira ya dhati kwenye mazao makuu ya biashara kuweka mfumo wa stakabadhi ghalani. Hakuna asiyejua ndani humu leo tunazungumza vizuri Mtwara, tunazungumza vizuri Lindi, Tunduru kwa sababu ya mfumo wa stakabadhi ghalani. Wakulima wananeemeka sana kwa bei nzuri kwa sababu ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri Mkuu usikate tamaa pamoja na Waziri wa Kilimo. Mtwara haikuwa kazi rahisi watu kuwageuza kufika kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani. Utapata vijembe kwa sababu inakata mirija ya wale wote ambao walikuwa wanafaidika na mfumo ule holela. Naomba sana ili kumsaidia mkulima wa kahawa, tumbaku, pamba kama ilivyofanywa kule Mtwara basi mazao hayo kama dhamira ilivyo yaingie kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuliongelea ni suala la afya. Naishukuru Serikali nimepata kituo kimoja cha afya kinaendelea kujengwa, naishukuru sana

Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Lakini pamoja na hayo nina kata 15, katika kata 15 nina zahanati 21 na katika hizo kata 15 nina vituo vya afya vitano tu, mtu anatembea zaidi ya kilometa 15 kufuata huduma ya afya. Naomba sana hii mikoa ya pembezoni hebu tuangalieni tuna hali ngumu sana kwenye afya. Tunapakana na Msumbiji wateja wengi wanaohudumiwa na zahanati zile wanatoka Msumbiji. Kwa hiyo tunaomba sana jitihada ziendelee kufanyika kuhakikisha kwamba haya maeneo ambayo yako pembezoni yanapewa huduma za afya ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo vituo vyangu hivyo 22 kila kituo au zahanati ina watumishi wawili au mmoja. Kwa hiyo, mmoja akiugua anaenda hospitali maana yake kituo kinafungwa, mmoja akifuata mshahara mjini maana yake kituo kinafungwa. Mwaka jana alikuja Naibu Waziri ambaye sasa hivi ni Waziri kamili wa TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo aliona matatizo ya upungufu wa wafanyakazi Tunduru na alituahidi akasema mko miongoni mwa wale sita ambao mna tatizo kubwa la wafanyakazi. Ukweli afya ya Tunduru inalegalega kwa sababu hatuna wahudumu, tuna ukosefu zaidi ya wafanyakazi 700 wa afya. Sasa hili jambo ni tatizo kubwa na halileti afya kwenye utawala wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo suala la elimu, nitaendelea kushukuru elimu bure lakini nitaeleza mapungufu ambayo yamejitokeza na elimu bure. Tumesajili watoto wengi, wako madarasani, ukitembea huko vijijini utakuta darasa moja kuna madarasa mawili huku 120 huku mi120 wameweka pazia katikati. Huku wanafundisha darasa la kwanza huku wanafundisha darasa la pili, kwa kweli majengo ni tatizo. Hata hayo yaliyokuwepo yamejengwa miaka ya 1975/1970 utawala wa Nyerere, mpaka leo yanauliza tuue lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na majengo hayo vyoo ndiyo kabisa hakuna. Nyumba za walimu ni mtihani, katika hili nashukuru Mkuu wa Mkoa aliyepita alihamasisha sana ufyatuaji wa tofali katika kila kijiji kuwa

na tofali laki moja. Lakini tuliwaahidi kwamba mkiwa na tofali Halmashauri itatoa fedha kununua vile vitu vya madukani, lakini kwa kuwa Halmashauri ile ni kubwa ina jumla ya kata 39 Halmashauri inashindwa. Yale matofali yanageuka kuwa kichuguu, hivi inakuwa mbogo kwetu hata unavyoenda kwenye mikutano ya hadhara swali la kwanza unaulizwa matofali haya yatatumika lini.

Kwa hiyo, naomba sana kwa kuthamini ule mchango wa wananchi wale waliofyatua tofali zile nyingi basi Serikali ione namna ya kusaidia wananchi hawa waweze kupata fedha ili madarasa, vyoo na nyumba za walimu ziweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika hili ni suala la afya ni suala la wagonjwa wa UKIMWI. Kama nilivyozungumza mwanzo zahanati ziko chache, vituo vya afya viko vichache hata vituo vyenyewe vinavyotoa huduma ya wagonjwa wa UKIMWI ni tatizo. Mgonjwa anatembea zaidi ya kilomita ishirini, kumi na tano kufuata dawa. Nadhani imefika mahala pamoja na kwamba misaada inapungua basi tufikirie nilisikia jana hapa kuna marekebisho ambayo yanaweza kufanyika kwenye masharti inayoonesha namna ya kutumia asilimia kumi, basi naomba katika hilo hata angalau mtakapoweka walemavu asilimia mbili au moja basi na hawa wagonjwa wa UKIMWI muwatengee asilimia moja au mbili waweze kujikimu ili waweze kufanya kazi zao vizuri, wapunguze *stress* za maisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na baadae Mheshimiwa Boniventura ajiandae na Mheshimiwa Mwalimu Bilago na Mheshimiwa Aida Khenan.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa hii niweze kuchangia hoja yetu ambayo iko mezani. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi katika Ofisi hiyo, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wote na watendaji wote wa Wizara hiyo wanavyochapa kazi katika Awamu hii ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii naona imejipambanua sana imeweka kipaumbele katika miradi ya miundombinu; miradi ya barabara, bandari, viwanja vya ndege, reli, miradi hiyo ya miundombinu. Miradi hii ni miradi ambayo inachochea ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, ninawapongeza na kuwapa moyo muendelee kuwekeza katika miradi hiyo kwa sababu inachochea sana ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleze pale ambapo aliishia Mheshimiwa mwenzangu Mheshimiwa Oran Njeza Mbunge wa Mbeya Vijijini. Uwanja wa Songwe sawasawa na Serikali mmekula ng'ombe mzima tunashindwa kumalizia mkia, uwanja umejengwa ni mzuri sana, bado kuweka taa za kuongoza ndege, bado uzio na kumalizia jengo la abiria. Mbeya, Nyanda za Juu kote huko kuna fursa nyingi sana ya mazao. Kuna ndizi, kuna maua, kuna viazi, kuna mpunga anaolima Mheshimiwa Haroon, vyote vinahitaji usafiri wa kwenda nchi za nje.

Kwa hiyo, naomba uwekezaji uliobaki ni mdogo sana, kuweka taa kuweka na uzio na kumalizia uwanja wa ndege ni mdogo mno. Naomba Serikali katika bajeti hii ionyeshe nia ya kwelikweli kwamba inamalizia uwanja wa ndege wa Songwe ili biashara iendelee kama kawaida. Inauma sana pale ambapo ndege inatoka Dar es Salaam inafika Songwe inakuta kuna ukungu inageuza kurudi Dar es Salaam ni hasara kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali imalizie mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *Stiglers Gorge* ni mzuri sana utaongeza nguvu kwenye uchumi, utaongeza umeme karibu megawati 2100, lakini mradi huu unategemea

maji, maji ya Mto Ruaha, Mto Kilombero, Mto Rufiji, mto huu unakauka. Mto Ruaha, Kilombero, Rufiji inakauka *seriously*. Ukiuona mto huu ulivyokuwa mwaka 2008 na leo utalia. Mheshimiwa Makamu wa Rais ameenda Iringa kutembelea Bonde la Mto Ruaha akashtuka, ameunda Tume ya kufuatilia mto huo. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili ameenda Kilombero ameona Kilombero, ameona mto unavyokauka na vijito vyake ambavyo vinaingia kwenye mto huo vinakauka naye akaunda tume ya kufuatilia mto huo.

Naomba Wizara zote zinazohusika zikae pamoja ziunganishe vichwa pamoja na Chuo Kikuu cha *SUA*, tuunganishe vichwa na kuurejesha mto huu uweze kuweze kuleta maji kwenye Bwawa la *Stiglers* isije ikawa *white elephant.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee barabara ya Mbeya - Chunya - Makongorosi. Naishukuru sana Serikali imejenga barabara hiyo imefika Chunya kilometa 72, sasa hivi bei ya usafiri kutoka Mbeya kwenda Chunya ni shilingi 3,500 kama ilivyo kwingine kutoka Mbeya kwenda Tukuyu, na wananchi wangu wanaanza kusafirisha mazao kwa haraka kutoka Chunya kwenda Mbeya. Sasa hivi Serikali inaanza mwaka huu kujenga barabara hiyo kutoka Chunya kwenda Makongorosi, naishukuru sana. Wakati huo huo inaanza kujenga kutoka Mkiwa kwenda Itigi ili tukutane katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina ombi; mara nyingi nimeongea hapa kwamba barabara hii ya Mbeya Chunya imekamilika lakini malori yanayobeba mbao yanayobeba tumbaku Chunya - Mbeya yanabeba lumbesa. Wakifika Mbeya ndiyo wanagawa yanakuwa malori mawili, kwa hiyo, barabara inaumia. Hii barabara sasa hivi kwetu sisi ni mboni ya jicho inaumia, naomba Serikali iweke *weigh bridge* hata *mobile weigh bridge* tuweze kuilinda barabara hii, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maji vijijini. Naunga mkono Wabunge wenzangu wengi

wameongelea suala hili na wameiomba Serikali kwamba kama Serikali ilifanya vizuri iliunda *TANROADS* inajenga barabara vizuri, ikaunda *REA* inaweka umeme vijijini vizuri, imeunda *TARURA* imeanza kazi vizuri ya kuweka barabara za vijijini na mijini, umefika wakati wa kuweka Wakala wa Maji Vijijini. Naunga mkono sana hoja hiyo.

Pamoja na hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Chunya alitukuta tuna shida ya maji kwenye Mji wa Chunya akaidhinisha fedha zimetoka na kinajengwa kisima kikubwa sana Chunya na nadhani katika mwezi huu na mwezi ujao kitakamilika, kwa hiyo wananchi wa Chunya kwa asilimia 80 watapata ahueni ya maji. Naomba fedha iliyobaki itolewe kwa muda ili tutatue tatizo la maji kwa wananchi wa Chunya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wananchi wa Mji wa Makongorosi nao wanachimba kisima, kuna wananchi zaidi ya 20,000 wana shida sana ya maji, naomba Serikali nayo ielekeze macho kwa wananchi hawa wa Makongorosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bwawa la Matwiga Serikali imetoa fedha nyingi sana kujenga Bwawa la Matwiga. Bwawa hili likikamilika litaweza kuhudumia kata zaidi ya sita, sasa limechimbwa limejaa maji liko tayari, linasubiri miundombinu ya mabomba, matanki ili tuweze kupeleka maji kwenye kata hizo. Naomba Serikali itoe fedha haraka kwenye bajeti hii ili tukamilishe mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chunya ni moja kati ya Wilaya kumi ambazo ziliteuliwa na Serikali kwamba wajenge Vyuo vya *VETA.* Tukakubali tumetenga eneo lakini mpaka sasa hivi chuo hakijajengwa, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu atakapokuja hapa atuambie ni lini watatoa fedha za kuanza kujenga Chuo cha *VETA* kwa Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo la mwisho, kuna Watendaji wa Vijiji na wa Kata. Watendaji hawa wamekuwa wana sakata refu sana na Serikali. Serikali ilisema

watendaji ambao waliajiriwa wakiwa darasa la saba walidanganya vyeti waliondolewa kuanzia mwaka 2004, lakini wale ambao walioajiriwa kabla ya hapo waliendelea kufanya kazi. Mwaka huu Serikali inawaondoa hawa watendaji kuleta watendaji wengine, inasema walipewa muda wa kujiendeleza hawajafanya. Sasa watendaji hawa ndio wamesaidia kujenga shule za sekondari, wamesaidia kujenga vituo vya afya, wamesaidia kujenga zahanati, walikuwa hawana muda wa kujiendeleza, naiomba sana Serikali hawa watendaji wengi karibu wanaelekea muda wa kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watendaji hawa waachwe wamalizie muda wao wastaafu kwa amani hawakutenda kosa lolote, hawakusema wako *form four* hapana, waliajiriwa wakiwa darasa la saba.

Kwa hiyo, naomba Serikali iwe na moyo wa huruma, kwenye *human face* iwaache watendaji hawa wamalizie muda wao wastaafu kwa amani kwa sababu wameifanyia kazi Serikali.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika, naomba ukae.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Kiswaga baadae Mheshimiwa Mwalimu Bilago, Mheshimiwa Aida Khenan na Mheshimiwa Rukia Kassim wajiandae.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia nami hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanatheolojia wanatufundisha kwamba ili Mungu akusikilize lazima uanze

kumsifu kwanza. Kwa hiyo, ili Serikali iweze kunisikiliza ni vizuri nikasema mazuri ambayo inayafanya.

Kwanza napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anazozifanya likiwemo hili la ununuzi wa ndege. Unajua historia wanaweza watu wasiifahamu sana. Nchi yetu ilikuwa na ndege ambazo tuligawana kutoka *East Africa* na ndege mpya ikanunuliwa sasa ya Rais na Benjamin William Mkapa. Kwa hiyo, tangu hapo huyu ni Rais wa kwanza kununua ndege mpya za nchi ya Tanzania. Kwa hiyo ni jambo ambalo limeingia katika historia na atakumbukwa milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukafahamu hilo, lakini tujue pia kwamba yale mambo yote yanayofanyika ya kitaifa ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanafikishwa mahali ambapo wanahitaji, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa uhamasishaji wake wa mazao matano ya kibiashara ikiwemo pamba. Ili uchumi ukue ni vizuri mazao ambayo yanaleta uchumi yahamasishwe na kusimamiwa na Serikali. Serikali ya Awamu ya Tano imefanya hivyo chini ya Waziri wa Kilimo pamoja na Waziri Mkuu. Tumepata madawa ya kutosha ya pamba na pamba tunaamini kwamba inaweza kuwa nyingi. Kinachotakiwa sasa ni kuhakikisha kwamba wanunuzi wanapata fedha za kutosha ili mkulima asiweze kukopwa, ni kazi kubwa sana ambayo Waziri Mkuu ameifanya ya kuhamasisha pamoja na kufanya mambo mengine ambayo anayasimamia katika Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanaweza kuwepo maneno, lakini nataka nikwambie kwamba katika zawadi ambazo Mwenyezi Mungu ametujalia Tanzania ni pamoja na kuwa na Kiongozi, Rais wa Jamhuri ya Muungano Ndugu John Pombe Magufuli, Waziri Mkuu Majaliwa pamoja na Makamu wa Rais hizi ni zawadi ambazo Mwenyezi Mungu

ametupa Watanzania, ni vizuri tukawaombea kwa sababu wanafanya kazi ile ambayo wananchi wanaihitaji, ile ambayo hata Mwenyezi Mungu anaihitaji, kwa hiyo lazima tuwapongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwanzo Wafalme wakiendelea walikuwa wanalalamikiwa hivi hivi, Mfalme Daudi alilalamikiwa sana, lakini katika utenzi wake wa nyimbo zake Zaburi ya 34:19 alisema maneno mafupi tu kwamba; "Mateso ya mwenye haki ni mengi lakini Bwana humponya nayo."

Kwa hiyo, tunaamini mateso, mahangaiko ambayo viongozi wetu mnahangaika nayo mnateseka nayo, Bwana Mungu atawaponya nayo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Amen*.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia yale ambayo wananchi wanayahitaji. Ofisi ya Waziri Mkuu ina mradi wa *MIVARP* ambao unaongeza thamani kwa mazao ya wakulima kwa kujenga barabara pamoja na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni muhimu sana umefanya mambo makubwa sana, yako maeneo ambayo wananchi walikuwa hawawezi kusafirisha mazao yao sasa wanasafirisha. Lakini mradi huu sasa ni vizuri ukaendelea. Kwa mfano, kule Magu tunalo eneo bovu sana sasa ambalo tunategemea wakulima wabebe pamba yao kwa tela za ng'ombe kutoka kilometa tano mpaka kilometa kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri *MIVARP* kwa wakati huu sasa maeneo yale ambayo tunataka kusafirisha mazao ikapeleka nguvu za ziada ili ziweze kutengeneza barabara hizo na kuongeza thamani ya zao la mkulima, kwa sababu bila barabara hizo hatutasafirisha pamba yetu kuleta kwenye soko na barabara hiyo ni Ng'haya - Mwabulenga ni barabara muhimu sana kiuchumi na ndiko wananchi pia wanalima mpunga wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiziachia *TARURA* hizi barabara nina imani kulingana na uwezo mdogo wa kibajeti havitatosha. Pia niombe kwenye *TARURA* hapa; mfumo ambao tumeuweka kwenye *TARURA* nadhani si rafiki sana kwa sababu *TARURA* haina bodi sasa, haingii hata kwenye Baraza la Madiwani, kwenye Kamati ya Fedha, je, barabara hizo zinahojiwa na nani? Mpaka twende *Road Board* ndipo tukakutane na matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri ukatengenezwa mfumo wa kiwilaya, ikawepo Bodi ya *TARURA* ya Wilaya ili Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani na viongozi wote wa Serikali waweze kwanza kudhibiti upungufu wa barabara zilizopo kwenye Halmashauri ndipo sasa twende kwenye *Road Board.* Kwa hiyo, naomba sana hilo liweze kuangaliwa kwa makini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mheshimiwa Mbunge anahitaji maji hapa, kila tunaposimama tunahitaji maji; mimi nadhani ni wakati muafaka sasa wa kuangalia kama Taifa. Kama ambavyo hotuba ya Waziri Mkuu imesema kwamba tunao uwezo wa kukopesheka, hivi hatuwezi kukopa tukaweka miundombinu ya maji ili wananchi waweze kupata maji salama kwa ukaribu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali hii ambayo ipo tayari kuwatumikia Watanzania, tukope, tuweke miundombinu ya maji ili wananchi akina mama ambao wanateseka kwa muda mrefu kuchota maji, wanachelewa kwenda kuzalisha shughuli za kiuchumi tuweze kuwawekea mtandao wa maji unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nalalamika kila Bunge ninaposimama hapa, kila ninapochangia hotuba hizi za Waziri Mkuu, TAMISEMI na Maji yenyewe, Waziri wa Maji, Tarafa ya Ndagalu ni kilometa 58 kutoka Magu Mjini, ni kilometa 65 kutoka Ziwa Victoria lakini haina hata mto. Ni Tarafa kame inapakana na kwa Mheshimiwa Chenge kule naye ana shida ya maji, imepakana na Itilima na Maswa kule nako kuna shida ya maji. Ni vizuri tukaangalia namna

ambavyo tunaweza kuisaidia Tarafa hii, ni Tarafa kubwa lakini wananchi wake wanateseka, haina mto wala mabwawa. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana uangalie utakapokuja kwenye bajeti yako uweze kuona utaisaidiaje Tarafa hii ya Ndagalu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la walemavu, bahati nzuri Serikali ya Awamu ya Tano inawajali kikamilifu walemavu na ndiyo maana hata Naibu Waziri ikamteua yule anayelingana na mazingira ya hawa ambao nataka kuwasemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walemavu bado hatujawaangalia sawasawa hasa kwenye mikopo ya uzalishaji mali, tunawaunganisha tu kwenye mifuko ya vijana na wanawake, lakini hii mifuko tungeweka mfuko kwa sababu ya kuwawezesha walemavu ili waweze kujikomboa kwenye biashara ndogo ndogo, wawe na uchumi ambao unaweza kuwasaidia katika maisha yao na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko ya watumishi ambao wakati huo walikuwa wanachangia *NPF* na baadae wakahamishiwa *NSSF* kwamba zile fedha zao walizokuwa wamechangia *NPF* wanapokwenda kustaafu wanategemea *NSSF* itakuwa imeziingiza na zile, wanajikuta hizo fedha hazipo, wanahangaika kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Waziri wa Fedha kwenye jambo hili litazame kwa moyo wako wa huruma maana hawa watumishi wametumika kwa muda mrefu sana, wanapokosa mafao haya wanapata taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mfuko huu wa *NSSF* inaonekana mteja anapochangia kwa maana ya mtumishi, hakuna ongezeko lolote ambalo linaongezeka kwenye mchango wake. Anapokwenda kulipwa mafao yake analipa mafao yale yale, hilo ndilo lalamiko la watumishi wengi hasa waliopo kwenye Idara ya Afya. Niombe sana hili jambo Serikali iweze kuliangalia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kuzungumzia suala la Watendaji wa Vijiji ambao waliajiriwa kwa darasa la saba, hawakuwa na kiwango cha elimu ya sekondari. Hawa wametumika kwa nchi hii na hawa si wengi sana waliobaki, ni vizuri tukawaangalia namna pekee ya kuwasaidia ni kuwarudisha kazini kwa sababu wamebakiza muda mchache. Mambo ambayo wanayafanya yanalingana kabisa na elimu yao, hawa ndio waliojenga shule za msingi, zahanati, sekondari na ndio walinzi wa amani kwenye vijiji hivyo, leo tukiwaacha hawa hiyo ndiyo adhabu yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi yupo hapa, Makatibu Wakuu wapo na Waziri Mkuu yupo, muone namna, hatuna sababu ya kuendelea kujadili Bungeni hapa, ni kutoa waraka tu hata kama ni kesho ili warudishwe kazini wale ili baadaye sasa tuangalie utaratibu wa wale wanaoendelea kuajiriwa wenye sifa zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nataka niwaambie hawa wanafanya kazi...

*(Hala kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Mwalimu Bilago, Mheshimiwa Aida Khenan na Mheshimiwa Rukia Kassim wajiandae.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Bunge lililopita nilisimama hapa na Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2) juu ya kazi za Mbunge, kazi ikiwa ni kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana nishauri Waheshimiwa Wabunge tutimize majukumu yetu ya kikatiba. Hii habari ya kusimama Bungeni na kusifia sifia wakati mambo yanaharibika haitatusaidia kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unashangaa mtu anaunga mkono anasema asilimia mia moja halafu anaweka neno lakini sasa mimi kama mwalimu haiingii akilini; kama una mambo yameharibika ueleze yalivyoharibika tu usianze kutafuta mambo mazuri wakati hayo mazuri hayapo. Kama unaona hayapo hili Taifa ni letu wote; tuisimamie Serikali na kuishauri, ndivyo ambavyo Katiba imetuambia, hii hapa ibara ya Ibara ya 63. Sasa kuna watu humu wanaremba remba wanapamba mambo ambayo hayapo, wanaogopa kuishauri na kuisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninyi Wabunge wa CCM mlikuwa na nafasi nzuri sana ya kuisimamia Serikali yenu inayoongoza ya Chama cha Mapinduzi, maana sisi tukitoa ushauri huku bahati mbaya tunaonekana kama ushauri wetu bado hamuukubali, lakini hatutachoka kusema, tutaendelea kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zote zimekwenda kwenye ukaguzi wa miradi, lakini fedha za miradi ya maendeleo hazikwenda/hazijapelekwa. Ilikuwa ni aibu wakati fulani mnakwenda kwenye mradi hata shilingi moja haijapelekwa, mnakwenda kukagua fedha za wafadhili wengine tu waliojitolea kuleta fedha, ninyi za kwenu nchini hazijapelekwa. Hili nalo tukishauri mnatuona wabaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa tulisimama tukashangilia bajeti hii ya mwaka, ya karne, haijawahi kupatikana, haya ndio madhara yake sasa sisi tuliona haikubaliki ndiyo maana tulikataa kuiunga mkono. Tulikataa kuunga mkono kwa sababu tulijua ni bajeti ya mbwembwe ya maandishi mazuri kwenye karatasi utekelezaji wake haupo, tunafanyaje hii kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia miradi inatekelezwa, fedha za maendeleo kwenye wizara zinapelekwa asilimia 11, asilimia 33, kilimo wamepeleka asilimia 11, hiki kilimo tunakipeleka wapi kama kinapelekwa kwa asilimia 11 tu ya maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bahati nzuri kuna mtu mmoja wa Hazina alikuja akatuambia akasema kwa kweli Serikali ina majukumu mengi, fedha iliyokusanywa ni kidogo na haiwezi kukidhi, hata wafadhili wenyewe waliokuwa wakituletea fedha hawaleti vizuri. Mimi nikahoji tuna mahusiano mabaya na mataifa ya nje? Kama yapo mtuambie uhusiano wetu wa kidiplomasia umekuwaje mpaka wafadhili walioahidi kuleta fedha hawaleti fedha nchi hii? Kwa hiyo, hili lazima tulione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni Wabunge humu, tusione tu Serikali ni kuisifia, tuishauri, wapo watu hapa, mimi napongeza naliona jambo zuri la ununuaji wa ndege, lakini sio kununua ndege kwa *cash.* Mataifa yote hayanunui ndege kwa *cash*, hii *cash* ingeweza kufanya shughuli zingine za maendeleo tukanunua ndege kwa mkopo ndege ikawa inalipa deni la ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndege ya mwisho iliyokuja tuliwahi sisi wapinzani kusema nje kwamba kuna ndege imeshikiliwa, lakini waliosema ndege imeshikiliwa walipata misukosuko, juzi Serikali imekiri ndege iliyokuwa imeshikiliwa Canada sasa imeletwa. Mimi napata wakati mgumu, tulipowaambia imeshikiliwa tulipata msukosko, imerudi mkakiri wenyewe iliyoshikiliwa imerudi sasa... *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege hii imekuja kama ndege moja tumenunua ndege tatu, kuna ndege moja ya bilioni 31 ambayo ndio hii iliyokuja ikaonekana baada ya kushikiliwa muda mrefu, lakini ili itoke tumelipa bilioni 78 sawa na fedha za Kitanzania bilioni 140 na kidogo ili hiyo ndege moja ipatikane. Sasa watu tunaposhangilia ni lazima tujiulize tumeumia kwa kiasi gani? Unanunua ndege moja kwa bilioni karibu mia moja na hamsini halafu tunalishangilia hilo, hapa

watu tuna matatizo ya maji na kiafya hatulioni hilo wala hatuishauri... *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Tuishauri Serikali...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**T A A R I F A**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa muongeaji anayeongea kuwa ile ndege haijanunuliwa mamia ya bilioni kama anavyosema. Hayo mahela aliyolipwa ni kwa ajili ya watu wanaodai, lakini sio manunuzi ya ndege.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umri wangu na aliyetoa taarifa haulingani, kwa hiyo, naachana nae kwa sababu ya umri nilionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri mzuri tu ambao unaweza ukatusaidia kwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye upande wa Wizara ya Elimu. Tunalo tatizo la uhaba wa walimu, hali ya uhaba wa walimu ni kubwa sana, tuna tatizo la upungufu wa walimu wa shule za msingi, walimu shule za msingi hawatoshi, tuna upungufu karibu wa walimu 95,000.

Vilevile bado tuna tatizo la walimu wa sayansi, walimu wa sayansi karibu 15 na *point* hawatoshi. Hivi viwanda tunavyohubiri katika nchi yetu bila walimu wa sayansi ni viwanda gani? Kwa sababu tunaweza kutafikia hatua; mimi sijui kama kuna kiwanda kinaendeshwa na mtu aliyesoma *history* na *geography* aka-*run* mitambo ya viwanda na hivyo viwanda vikawa salama na mwenyewe anayekiendesha akawa salama. *(Makofi)*

Tuchukue hatua za makusudi kunusuru taifa hili upande wa elimu. Walimu wamekata tamaa morali ya kufundisha imeshuka. Taarifa ya Haki Elimu inasema walimu waliobaki na morali ya kufundisha ni asilimia 37, hawa 60 na kidogo wote wamepoteza morali wa kufundisha kwa sababu tu ya kukosa motisha. Wana madai mengi hawalipwi, wamebaki kulipa wanadokoa dokoa. Mwezi wa pili tulidhani walimu watalipwa wote, walidokoa dokoa wakalipa baadhi ya walimu, hivi hii hali tunaipeleka wapi Taifa hili? Kama hatutakuwa na elimu nchini hakuna sekta ambayo itakwenda vizuri, sekta zote zinategemea elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufaulu sasa hivi *division four* na *division zero* ni asilimia 60 na *point,* yaani mimi hata sielewi ni ufaulu kwa sababu *zero* si ufaulu hata *four* yenyewe si ufaulu yaani waliopata *four* na *zero* ni asilimia 60 yaani tunatarajia nchi iendeshwe na asilimia 30 ndio uwezo kidogo waliofanikiwa darasani *division one, two* na *three, where are we heading to?* Halafu tunakaa humu tunasifia, tunapongeza, tupongeze lakini tuisimamie Serikali, tuinue ubora wa elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii tuliwahi kufikia hatua jamani tuwe na mkutano wa kitaifa wa elimu na bahati nzuri juzi alizungumza Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa akasema hali ya elimu ni mbaya tuwe na mkutano wa kitaifa kuliangalia hili. Naomba hili tuliangalie kwa pamoja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago naomba umalizie kwa dakika moja, muda wako umeisha.

**MJUMBE FULANI:** Bado tatu...

**MWENYEKITI:** Makatibu wanasema ni ya pili, kwa hiyo mimi namuongezea dakika moja amalizie.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia suala la utawala bora. Kwenye suala la utawala bora tuzungumzie habari ya Tume Huru ya Uchaguzi, kama hatutakuwa na Tume Huru ya Uchaguzi hatutakuwa na utawala bora hapa nchini, na hili ndilo limetufikisha hapa. Nafurahia maoni ya Kamati yaliyosema Tume Huru ya Uchaguzi iangalie wale wasimamizi wa uchaguzi waendeshe uchaguzi kwa uadilifu. Ile habari ya kila chaguzi ndogo zinazofanyika ni mauaji, ni fujo, vurugu na uporaji wa kura na matokeo mnaambiwa nendeni mahakamani, hatutaki; uchaguzi ufanyike ulio huru tuepukane na mahakama. Hii habari ya tunauliza humu....

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bilago, nashukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Aida Khenani baadaye Mheshimiwa Rukia Kassim na Mheshimiwa Hassan Masala wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, lakini na mimi napenda kupongeza mzungumzaji aliyetoka kuzungumza sasa kwa kutimiza wajibu wetu kama Wabunge kwa kuwa ni muhimili unaojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia hotuba ya Waziri Mkuu cha kwanza tunaangalia uhalisia wa Watanzania. Tukitazama uhalisia wa Watanzania tumeangalia jambo la msingi ambalo ni maisha ya kawaida wanayoyaishi kila siku. Maisha waliyonayo Watanzania hayaendani na hiki kilichosomwa au kilichoandikwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hali ya maisha ni ngumu sana. Tunapozungumza kwamba hali ya uchumi ni nzuri wakati Watanzania hali yao ni mbaya, tunaomba hayo

maandishi yaende kwenye uhalisia kwa Watanzania, hali ya maisha haifanani na kile kilichoandikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ajira mpya tunatazama vijana wengi ambao wamemaliza vyuo wapo mtaani. Leo vijana wetu wanajiingiza kwenye vitendo mbalimbali ambavyo si makusudi yao, ni maisha. Leo tumetazama taarifa mbalimbali hasa kwa jana, yaani imefikia mahali mpaka makanisani sadaka zimeanza kuibiwa. Hatutasema ni vijana peke yao ndio wanaoiba, lakini ni vyema Serikali ikajielekeza kwa kuangalia kundi kubwa la Watanzania ambalo ni vijana linawapeleka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi viongozi wetu wapo Segerea, tumeenda kutazama kule robo tatu ya wafungwa waliopo kule ni vijana, na hapo inajidhihirisha kabisa kwamba Tanzania suala la ajira imekuwa ni kidonda ndugu sasa. Ni vyema kama tunategemea kuleta amani tunayoizungumza kwenye Taifa letu tukatazama kundi kubwa la Watanzania na tukatafuta suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka kwenye Mkoa wa Rukwa ambao tunategemea kilimo, kilimo hicho ninachokizungumza ndicho ambacho Watanzania wengi tunategemea kuendesha Taifa. Leo wamesimama Wabunge wengi wakazungumzia kuhusu ununuzi wa ndege, si jambo baya, lakini ni wakati gani umenunua na je ndio uhitaji mkubwa wa Watanzania? Watanzania wangapi ambao watafaidika na hiyo ndege? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anaulizwa Mkurugenzi wa *ATCL* leo amesema nje ya kupanda ndege Watanzania watanufaika kuuza vipuli; mambo haya ni fedheha kwa Watanzania. Ni kweli ndege ingenunuliwa lakini kwa kuangalia kipaumbele cha Taifa letu ni ndege? Ni kweli taifa letu kipaumbele cha kwanza ni ndege?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapouzungumzia Mkoa wetu wa Rukwa ukiacha suala la usafiri wa anga kuna usafirishaji wa majini. Amezungumza Keissy pale kuhusu meli,

hiyo meli imekuwa ni wimbo. Meli ile ingewasaidia Watanzania wa kawaida hata kufanya biashara, kutoa mazao yao Mkoa wa Rukwa na maeneo mengine kupeleka hata nchi ya Congo; lakini leo ni Mtanzania gani wa Rukwa atakuja kupanda ndege hiyo iliyoletwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mkumbuke unapozungumzia ndege huzungumzii wananchi wa Dar es Salaam, unazungumzia wananchi wa Taifa la Tanzania na hizo ni kodi za Watanzania wote. Tungeomba mambo ambayo tunakuwa tunazungumza kama Wabunge yachukuliwe kama vile tunavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafikia mahali tunapata shida sana, kwamba hivi tunazungumza kwa kutimiza wajibu au tunazungumza kama mhimili ambao tunatakiwa tuisimamie Serikali? Kwa sababu yale tunayozungumzia hayawezi kwenda kama vile tunavyozungumza na mnakuja hapa matokeo yake sasa watu wamejaa hofu. Niwaombe Mawaziri, hata Mungu ni mkubwa lakini ana washauri wake ambao wako chini sana, Malaika; kaeni na Mheshimiwa Rais mumshauri uhalisia wa Taifa letu na Watanzania wanakabiliana na nini. Mkiwa waoga tukija hapa tutazungumza kumbe mkifika kule mnakuwa na hofu mnashindwa kutimiza wajibu wenu wa kumshauri Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza hivi, kabla hatujapitisha bajeti tayari bei ya petrol imepanda, bei ya mafuta ya taa imepanda, bei ya dizeli imepanda. Sasa unaanza kujiuliza huu uchumi uliokuwa ina maana shilingi ya Tanzania imeshuka thamani. Sasa hii tunayozungumza hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua hata mama yangu ameondoka lakini yupo Naibu Waziri pale; tunapozungumza kama Wabunge angalau basi muwe mnafungua masikio mnatusikiliza tunachokizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema hapa, tulizungumzia mambo ya petroli hapa, tulizungumza mambo ya mafuta ya taa; hivi leo ukipandisha bei kwenye petroli

unategemea Watanzania wangapi wanaoathirika? Hiyo inakwenda kuwaathiri moja kwa moja Watanzania wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha Watanzania wanaishi vizuri kwa kupewa mambo yao ya msingi. Mlipo kuja hapa mkazungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama kama Waziri, kama Kiongozi wa Serikali akazuia wakulima wasipeleke mazao yao nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni haki yenu na ni wajibu wenu kama Serikali kuhakikisha taifa lisipate njaa, lakini kama unaweza kupata nguvu ya kuzungumza kuzuia kwa nini usipate hiyo nguvu ya kuhakikisha Watanzania wanapata soko la uhakika la kuuza mazao yao? Kama hatujui pembejeo zao, yaani mpaka Mheshimiwa Rais anaweza kuzungumza kwamba sasa mnataka mbolea ziende wakati Waziri wa Kilimo yupo, tafsiri yake ni nini? Waheshimiwa Mawaziri wote mmeshindwa mpaka yeye aseme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa tumeenda kuwahamasisha, Mheshimiwa Rais amezungumza watu wafanye kazi, tumeenda kuwahamasisha wafanye kazi, wamekwenda kuchukua mikopo benki, wamezalisha kilimo cha kisasa, wakazalisha kwa wingi. Matokeo yake hivi ninavyozungumza kuna wakulima wameuziwa nyumba zao, kuna wakulima wanadaiwa na benki kwa sababu ya uzembe wa Serikali. Kwa sababu ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wakulima wake wanapata masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mtanzania wa kawaida amekwenda kuathirika kwa uzembe ambao umetokana na Serikali yenyewe. Kwa nini msiwasimamie wale mnaowalipa mishahara, mnawasimamia hawa ambao hatujui wamepataje pembejeo, hatujui wamefanyaje kuweza kupata hicho chakula? Hata viwanda tunavyoviimba ni viwanda ambavyo vitabaki kwenye historia tu kwenye maandishi, huwezi kuzungumzia viwanda wakati umeshindwa kuimarisha kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia viwanda ni lazima leo kama Serikali mjiwekeze, mhakikishe kabisa kwamba kipaumbele cha sasa ni kilimo, hivyo tutabadilisha wakulima wetu kwenda kuweka kilimo cha umwagiliaji, waachane na kilimo cha mazoea. Leo unasema asilimia kumi ndiyo mliyopeleka, huu ni utani, utani sana tu. Na tunapozungumza tukizungumzia Serikali tunazungumzia Chama cha Mapinduzi, ndicho chenye Serikali na Wabunge wanaposimama kuzungumza lazima wajue chama chao ambacho kinaongoza Serikali kimesababisha maumivu makali kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uvuvi, yaani leo ikitokea kipindupindu kimetokea kwenye Mkoa wangu wa Rukwa, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, wakulima pamoja na wavuvi wameenda kuchomewa nyavu zao pamoja na makazi, yaani leo hakuna njia ya kudhibiti kipindupindu mnawachomea watu makazi yao. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imewafikisha Watanzania mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani alikwambia kudhibiti kipindupindu ni kuchoma makazi? Yaani leo mmekosa kabisa njia mbadala ya kuzuia kipindupindu mnawaondoa watu wakawe maskini? Haya mambo ikifikia mahali kuna watu hawawezi kusema, sisi tuliotumwa leo kama wawakilishi wao kusema tukisema msiposikia kuna wakati mwingine watasema kwa milango ambayo hamtajua wanasemea wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye utawala bora na unapozungumzia utawala bora lazima uzungumzie utawala wa sheria. Leo unapozungumzia Mbunge wa chama cha upinzani ni kama unazungumza mtu ambaye ni adaui wa Taifa. Msajili wa Vyama vya Siasa kazi yake ni kulea vyama vya siasa, leo amekuwa muuaji wa vyama vya siasa. Katiba mpya imeelekeza maandamano ni haki ya Kikatiba, yeye anapaswa kuwaambia kwamba mnataka kuandamana kwa sababu gani, ameona kuna mvurugano wa vyama asimame katikati kuhakikisha vyama vinakwenda salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo CHADEMA wanaandamana, anasema ni kwa nini nisiwafutie usajili, na anajua Katiba inaelekeza kwamba maandamano ni haki ya msingi. Mbona wale wanaoandamana kumsifia Rais hawaambiwi waondoke nchini? Ila wewe ukiandamana kwa kutaka kumkosoa Mheshimiwa Rais wewe ni adui wa Taifa hili. Utawala bora bado kwa Tanzania ni jambo ambalo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Khenani. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Rukia Kassim, Mheshimiwa Julius Kalanga ajiandae na baadae Mheshimiwa Hassan Masala.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kuweza kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza na ukurasa wa 12; Serikali kuhamia Dodoma. Hili ni jambo jema sana Mheshimiwa Rais kuamua kama sasa kweli Serikali ihamie Dodoma, lakini nahisi bado Manispaa ya Dodoma haijajielewa kama Rais katoa amri hii kuwa Serikali ihamie Dodoma. Hivi ninavyosimama hapa hakuna *stand* ya magari, mabasi yanahangaikahangaika tu, wameondolewa hapo wamepelekwa Kilimo Kwanza, huko Kilimo Kwanza ni eneo la Jeshi ambalo wameliazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kama kweli Serikali imeamua kuhamia Dodoma wao bado hawajaliona hili na wakaanza kutayarisha kuwa hili ni eneo la ku-*park* na basi na eneo lingine waweke kwa ajili ya magari madogo madogo? Hiace zinarandaranda tu hapo barabarani, lakini

hawana *parking* za kukaa wala za kuweza kuchukua abiria. Hili ni tatizo, kwa hiyo naiomba Serikali waieleze Manispaa na wajielewe kwamba Serikali sasa imehamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuna viukuta hivi vya *road reserve,* hivi vimekuja mpaka kufikia nadhani Kilimo Kwanza, hapa katika mji havipo, lakini kuna viwanja ambavyo bado ni vitupu na wenyewe watajenga, kwa hiyo kama hawakuviweka mapema watu wakijenga wataingia katika eneo la *road reserve* baadae itabidi kuvunjwe. Kwa hiyo, mimi nawashauri wajipange na wajielewe na waweze kuweka vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mitaro ya majitaka; bado haijarekebishwa vizuri. Tunayaona maji yanasambaasambaa hovyo tu. Tatizo hili limejitokeza Dar es Salaam, Dar es Salaam wakati mji ule ulikuwa na watu wachache mitaro ya majitaka ilikuwa inakidhi haja kwa idadi ya watu waliokuwepo kwa wakati ule, lakini hivi sasa kama hawakuwaza kuliweka mapema na wakajua kwamba huu utakuwa ni mji wakaanza kutayarisha mitaro hiyo ili ikidhi haja ya watu watakapokuwa wengi, italeta shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo hili la mji hapo ambapo kuna vichochoro vile, kuna barabara za mitaa, zile barabara ni nyembamba mno utafikiria ulimi wa paka, hawajarekebisha, watu wanavunja majumba ya zamani wanajenga, lakini bado hawajaweka ile mitaa iongezeke, yaani walau gari ziweze kipishana. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali, mtu yeyote ambaye atajenga sasa katika eneo la mji kwanza ianze sheria kuwa ajenge ghorofa na waache nafasi ambayo itasaidia magari yaweze kupishana katika ile mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege, uwanja uliopo hapa ni aibu, ule si uwanja, sijui hata ni kitu gani, useme ni uwanja wa *volleyball* au sijui useme kitu gani. Serikali imepanga kujenga uwanja Msalato, kwa hiyo, mimi naishauri Serikali waanze kujenga ule uwanja Msalato ili aibu hii

iondoke. Wakianza kujenga uwanja kwa sababu sasa hivi mji umeanza kukua kuna Mabalozi wamehamia hapa, kuna maafisa chungu nzima wa Serikali wako hapa, sisi Wabunge tuko hapa, lakini uwanja uliopo ni mdogo, ndege kubwa haziwezi kutua, kwa hiyo hii ni aibu. Mimi naishauri Serikali waanze kujenga uwanja wa Msalato ili tatizo hili liondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa manispaa tunawaomba, sisi watu tunaokaa *Area D, Area D* sasa hivi imekuwa ni kisiwa. Ukitaka kwenda *Area D* mpaka uzunguke Mji wote wa Dodoma ndiyo uweze kufika. Kwa hiyo, mimi nawasauri angalau mle kandokando ya ule uwanja watutengenezee japo kijinjia kidogo magari yaweze kupita, wanaokwenda *Area D* isiwe kama ni watu wanaokwenda katika mji mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo najielekeza sasa katika vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria akimshauri Msajili wa Vyama vya Siasa vyama ambavyo vinakiuka maadili na Sheria ya Vyama vya Siasa vifutwe. Jambo hili si jema na ninaomba lisije likatokea katika nchi yetu, kwa sababu unapokifutia chama usajili ni kuwafanya wale walio na chama sasa,kwa sababu chama kile sio cha viongozi, chama ni cha wananchi wote; unapounda chama hata mkiwa ni wachache mmeunda kile chama lakini ni sawa na kujenga msikiti au kanisa, utalijenga baadae likikamilika muumini yeyote anayekwenda kusali pale tayari ana haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hivi vyama vya siasa sio vya viongozi, ni vyama vya wananchi, vitakapofutwa itabidi wale wanaofanya siasa sasa watakapokosa pa kufanyia watakwenda kufanya katika misikiti, kwenye nyumba za ibada, makanisa, hii itakuwa ni shida kubwa na italeta tatizo kubwa katika nchi. Mimi namshauri Msajili kama ni mlezi wa vyama chama kinapotokea matatizo awaite na awashauri na si kuwafutia usajili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimemsikia Mheshimiwa Mchengerwa akisema katika hotuba ya Kamati yake kumshauri Msajili wa Vyama vya Siasa aendelee kutatua matatizo kusaidia kusuluhisha tatizo lililopo katika Chama cha Wananchi *(CUF).* Mimi ni Mbunge kupitia *CUF,* nakiri kweli kuna matatizo katika Chama cha Wananchi *(CUF)* ambayo yamesababisha hata sisi wenyewe humu ndani hatuelewani, ni bora mtu wa chama kingine unamuona ni mwema zaidi kwako kuliko yule wa chama chako, hili ni tatizo. Na tunamuomba Msajili aendelee kutushauri na kutupatanisha kwa sababu mwisho wa yote haya ni matatizo kwetu. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa; Mheshimiwa Rukia subiri.

**T A A R I F A**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Msajili ameshtakiwa hana nafasi ya kufanya suluhu katika jambo hili; yeye mwenyewe mshtakiwa atafanya suluhu na nani? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi hayo maneno yake ya kisimani siyataki, nataka aongee maneno ya Kibunge. Msajili ana haki, Msajili ndiye mlezi wa vyama kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sheria Na. 5 ya mwaka 1992…

**MBUNGE FULANI:** Bwege!

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** …Sheria ya Vyama vya Siasa, inampa mamlaka Msajili kuvishauri na pia kushughulikia

vyama vya siasa. Kwa hiyo yeye ikiwa anasema Msajili kashtakiwa, kashtakiwa na nani na kwa sheria gani? Mimi nadhani hayo maneno ya kisimani akayasemee Kilwa, si humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Atakapoweza kutatua tatizo hili litatusaidia lakini inaonekana kuna baadhi ya watu hawataki, lakini mimi naona tu hawajajijua kwa sababu kama wanajijua, Profesa ndiye Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi *(CUF)* na ndiye mwenye mamlaka ya kuweza kuteua na ku... *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWNYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Khatib.

**T A A R I F A**

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampa taarifa muongeaji kwamba Mheshimiwa Profesa anayemuita Mwenyekiti wakati chama hiki yeye hayupo uchaguzi wa Kinondoni, Chama cha *CUF* tulipata kura 70,000 na kushinda jimbo, lakini leo yeye Mwenyekiti anayemtambua amepata kura sawa na mwaka aliyozaliwa, 1943, nampa taarifa hiyo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siwezi kulumbana na vi-*comedy;* huyo ni *comedy* katika Bunge hili. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Hatujasikia hiyo, Mheshimiwa arudie!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane jamani.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Hatujaskia vikobe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia, endelea.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nasema huyo ni *comedy* katika siasa. Na ninamuomba u-*comedy* wake akaufanyie kule Konde, si katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa ni Mwenyekiti kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Wananchi *(CUF).* Kama wao wanasema kwamba Profesa alijiuzulu anapojiuzulu Mwenyekiti au Katibu Mkuu au Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Katiba ya *CUF* mpaka mamlaka iliyomchagua ikubali, iridhie kujiuzulu kwake, kikao hicho hakikufanyika na Profesa alirudia nafasi yake kama Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kwa hiyo, namuomba kama ni Mbunge kupitia Chama cha Wananchi *(CUF)* amheshimu na ajue kwamba ni Mwenyekiti wake, na akiendelea na huo utumbo kuna Kamati imeundwa ambayo ni ya maadili ambayo mimi ni mjumbe wake, tutamshughulikia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Ashughulikiwe Khatib huyo!

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Rukia, muda wako umemalizika, ahsante, nashukuru. Tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aongeze dakika moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mimi kusema katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze katika hili suala la watumishi walioachishwa kazi, hasa wale watendaji wa vijiji, wa kata na madereva. Mimi naomba tu Waziri atuambie; hivi utu wa kibinadamu katika jambo hili umezingatiwa kwa kiwango gani? Kwa sababu kama Waziri ambaye anasimamia sekta hii na anayesimamia utaratibu huu anajua kabisa kwamba watumishi hawa waliajiriwa na Serikali miaka hiyo kwa sababu kulikuwa kuna uhitaji wake, lakini kwa sababu Serikali sasa imeona labda hawahitajiki tena imeamua kuwa-*dump* na kuwatupa kama watu ambao hawajawahi kulitumikia taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnatengeneza visa na chuki ambazo ni janga katika Taifa letu na kwa kweli hii laana ya watumishi ambao mliwachukua kwa uhitaji wenu, kwamba njooni fanyeni kazi mkiwa darasa la saba, mkiwa kidato cha nne, hawajaweza kujiendeleza kwa sababu ya mazingira pia, halafu leo mnawaondoa kazini na vilevile hamlipi stahiki zao wala hamsemi, kwa kiburi hiki, hakuna ambaye atabaki salama kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni muhimu mkatuambia hawa watumishi wanastahili au hawastahili. Kwa sababu mliwaajiri ninyi kwa sababu mlikuwa mna uhitaji, mlijua viwango vyao vya elimu na baadhi yenu hao madereva wa darasa la saba mliowaondoa waliwaendesha ninyi katika kutimiza majukumu yenu. Lakini leo kwa sababu mmepata uhitaji mmepata wengine mmewaacha hata hamtaki kulipa stahiki zao mnaamua kujadili siku mnayotaka; tunataka Serikali ituambie maslahi ya watumishi hawa walioondolewa kwa sababu ya kiwango cha elimu, maslahi yao na stahiki zao wanapewa lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, acheni uonevu kwa sababu hawa mliwachukua ninyi kwa sababu mlikuwa mnawahitaji. Leo mnawaondoa hata pensheni zao hamtaki kuwapa, leo mnawaondoa hata kuzungumza nao hamtaki kwa sababu mmemaliza kazi, mmewatumia halafu baada ya kuwatumia mmeamua kuwatupa na hili mmefanya hivyo makusudi kwa sababu mnafikiri mna dola, mna nguvu ya kuwatumia na

kuwafanya mnavyotaka. Ni muhimu mkasema kama wana haki wapewe na kama hawana haki basi muwaambie kuliko kufanya kama hisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili nawashangaa katika Hotuba hii ya Waziri Mkuu anasema Serikali inaendelea kutatua migogoro katika sekta binafsi na katika maeneo mbalimbali. Mnapata wapi *moral authority* ya kutatua migogoro kama ninyi mnafukuza kienyeji bila kufuata utaratibu? Unakwenda kumsuluhisha nani wakati wewe mwenyewe hufuati utaratibu huo katika kufukuza watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni muhimu mkaelewa kwamba ninyi mmekosa uhalali wa kusuluhisha migogoro katika nchi hii kwa sababu hata ninyi hamfuati sheria na utaratibu katika kuwaondoa watumishi kazini. Watumishi wa Umma hawa mnawanyima ruhusa kwenda kusoma lakini mnataka muwaambie wajiendeleze, wajiendeleze kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu sio ubinadamu na wala haufai kabisa, Waziri ambaye na wewe ni binadamu na una watoto unadiriki kushiriki katika dhambi ya namna hii ya kudhulumu watu jasho lao walilotumikia nchi kwa zaidi ya miaka 15 eti kwa sababu ni darasa la saba, lakini waliwaendesha katika mapori mkitafuta kura na vilevile mkifanya majukumu yenu, leo mnawaondoa bila kuwazingatia, huu si ubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili, ukisoma katika Hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 35, imezungumzwa habari ya ujenzi wa viwanda na hili ni jambo jema sana na mimi napenda kulipongeza kama ni la ukweli. Hata hivyo mnavyozungumza viwanda mnasema mmejenga viwanda 3,306 lakini ukiwauliza hawa Wabunge ni Mbunge gani hata mmoja anaweza akasimama, hata kumi kuonesha viwanda vilivyojengwa kwenye maeneo yao? Hakuna hata mmoja. Hivi viwanda mnajenga wapi? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa rafiki yangu Julius Kalanga Mbunge wa Monduli na namtajia majina ya viwanda *Googwill Industry* kiko Mkiu Mkuranga moja, *Lodhia Industry* kiko Kisemvule, Mkuranga mbili, *Rhino Cement* kiko Kisemvule, Mkuranga tatu, *yes!* Na kadhalika na kadhalika.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba mimi kwangu peke yangu Mkuranga tuna viwanda zaidi ya 80 na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga katika mapato yale ya *service levy number one* tunapata kutoka katika viwanda vilivyopatinaka katika Awamu hii ya Tano ya Mheshimiwa Rais JPM, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii angenipa Mbunge wa kawaida ningeweza kumuelewa, yeye anatetea nafasi yake na taarifa hii haieleweke kwa sababu nchi hii si Mkuranga peke yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema haya kwa ajili ya lengo la kujenga nchi yetu, tunataka Serikali ituonyeshe viwanda hivyo 3,306 viko wapi kwa majina na vinanzalisha nini ili sisi Wabunge tuweze kushuhudia Serikali katika hili jambo, ndiyo dhana yetu.

Lakini la pili tunataka viwanda vioanishe na maisha ya Watanzania, unajenga viwanda lakini unasema hakuna masoko wakulima hawa hivyo viwanda mnalisha nini kama malighafi haitokani na Watanzania wanaofanya kazi? Ni muhimu mkatuambia ni zao gani leo ambao mmezalisha viwanda zao hilo limepata soko na wakulima wamefaidi

nchi yao kwa sababu viwanda vimechukua zile malighafi, mnatengeneza viwanda vya *white elephant* alafu baadae nchi yetu ibadilike kuwa dampo la bidhaa kutoka kwa ajili ya kulisha viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Serikali ituambie viwanda hivyo vimejengwa wapi msituambie hii habari, nimesikia jana mtu anasema eti mashine ya kukoboa na kusaga mahindi ni kiwanda, mnasema brenda ni kiwanda, mnasema cherehani tatu ni kiwanda naona Mheshimiwa Naibu Waziri ananipiga taarifa lakini kwa wakati wake ana nafasi ya kujibu...

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msiwape Naibu Mawaziri nafasi ya kutupa taarifa, wajibu majibu baadae.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri taarifa

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kwanza asiupotoshe umma. Viwanda hivi vimekuwa *categorized* kwa mujibu wa sera yetu ambayo inasema kila kiwanda na *level* zake.

Kwa hiyo, aanze kwenye msingi wa sera ndipo atakapoweza kuelewa haya ambayo anayakataa sasa hivi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Julius.

**MHE. JULIUS K LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe na Mawaziri mvumilie mtajibu, kwa nini mnakosa hata Wabunge wakuwatetea subirini mtajibu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba lengo letu ni jema tu, tunataka viwanda hivi visaidie unafuu wa maisha ya Watanzania tunataka mtuambie hiyo sera inayosema ina *categorization* viwanda mlete *categorization* ya viwanda hivyo kulingana na sera mnayosema, tatizo liko wapi? Kama cherehani ni kiwanda semeni, kwa sababu mnasema eti ikiwaajiri watu watatu ni kiwanda, cherehani kuna yule anayekata nguo na anayeshona ni kiwanda tayari mtuletee hizo *categorization.* Tunataka viwanda vya nchi vioanishe na maisha ya Watanzani ili malighafi tunayozalisha sisi tupeleke kwenye viwanda vyetu, leo mnazungumzia kwenye... *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** taarifa Mhehsimiwa Peter.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nilitaka nimpe taarifa mchangiaji kwamba tangu Uhuru nchi hii tulikuwa na vyerahani, tulikuwa na mashine ya kukoboa ambayo Serikali ya Awamu ya Tano sasa inaita viwanda na kushangilia, nilitaka nimmpe taarifa. *(Makofi)*

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa hii, sekta ya mifugo ambayo inaajiri Watanzania asilimia 50 pamoja na...

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Julius subiri kidogo taarifa huku.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utunze muda wangu.

**MHE. OMARY T MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji...

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba utunze muda wangu.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Morogoro vijijini na yeye mwenyewe alishuhudia Kiwanda cha Philip Morris kinatengeneza sigara na inatumia malighafi za Tanzania tumbaku kutoka Tanzania kipo Morogoro na kimeshaisha na Mheshimiwa Rais wiki mbili zilizopita aliendа kuzindua, kimejengwa kwenye kijiji cha Pangawe Kata ya Mkambarani Halmashauri ya Morogoro vijijini. *(Makofi)*

Kiwanda cha pili ni cha kuchakata mbaazi; kutokana na matatiizo ya bei ya mbaazi mwaka jana 2017 Serikali ya Awamu ya Tano imepata mwekezaji, kinajengwa kwenye jimbo langu katika kijiji cha Mtego wa Simba sasa hivi kiwanda kimekwisha na mwaka huu 2018 kitaanza kuchakata.

Kiwanda cha tatu nimpe kiwanda cha kutengeneza Sukari cha Mkulazi chenye uwezo wa kuzalisha tani zaidi ya laki mbili, mashine zimeshafika na Mkurugenzi ameenda kupokea bandarini leo kinaenda kufungwa, nilitaka kumpa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Imetosha, Mheshimiwa Julius endelea.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu. Mimi siweze kushabikia, kwanza ni kiwanda cha kutengeneza kansa kwa wananchi halafu kiwanda ni cha zamani, ni sawa sawa umejenga shule ukijenga darasa jipya unaona umefanya maendelezo mapya unafungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukaelewa, ukizungumza taarifa hii Wizara ya Mifugo, sekta ya mifugo imezungumzwa chini ya maneno 100, sekta ambayo inagusa

asilimia kubwa ya Watanzania, imezungumzwa kwa kiwango ambacho nusu *page* halafu imezungumzwa kupiga chapa hivi ng'ombe ni chapa? Nchi ya pili Afrika kwa uzalishaji wa mifugo unazungumza habari ya chapa, ndiyo sera ya Serikali inakuja kuzungumza kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamheshimu sana Mheshimiwa Mbunge, ninaomba tu afuate utaratibu na ajue kwamba mfumo wa uwasilishaji bajeti ndani ya Bunge hotuba ya Bajeti Mheshimiwa Waziri Mkuu na wakati anaiwasilisha hapa mbele alisema, hotuba yake inatoa mwelekeo tu kwa ufupi wa sekta zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Bunge hili litakaa hapa kwa takribani miezi mitatu na kila sekta itapata nafasi sasa ya kueleza kwa kina katika kila eneo ni nini ambacho kimefanyika kwa ukubwa wake na matokeo ya utekelezaji katika kila sekta. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, labda Mheshimiwa Mbunge angeelewa kwanza utaratibu tunapokezana yeye ataendelea tu na Mheshimiwa Kalanga usiwe na haraka utaendelea tu.

Kwa hiyo, ninachotaka kumueleza Mheshimiwa Kalanga ni kwamba asubiri wala asiwe na presha, na Kanuni zinakataza kuwahisha mijadala asubiri tu itakapofika Wizara husika ataelewa mambo yote ambayo yametekelezwa

kwenye sekta ya mifugo na sekta nyingine, mimi nilikuwa naomba nimpe hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo ndio chapa? Nimesema taarifa iliyozumnguzwa huko unazungmza habari ya chapa hivi mwelekeo ya Wizara ya Mifugo kwetu sisi wafugaji ni chapa? Ndiyo mwelekeo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuelekeza, chapa ndicho tunachosema katika eneo hilo hatujatendewa haki kama sehemu ya ufugaji wa nchi hii. Tunamahitaji mengi hakuna maeneo ambayo imeelekeza tufanye nini, mnatuambia chapa, milioni mbili sijui ngapi, mnaharibu ngozi, mmeleta sheria halafu mnazungumza badala ya kutusaidia tupate malisho, maeneo ya nchi hii ni mapori mmeshindwa kutupa ameneo mnazungumza chapa, halafu tupige makofi, hatuwezi kupiga makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema jambo langu la mwisho, kuhusu upatikanaji wa fedha katika miradi ya maendeleo na hili ni muhimu sana Serikali ikajua Wabunge tunataka nini. Mimi nafikiri ni muhimu kwa sababu mmeshindwa kupeleka fedha za miradi ya maendeleo, tuchague vipaumbele vya miradi michache halafu tukaitekeleza tukawa na miradi ya mfano, hutasikia tukigombana kwenye hili Bunge kama kila Mbunge atasema mlikuwa mmependekeza kutengeneza mradi wa maji na akauona mradi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaleta hapa *figure* za maneno ili kuionesha nchi mnayo fedha, lakini kwenye maendeleo ya miradi yetu hamtuletei fedha, miradi imebaki viporo. Tunaomba kama Serikali ina nia ya kusaidia wananchi tuangalie vipaumbele vya kila Halmashauri halafu tupeleke fedha hata kama ni mradi mmoja, lakini ukakamilika ukawanufaisha wananchi. Lakini zaidi ya hivyo mkiwa mnaongeza kila kitu trilioni hizo trilioni za kwenye karatasi hazitusaidii sisi, tunayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kalanga muda wako mmelindwa na umetosha tayari kwa sababu umeshazungumza na tumeulinda muda wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Masala, baadae Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Amina Mollel wajiandae.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa pongezi kwa Serikali kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na wanaendelea kuifanya. Vilevile naomba nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wa hotuba yake. Watanzania wanaona, Watanzania wana akili, lakini ambacho wenzetu walikuwa wanakililia na ndicho ambacho Mwenyezi Mungu ametujaalia, sisi tunaendelea kumuombea Mheshimiwa Magufuli kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote ndugu zetu wa upande wa pili walitaka Mheshimiwa Rais ambaye atathubutu, Rais ambaye atakwenda kutenda, kwa hakika Mheshimiwa Magufuli anatenda na sisi Wabunge wake tuko nyuma yake tunawa-*support* Waheshimiwa Mawaziri wetu kwa kazi nzuri ambayo wanaifabnya ya kuwatumikia Watanzania na hatimaye naamini Watanzania wale wale watakwenda kufanya maamuzi mwaka 2020 kwa kadri wanavyoendelewa kutumikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naomba nichukue nafasi hii kutoa ushauri; yako baadhi ya maeneo ambayo kwenye bajeti ya mwaka jana nilisimama hapa nilishauri, lakini niishukuru Serikali yangu kwa sababu baadhi ya mambo mengi wameyafanyia kazi na kwa

wakulima wetu sisi ambao tunawawakilisha yameanza kuleta tija kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliotangulia wa Mikoa ya Lindi na Mtwara wamezungumzia sana masuala ya elimu, kilimo, miundombinu, nishati na maeneo yote yanayohusu huduma za kijamii. Mimi naomba nijielekeze kwenye eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulitoa mapendekezo ya kusaidiwa wakulima wetu kupata pembejeo hasa *sulphur* bure na Serikali yetu sikivu ilifanya hilo zoezi kwa kutoa *sulphur* na pembejeo nyingine kwa wakulima wetu. Uzalishaji ulipanda na wakulima wetu wamepata tija kubwa sana kwa zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kutoa hizi *sulphur* na pembejeo nyingine bure bado yako maeneo ambayo tulifikiri ni muhimu tukaendelea kushauri, tukamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya Kilimo waangalie namna ambavyo wanaweza sasa ku-*fast track* ili wakulima wa maeneo haya waweze kupata pembejeo kwa haraka iwezekanavyo. Hapa tunapozungumza leo ni mwezi wa nne tayari watu wameshaanza maandalizi ya mikorosho. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana watu wa Wizara ya Kilimo waharakishe upatikanaji wa pembejeo ili wakulima wetu waweze kuhudumia mikorosho yao kwa wakati ili waweze kuendelea kuzalisha na hatimaye tuliingizie taifa letu kipato kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka pia nishauri ni eneo ambalo linahusu malipo. Utaratibu ambao umetumika kwa msimu wa mwaka jana 2017 toka tumeanza utaratibu huu mpya wa stakabadhi ghalani ulioboreshwa bado kuna baadhi ya makampuni ambayo yamekuwa yanachukua korosho za wakulima yameendelea kuchelewesha malipo kwa wakulima wetu. Yako baadhi ya maeneo mpaka sasa hivi baadhi ya makampuni hawajamaliza kulipa fedha za wakulima ambazo

zimeshauzwa toka mwaka jana wakati ambapo minada ilishafungwa toka mwezi wa kumi na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na timu yake watie mkono katika kuhakikisha makampuni yote ambayo yalichukua korosho za wakulima wanamalizia kulipa malipo ili wakulima waweze kupata nafasi ya kuhudumia mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nilishauri Serikali yetu ni eneo la ufufuaji wa viwanda. Katika jimbo la Nachingwea tunacho Kiwanda cha Ubanguaji wa Korosho ambacho kwa muda mrefu hakifanyi kazi. Pia kupitia Wizara yetu ya Viwanda ambayo tayari nilishakwenda kufuatilia walitupa maelekezo ya kufufuliwa kwa viwanda vyote ambavyo vilishakufa tangu muda mrefu. Korosho inayozalishwa katika maeneo haya tulipenda sana ipate thamani kubwa zaidi kwa kubanguliwa katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wawekezaji ambao wameingia ubia na baadhi ya vyama vyetu vikuu ikiwemo *Lindi Farmers*. Hata hivyo bado uwekezaji ambao unaendelea kule haujakaa vizuri, kupitai Wizara ya Viwanda Mheshimiwa Waziri lakini pia watu wa kilimo naomba watie mkono waone wale wawekezaji wa *Sunshine* ambao wamechukua viwanda vya Nachingwea, Mtama pale pamoja na maeneo mengine ya Newala waweze kuona nini ambacho kinaendelea ili ikiwezekana katika msimu huu wakulima wetu waweze kubangua korosho na kuipandisha thamani ili tuweze kupata pesa kubwa zaidi ya hii ambayo tunaipata sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nilishauri ni eneo la stakabadhi ghalani katika mazao mengine. Tunakwenda kwenye msimu wa kilimo cha ufuta Mkoa wa Lindi tumeadhimia kuingiza ufuta safari hii katika stabadhi ghalani. Niombe Wizara ya Kilimo ione namna inavyoweza kuhamasisha na kuangalia mikoa mingine yote inayolima ufuta ili tutakapoanza kwenda kutekeleza mfumo

huu basi ukae katika misingi ambayo itakuwa haitoleta shida na haitopishana kati ya mkoa mmoja na mkoa mwingine; na hii kwa sababu kipindi cha nyuma ufuta umeuzwa kwa kila mkoa kwa utaratibu ambao si ule ambao tumeuzoea wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tulishakuja kwako mwaka jana na mwaka huu sisi tumeshapitisha katika vikao vyote tulikuwa tunafikiri ni wakati wenu sasa kama Wizara muone namna ambavyo mtasimamia ili tuhakikishe mfumo huu utakapoanza kwa msimu huu basi uwe ni *uniform* katika maeneo yote yanayolima ufuta, lengo likiwa ni lilelile kuongeza tija kama ambavyo tunafanya vizuri katika zao la ufuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitajka nilkizungumzie ni eneo la zao la mbaazi. Mwaka jana tumelalamika sana juu ya changamoto za bei kwa zao la mbaazi ambalo wakulima wetu wengi wamechangamkia na kuiona fursa. Mheshimwa Waziri wakati anakuja hapa tulimuomba atupe ufafanuzi, lakini pia atueleze namna ambavyo wale wanunuzi hasa Wahindi ambao waliingia mkataba walivyojipanga kwenda kununua mbaazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunapata shida kidogo kuwahamasisha wakulima wetu juu la suala la ulimaji wa mbaazi kwa sababu bado hatujawa na uhakika. Kipo kitengo ambacho kinashughulika na utafiti ndani ya Wizara ya kilimo, tunaomba kitengo hiki sasa kitoe maelekezo; kitoe dira lakini pia watupe uhakika wa masoko ili tuweze kupata nguvu ya kuwahamasisha wakulima wetu kama wanaweza wakaendelea kulima mbaazi kama zao la biashara au walime kama zao la chakula kama ambavyo tulikuwa tunafanya kipindi cha nyuma. Jambo hili nafikiri litatusaidia ili kuweza kuondokana na kile ambacho kimejitokeza miaka miwili mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pilli ambalo nilitaka nichangie ni suala zima la miundombinu ya barabara. Hatuwezi kujadili maendeleo hatuwezi kupanga mikakati

mizuri kama hatuwezi kuangalia hali ya barabara zetu. Kwa mwaka jana barabara ya Masasi - Nachingwea - Nanganga, tulitengewa shilingi bilioni tatu na milioni mia tano; nimefuatilia sana na ninaendelea kufuatilia sana. Hiki ni kilio cha wanachi wa jimbo la Nachingwea ambao wanapakana na Wilaya ya Masasi, wanapakana na Wilaya ya Ruangwa, Liwale. Barabara hii ni barabara ya kiuchumi; naomba niwaombe watu wa Wizara ya Ujenzi ya waone namna wanavyoweza kwenda kuanza utekelezaji wa ahadi ambayo wamenihaidi kwa miaka miwili sasa mfululizo; kwamba ujenzi utaanza na anatafutwa mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa jimbo la Nachingwea na maeneo yote ya jirani wamenituma na wanaendelea kunisisitiza kuendelea kuiomba Serikali yao sikivu iweze kuanza ujenzi huu kwanza kwa kulipa fidia, lakini pili kwa kuanzisha ujenzi ambao sasa utatusaidia kusafirisha mazao yetu bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiondoa barabara hii iko barabara inayotoka Nanganga kwenda Ruangwa kwenda kutokea Nachingwea barabara hii tayari usanifu umeshafanyika tunasubiri ahadi ya kuanza utekelezaji wa ujenzi wa kiwango cha lami. Iko barabara inayotoka Nachingwea kwenda Ruangwa kuunganisha Kiranjeranje; ni barabara ambayo ikifunguliwa nayo itakwenda kufungua uchumi wa Mkoa mzima wa Lindi kwa sababu Wilaya ya Nachingwea na Wilaya za jirani ndizo Wilaya ambazo zinaongoza kwa kusafirisha na kutoa mazao ambayo kimsingi yanaletea faida kubwa sana taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo la nishati. Hali ya upatikanaji wa umeme katika mikoa yetu si mzuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia sentensi yako, muda wako umeishisha.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana kupitia watu wa Wizara mashine walizozileta Lindi waende wakazifunge, muda tuliokaa kusubiri unatosha sana. Tumepewa miezi minne umeme utakwenda kutatuliwa, lakini muda huo ni mwingi tunaomba Wizara wazifunge zile mashine ambazo tayari wameshazileta ili tukae tuwe na umeme wa uhakika ambao utatuwezesha kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana na ninaomba nionge mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masala, tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo na baadae Amina Mollel ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze kiujumla Serikali na hususani Waziri Mkuu ambaye amewasilisha hii bajeti pamoja na timu yake Mheshimiwa Jenista na Manaibu Mawaziri kwa kutukuka kwenye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwenye eno moja ambalo watu wengi na hasa upande wa pili kule wanaona uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati kama ujenzi wa reli, ununuzi wa ndege na kazi nyingine ambazo Serikali ya Chama cha Mapainduzi inafanya, wanaona kwamba mpangilio wa rasilimali haukuwa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano, Wabunge waliopo hapa ndani wengi wamekopa pesa, wamewekeza katika kujenga ma-guest *(guest houses),* kujenga nyumba za kupangisha, magari, wanafanya biashara ili wapate faida na wafanye shughuli zingine. Kwa hiyo, kwa upande wa Serikali kuweza kununua ndege na kuboresha usafiri wa ndege ndani ya nchi yetu inasaidia na sekta zingine, mojawapo tutapata faida. Ili tuweze kuongeza mapato ya Serikali lazima

tuboresha usafiri wa ndege ili na watalii wetu waweze kufika maeneo mbalimbali ya nchi. Kama vile Mkoa wetu wa Katavi tuna Mbuga ya Katavi, Nyanda za Juu Kusini vipo vituo vingi tu lakini tatizo ni miundombinu ya kuwafikisha watalii wetu na wananchi mbalimbali. Pia usafiri wa ndege unasaidia mtu unakuwa *in efficiency* unakwenda kwa wakati na wengi mnapanda ndege kama vile *Fastjet* ilivyoingia na kubadilisha *mind* za watu kwamba usafiri wa ndege si ghali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika masuala ya reli; ukiangalia kwa mfano treni inayotoka Tabora kwenda Mpanda inatumia lita 1000, sasa tukiboresha hii njia na kutumia umeme maana yake gharama za uendeshaji itashuka na matokeo yake nauli zitakuwa nafuu na usafirishaji wa mizigo kwa hiyo itakwenda kukuza uchumi. Kwa hiyo, mnapoona kwamba mikakati ya Serikali inafanyika katika maeneo mbalimbali ni mtambuka na kusaidia sekta zingine na kushusha gharama. Kwa hiyo, ni kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunajua chini ya Ofisi ya Waziri MKuu wanashughulika na Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu nitagusa hayo maeneo kama ifuatavyo:-

Ningependa sana niunganishe upande wa kazi pamoja na vijana. Tunajua kabisa asilimia kubwa ya Watanzania ni vijana na wengi wanahitaji kuweza kupata ajira na maeneo mengi kwa mfano Jimbo la Nsimbo asilimia 95 ya wananchi wanashughulika na kilimo. Sasa ningeomba kwa upande wa Serikali tujaribu kuangalia kwenye sekta ambazo zinatoa ajira kubwa upande wa kilimo. Ni jinsi gani tutahusisha kuboresha kilimo katika nyendo zake pamoja na hali ya hewa kwa sababu tunategemea tu mvua moja, sasa namna gani tutalima mara mbili na kuongeza hayo maeneo ili tuendelee kuboresha upande wa ajira.

Mheshimiwa Mwneyekiti, sambamba na kilimo, tunajua kaulimbiu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika hii Awamu Tano ni kwenda kwenye nchi ya viwanda, sasa

malighafi ya viwanda tulivyonavyo inahitaji pia malighafi kutoka upande wa kilimo. Sasa hivi viwandani vinavyohitaji malighafi za upande wa kilimo tunahakikisha kwamba tunafanya nini. Kwa sasa hivi tuna viwanda vingi vinavyotumia malighafi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukienda kwenye ngano, mafuta ya kula. Tuchukue tu mfano Bakhressa ambaye anatoa ngano na tunapata unga, sasa asilimia kubwa ya malighafi ya Bakhressa inatoka nje ya nchi, sasa kwa kiasi gani tunakwenda kuwavutia wawekezaji upande wa kilimo na kuwashawishi wananchi wetu waweze kulima hizi kwa ajili ya viwanda ambavyo tayari vinatumia malighafi za kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa upande wa mafuta ya kula, asilimia kubwa tunaagiza kutoka nje. Ni jinsi gani tutapunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje na tuweze kujenga zidia ajira zetu upande wa vijana na wananchi katika Tanzania yetu. Kwa hiyo, tuombe Serikali huu mkakati unakwenda kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la upande wa umeme vijijini. Bahati mbaya hatuwezi kuingiliana kwenye kuzungumzia mihimili, lakini naomba tu tuseme Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma kwa umeme vijijini, Mkandarasi kesi iko mahakamani kila siku inasomwa haijaanza kusikilizwa. Sasa ni lini itakamilika ili wananchi waingie kwenye kupata huduma ya umeme kama ilivyo azma ya Serikali? Kwa hiyo kwa namna nyingine basi na mhimili mwingine uone jinsi gani ya kuharakisha hiyo kesi ili miradi ya maendeleo kwa upande wa umeme vijijini ikatekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo mwaka jana tuliibadilishia sheria na tuliweza kutoa tozo na kuweka nafuu chini ya tani moja, lakini tulisahau kwenye bidhaa ambazo hazidumu kwa muda mrefu *(perishable goods)*. Sasa ni jinsi gani utaitoa shambani ukaitunze nyumbani kama vile nyanya, hoho, mboga mboga? Hapa tulipasahau kupaangalia. Sasa tumekuwa nachangamoto kwa

wakulima wanakuwa wanatuhoji kutokana na kauli na maelekezo ya Serikali kutokutoza chini ya tani moja unapotoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Mwenytkiti, tatizo tulilonalo ni kwenye mboga mboga na bidhaa nyingine ambazo hazidumu *(perishable goods).* Kwa hiyo, Serikali naomba mliangalie, na nashukuru Mheshimiwa Jafo nimeshamtaarifu na barua nimeshamwandikia, basi lishughulikiwe kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu walemavu; kama Sheria Namba 9 ya mwaka 2010 ilivyo, kuna Mabaraza ya Kata nao wawezeshwe katika ile asilimia 10 ambayo inakwenda kwa vijana, akina mama pamoja na walemavu asilimia mbili. Tuwe na uwezeshaji wa miradi ya moja kwa moja kwa ajili ya kusaidia walemavu ili waweze kujiongezea kipato na waache utegemezi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbogo

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanye, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Mollel na baadae Mheshimiwa Mattar Ali Salum na Justin Monko wajiandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Seriakli yetu kwa kazi nzuri inayofanya, na hapa nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais kwa jitihada anazofanya katika kuwatetea wanyonge wa taifa hili; Waswahili wanasema kwamba mti wenye matunda ndiyo unaopigwa mawe na hili tunalishuhudia. Nimpongeze pia

Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, nimpongeze sana Dada yangu Jenista Mhagama kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na wasaidizi wake Mheshimiwa Ikupa pamoja na Mheshimiwa Mavunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia hotuba hasa katika ukurasa wa 24 ambako kumezungumziwa huduma kwa watu wenye ulemavu. Tumeona jitihada za Seriakli katika kusaidia kundi hili la watu wenye ulemavu, na nitoe pongezi za dhati kwa jitihada zinazofanywa. Kwa mfano, tumeshuhudia kuanzia mwaka jana vifaa kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum vimepelekwa katika shule mbalimbali ingawa bado uhitaji ni mkubwa, kwa hiyo, niisisitize tu kwamba Wizara kuendela kuangalia na hasa maeneo mengi ya vijijini kwa kweli bado uhitaji ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia kwa kuona umuhimu wa kuboresha vyuo vya watu weye ulemavu, kwa mfano Chuo cha Yombo ambacho kilikuwa ni msaada mkubwa sana katika kuwajengea uwezo, kuwapa ujuzi watu wenye ulemavu ambao walikuwa wakitoka hapo wanakwenda kujiajiri wao wenyewe na si kutegemea tena ajira.

Kwa hiyo, hiki chuo ni muhimu sana na niisisitize Wizara katika kuhakikisha kwamba kweli wanaboresha na kukirudisha katika ule ubora uliokuwepo pale awali na kuongezea pia na wakati huu tulionao hivi sasa wa karne ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize tu pia kwamba katika vyuo hivi mbali ya chuo hiki cha *VETA,* lakini tuone pia katika Vyuo vya *VETA* ambavyo tunaona kabisa kwamba vinazalisha vijana na vinawajengea uwezo. Katika vyuo hivi nitoe mfano tu ambapo katika kipindi kilichopita nilikuwa Mjumbe katika Kamati ya *PIC* ambako tuliweza pia kukutana na *VETA.* Mimi masikitiko yangu ni kwamba *VETA* kwa kweli hawana kipaumbele kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, hapa nisisitize Serikali kuhakikisha kwamba vyuo vyote

hivi vinajali kundi hili ili kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo kuwapa ujuzi wakitioka pale waweze kwenda kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu asilimia mbili; tangu jana pia tumeona hata katika maswali ya Waheshimiwa Wabunge tumeona uhitaji wa kundi hili. ni kweli kabisa kwamba katika bajeti ya mwaka jana, Waziri alitoa ahadi na alitoa tamko kwamba sasa ile asilimia 10; asilimia nne iende kwa wanawake na asilimia mbili iende kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu. Sasa hili lilikuwa ni tamko, ninasisitiza na kuona uhitaji kwamba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa tunahitaji sheria, kwa sababu kukiwepo na sheria, sheria hii itatoa muongozo, itawaelekeza wakurugenzi na hakuna Mkurugenzi ambae sasa ambaye atafanya kwa utashi wake bali atafanya kwa kzuingatia kanuni, sheria na taratibu zilizopo kwa ajili ya watu hawa wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye ulemavu kwenye mabenki hawakopesheki na hawakopesheki kwa sababu dhana iliyopo miongoni mwetu bado watu wengi wana ile dhana potofu ya kuona kwamba huyu mwenye ulemavu hawezi kurudisha huo mkopo, kwa hiyo, hii asilimia mbili mimi nasisitiza tuone umuhimu kwamba hili ndilo kimbilio lao, ndilo tegemeo lao kwa kuwapa asilimia hii mbili waweze kujiajiri kwa kufanya biashara mbalimbali.

Tumeshuhudia; hizi zitawawezesha wao kuondokana na hali ngumu ya maisha na wakati wenyewe uliopo hivi sasa. Kwa hiyo nasisitiza umuhimu na ninaomba sana dada yangu mpendwa, dada mkubwa Jenista Mhagama utakapokuja hapa basi uje kutupa majibu na nitafurahi nikisikia ni tamko na utueleze kama ni sheria au kanuni na taratibu zitaandaliwa lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Wizara hasa Ofisi yangu hii ya Dada yangu Jenista Mhagama kwa jitihada wanazofanya kwa kuhakikisha kwamba kundi la vijana linawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kilimo, kilimo hiki tunaangalia ni kwa namna gani tunawawezesha vijana, vijana ndiyo nguvukazi ya Taifa. Vijana hawa mikopo ambayo ipo na tumeona kwamba mikopo hiyo baadhi wamekuwa wamefaidika na vijana wengi hivi sasa wanahamasika tuone sasa ni kwa jinsi gani tutawajengea hawa vijana na kuwapa hii mikopo wajiingize kwenye kilimo. Kilimo chenyewe ambacho tunakihitaji hivi sasa ni kilimo cha kisasa, kilimo biashara. Kilimo hiki biashara kitawawezesha vijana waweze kujiajiri wao wenyewe na kupunguza basi lile tatizo la ajira. Kwa mfano, hizi *green house* ni muhimu sana, vijana wengi tumeshuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakiwezeshwa kwa kupitia hii mikopo na vijana hawa wakaandaliwa mafunzo kupitia ujasiriamali mbalimbali wataweza wao wenyewe, kwa sababu kikubwa kinachohitajika pia ni elimu. Katika kilimo wakiwezeshwa; tunaona kwamba kuna ufugaji wa kuku, kuna ufugaji wa samaki vyote vinaingia katika kilimo biashara. Kwa hiyo naisisitiza sana na naiomba sana Serikali tuone umuhimu wa kuwawezesha vijana hawakwa kuwapatia hiyo mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia kwamba program ya kuwawzesha vijana katika Vyuo vya *VETA,* tuangalie sasa, tunapokwenda katika sekta ya utalii kwa wenzetu utaratibu mzuri wanaoweka ni haa kuhakikisha kwamba vijana hawa kwa mfano, wanaofanyakazi katika sekta hii ya utalii wanapata elimu ambayo *customer care* ni muhimu sana. Ukienda nchi za Kenya jinsi ambavyo wenzetu wanavyoweza kuhudumia ile *customer care* ni muhimu sana; kwa hiyo na sisi huku kwetu kama tumedhamiria kuona kwamba tunawawezesha vijana wetu kwenda katika mafunzo hayo kwa mfano kupitia programu ya Chuo cha Utalii, vijana wetu watumike kupata ujuzi lakini pia wafundishwe jinsi ya ule ukarimu wa kuwapokea wageni wanaofika hapa. Tunafahamu sekta ya utalii ni pana na inaongeza pato katika nchi hii, kwa hiyo, tuwawezeshe katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, kuwepo na programu, kwa mfano; Wizara hii husika kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu hata madereva *taxi* wapatiwe mafunzo, kwa mfano wanapokwenda kumpokea mteja ajue ile namna gani ya kuweza kumpokea mteja kwa ukarimu ili kwamba anapoondoka ibaki ile sifa yetu kuwa Watanzania kama ilivyo kwamba sisi ni wakarimu. Kwa hiyo, kwa kupewa mafunzo hayo hata hawa madereva *taxi* watajua, hata mgeni kama anasahau kitu kwenye gari ni rahisi sana kuangalia ni kwa namna gani ya kuweza kumsaidia huyo mgeni anayefika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie katika ukurasa wa 18, suala la ajira. Ninasisitiza ni kazi nzuri, mpango mzuri ambao umeandaliwa wa kukusanya kanzidata kwa wahitimu wenye mahitaji maalum. Nasisitiza tena kwamba wapo vijanaa wengi wamemaliza vyuo vikuu wenye ulemavu, wasioona, viziwi na wengine wengi tuone kwamba ile asilimia tatu inazingatiwa siyo kwa Taasisi za Serikali tu hata katika *private sector.* Sasa hivi tupo katika suala zima la viwanda, katika viwanda hivi je, tunawaandaaje watu wenye ulemavu ili na wao basi waweze kuingia huko, wapate ajira na kuweza kufanyakazi huko kuhakikisha kwamba tunawaondoa katika dimbwi kubwa la umaskini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Amina, nimekuachia kidogo muda wako kengele yako ilipiga.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu tafadhali naomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arumeru katika kijiji, Kata ya Oldonyowasi maji yenye *fluoride* yanatuumiza watu wa kule. Ukienda kule utakuta watoto wanapinda miguu na wazazi/wamama na vikongwe wanapinda migongo. Naomba sana watalaam mbalimbali

wameshafanya utafiti tatizo ni kubwa naomba sana. Na Mheshimiwa Dada yangu Jenista utakapokuja naomba pia utueleze kwa sababu mwaka jana tumeona Waziri Mkuu kweli ametupatia mradi na kwa mara ya kwanza ndani ya miaka 50 tumepata maji. Kwa hiyo, naomba sasa katika Kata hii ya Oldonyowasi tuone ni kwa jinsi gani tunaweza kupunguza tatizo la madini ya *fluoride.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Amina, tunamalizia na wachangiaji wawili Mheshimiwa Mattar Ali Salum na Mheshimiwa Justin Monko kwa muda wa dakika tano tano.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini la pili nimpongeze sana Rais Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo anafanya. Vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu kwa kazi ambazo anazifanya, ni haki yake kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika mchango, kwa kuwa dakika zangu ni kidogo nigusie katika watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Niiombe Serikali yangu tukufu, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanapata taabu sana katika kupata matibabu yao. Niombe sana kila Halmashauri iweze kutenga fedha kiasi cha asilimia mbili au asilimia tatu wapewe watu wanaoishi na maradhi ya UKIMWI ili waweze kuunda vikundi ili waweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili kwa kuwa kuna mifano ambayo imetoka, baadhi ya Halmashauri wamepewa nafasi hizi na wamepewa fedha hizi wameweza kujiendeleza kwa makini na wameweza kujiwekeza kupata mpaka kadi za matibabu wao wenyewe na mitaji yao imekuwa mikubwa. Nimuombe Mheshimiwa Waziri kama hawa watu watapewa fedha kutokana na Halmashauri zetu na kuwe kuna sheria maalum ambazo Halmashauri hizi zilazimike kuwapa pesa watu hawa ili waweze kufikia hatua tunayotaka. Tukiwapa fedha tutaondoa utegemezi mkubwa kwa watu wenye kuishi na maradhi ya UKIMWI kwa sababu

wanaweza kujitegemea, lakini Serikali inahitaji lazima iweze kuwainua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niligusie sana hili suala la watu hawa wanaoishi na maradhi ya UKIMWI na wanaoishi na VVU, hata ukitoa fedha kwenye mfuko wa Waziri Mkuu wakipewa hawa watu basi wanaweza kujiendesha kwa hali kubwa sana na wana uwezo mkubwa sana. Nimuombe Dada yangu Jenista aliangalie kwa makini ili aweze kuzi... Halmashauri zote ziweze kutoa fedha kwa watu wenye kuishi naVVU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika jambo la pili, suala la miradi ya maji. Miradi ya maji ndani ya nchi yetu inakwenda vizuri na uendaji wake vizuri ni kutokana na fedha za Mfuko wa Maji ambayo si fedha za bajeti. Fedha za bajeti zinazokwenda bado ni kidogo sana na niiombe Serikali iweze kuewekeza pesa za maendeleo za bajeti katika Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fedha zetu za Mfuko wa Maji ambazo ndizo tegemeo kubwa katika miradi yetu ya maji. Sasa tuiombe Serikali iweze kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge ili kuongeza shilingi 50 iwe shilingi 100 ili wananchi wetu waweze kupata huduma ya maji kwa makini. Mimi nashangaa sijui ni kwanini Serikali inapata kigugumizi kuongeza hii shilingi 50 ili itimie shilingi 100 ili Wananchi wetu waweze kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilielekeza kabisa maji ni muhimu, sasa tunashangaa kama Serikali haiwezi kukubaliana na sisi Wabunge ambao tumetumwa na wananchi tuje kwenu ili tuweze kuiambia Serikali kwa yale ambayo tunayoyataka, tunashangaa Serikali inapata kigugumizi wakati hao wananchi wenyewe ndiyo wanataka hii fedha iongezwe ili wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na suala lingine la kilimo; sera ya nchi yetu imejielekeza katika uchumi wa viwanda. Ni kweli ni sera nzuri ambayo inaleta matumaini

makubwa, lakini ili uchumi wa viwanda uende vizuri lazima kuwe na kilimo bora. Sisi mpaka sasa nchi yetu tuna ardhi nzuri ya kilimo, lakini hatujakaa vizuri katika suala la kilimo. Kwa hiyo, tukikubaliana kuimarisha kilimo cha uhakika basi ninaamini hivi viwanda ambavyo tunavyovitaka vitakuwa vinafanyakazi kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia suala la mradi wa kilimo hasa upatikanaji wa pembejeo, Mheshimiwa Waziri na Bunge lako tukufu lilipitisha uhakika wa unuaji wa mbolea wa pamoja lakini mpaka hivi sasa ule uendeshaji, upatikanaji wa zile mbolea bado ni tabu haujakuwa sahihi na kwa sababu moja, kwa kuwa leo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo yupo ananisikia nimshauri nia halisi ya kufanya ili aweze kufika hatua hawa wakulima wetu wasiweze kupata taabu. Mheshimiwa Waziri nikushauri jambo dogo tu, huu ununuaji wa mbolea ni mzuri, una sifa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar malizia sentensi yako.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** ...Mheshimiwa Waziri ununuaji wa mbolea mzuri. lakini uweze kununua mbolea kwa wakati wote usingoje msimu wa kilimo ndipo uanze kuagiza mbolea. Hii mbolea inatakiwa iwepo kila wakati humu madukani Mheshimiwa Waziri... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Justin Monko.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna inavyoshughulika na masuala ya wananchi kupitia bajeti zake na kupitia watendaji wake wote kwa ujumla. Kwa sababu ya muda wangu mfupi nitajaribu tu kueleza niliyoyaona katika bajeti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kilimo; bado kuna tatizo kubwa kwamba tuna uwekezaji mdogo saa wa kilimo. Tunayo maeneo makubwa, mazuri ambayo yanafaa kwa kilimo, tunayo mabonde mazuri ambayo yanafaa katika kilimo cha umwagiliaji, lakini tunachokifanya sasa hivi ni kufanya umwagiliaji kwenye bahari, kumwagilia maji kweye mito, lakini kilimo cha umwagiliaji bado hakijawa na tija katika nchi yetu.

Kwa hiyo, niiombe sana Serikali ijaribu kuwekeza hatuwezi kwenda kwenye hatua ya viwanda ambayo tunazungumza na tumesisitiza kwamba viwanda vyenyewe lazima viwe ni viwanda ambavyo vitatokana na malighafi za ndani. Malighafi hizo ni za kilimo na tumekuwa na uwekezaji mdogo sna katika sekta ya kilimo.

Katika masuala ya elimu, katika hotuba ya Waziri Mkuu tumeona katika masuala ya elimu kwa kweli udahili wa wanafunzi umeongezeka kwa asilimia zaidi ya 35, lakini miundombinu yetu katika shule za msingi hata katika sekondari kwa kweli ina changamoto kubwa. Zipo shule nyingi katika Jimbo langu zina matatizo. Iko shule moja ya Mikuyu ina madarasa mawili, ina choo ambacho ni cha muda, lakini ina darasa kuanzia chekechea mpaka darasa la sita na haina hata ofisi ya walimu, lakini shule hii imesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko shule nyingine ambayo iko Mighanji katika Kata ya Ngimu. Shule hii ina wanafunzi wengi, wako wanafunzi wanasoma wanatoka zaidi ya kilometa 11 kwenda kwenye hiyo shule. Wananchi

wa vitongoji vya Ngaramtoni wamejitolea kujenga shule lakini bado haijapata usajili. Wanayo madarasa manne lakini sasa hivi imeshindwa kusajiliwa kwa sababu haina lipu, haina sakafu na bado tumeacha watoto wetu wale wadogo wanaendelea kutembea kwa zaidi ya kilometa 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa ukichanganya na tatizo la upungufu wa walimu, kwa kweli limeleta shida sasa katika Jimbo langu na ndiyo mtaona hata matokeo yaliyopita kwa kweli Jimbo letu limefanya vibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia shule za sekondari. Tunayo matatizo ya maabara, maabara nyingi katika Jimbo langu hazijakamilika na nilipotembelea katika Jimbo lile nimeona nyingi zinahitaji fedha karibu shilingi milioni 90 kumalizia. Ni nyingi na suala hili sasa hivi katika bajeti ya Halmashauri yenye makusanyo ya ndani ya shilingi bilioni 1.3 haiwezi kufanya jambo lolote. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali ifanye mkakati wa makusudi katika kuhakikisha kwamba inasaidia kumalizia ujenzi wa hizi maabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niangalie katika suala la afya. Suaa la afya katika Jimbo langi la Singida Kaskazini poa ni tatizo kubwa. Nina vijiji 84 lakini tuna zahanati 32 tu. Vituo vya afya vilivyopo ni viwili, Kituo cha Mgori na Kituo cha Ilongero. Vituo hivi havitoi huduma ya upasuaji. Kwa bahati mbaya sana vituo vyote viwili havijapata fedha za ukarabati kama ambavyo katika halmashauri nyingine zimepata.

Kwa hiyo, niiombe sana Serikali ifanye haraka kwa sababu Halmashauri hii haina hata hospitali ya wilaya tunategemea Hospitali ya Mtinko ambayo ni hospitali ya *mission* na wananchi wanapata matatizo sana katika masuala ya matibabu. Viko vijiji vinafuata matibabu kwa zaidi ya kilometa 40. Kiko Kijiji cha Mkulu ambacho makao makuu yake ya kijiji ni kilometa 26. Viko vitongoji vitatu ambavyo viko Mkulu, lakini kijiji chenyewe ni cha Nduamuhanga kiko kilometa 26; na huko ndiko ili zahanati.

Ukitoka hapo ni lazima ukatize kwenye pori, kwenye hifadhi au upite katika Wilaya ya Chemba. Tunahitaji kwa kweli kupata msaada kwa sababu wananchi wale wanahitaji kupata msaada wa haraka ili kusudi waweze kuepukana na matatizo na kuokoa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la barabara. Jimbo la Singida Kaskazini lina mtandao wa barabara wa kilometa 772.39...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monko malizia sentensi yako tunakamilisha leo.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, lakini kinachosikitisha barabara hizo zimejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa asilimia 8 tu, yaani kilometa 68 kati ya hizo 774.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali iweze kutenga fedha katika bajeti hii inayokuja kuhakikisha kwamba Jimbo hili linasaidiwa. Hatuwezi kuendelea kuwa na barabara za udongo kwa zaidi ya asilimia 91 katika karne hii. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Monko.

Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo, nawashukuru wote kwa michango yenu na kazi nzima ambayo tumefanya kutwa ya leo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3:00 asubuhi

*(Saa 1:45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 6 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*